# KINAYA KAMA NJIA YA KUBAINISHA MAUDHUI: MIFANO KUTOKA RIWAYA YA *CHOZI LA HERI* NA TAMTHILIA YA *KIGOGO*

**MWANIKI MILKAH WANJUGU**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KARATINA**

**OKTOBA, 2023**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu asili wala haijawahi kuwasilishwa kwa madhumuni ya shahada yoyote katika chuo kingine.

**MTAHINIWA**

Sahihi………………………….. Tarehe…………………………..

**MILKAH WANJUGU MWANIKI**

**E303/2356P/15**

**WASIMAMIZI**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa minajili ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu Cha karatina.

**Prof. Joseph Nyehita Maitaria**

Idara ya Sanaa na Lugha

Shule ya Sanaa na Sayansi za Jamii

Chuo Kikuu cha Karatina

Sahihi…………………………………. Tarehe……………………………..

Dkt. Peter Kinyanjui Mwangi

Idara ya Sanaa na Lugha

Shule ya Sanaa na Sayansi za Jamii

Chuo Kikuu cha Karatina

Sahihi………………………………… Tarehe………………………………

# IKISIRI

Kinaya ni mbinu muhimu ya kimtindo ambayo hutumiwa na waandishi wa riwaya na watunzi wa tamthilia kuwasilisha ujumbe wao katika kazi za fasihi. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa: Kuchunguza matumizi ya kinaya kama mbinu ya kimtindo katika kubainisha maudhui na wahusika katika matini mbili za fasihi ya Kiswahili ambazo ni: riwaya ya Assumpta K. Matei ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* ya Pauline Kea. Malengo ya utafiti yalikuwa; moja, kubainisha aina mbalimbali za kinaya katika kazi teule za fasihi; mbili, kueleza jinsi kinaya kimetumika kuendeleza maudhui katika matini mbili teule za fasihi ya Kiswahili; tatu, kueleza jinsi kinaya kinavyotumika katika kujenga sifa za wahusika katika kazi teule. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Kimtindo pamoja na mihimili yake ambayo iliongoza kila sura ya utafiti huu. Nadharia hii inaeleza kwamba ili kuielewa kazi ya fasihi, msomaji anafaa kuelewa kuhusu mbinu za lugha ambazo zimetumika. Utafiti huu unaangazia mbinu ya kinaya vile imetumika katika kubainisha maudhui kama vile uongozi mbaya, ukatili, unafiki na ufisadi. Miongoni mwa waasisi wake ni Coombes (1953). Riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* ziliteuliwa kimakusudi kwa msingi wa utajiri wao wa kinaya. Ili kupata data katika utafiti, mtafiti alisoma vitabu, nadharia, na majarida yanayohusiana na mada ya utafiti. Utafiti ulitumia muundo wa utafiti wa kimaelezo. Mjadala wa vikundi lengwa uliohusisha washiriki wanne pamoja na mtafiti ulitumika kukusanya data kutoka katika matini teule. Data ilichanganuliwa kwa misingi ya malengo ya utafiti. Utafiti unabainisha kuwa kuna aina mbalimbali za kinaya katika kazi za fasihi. Hizi ni: Hali, drama, mazungumzo, kilimwengu, na kinaya cha kisokratiki. Utafiti pia unadhihirisha kuwa vinaya vya hali, mazungumzo na drama ndizo msingi katika ukuzaji wa dhamira na wahusika katika matini mbili teule. Utafiti huu ulihitimisha kuwa kinaya huwa muhimu katika fasihi kwa kuwa hutumika katika kubainisha maudhui hasi katika jamiii kwa kuonyesha matendo maovu ya wahusika wanayotenda kinyume cha matarajio ya wahusika wengine. Kwa mfano viongozi wanaweza kujitokeza wakitenda matendo hasi kama vile mauaji, usaliti uzinzi na ubinafsi kinyume na matarajio ya wananchi waliowateua.Tena kinaya ni muhimu kwa kuwa hutumiwa kueleza sifa za wahusika katika fasihi kwa kuonyesha vile wahusika wanatenda maovu jambo ambalo ni kinyume cha matarajio ya wahusika wengine na pia wasomaji.kuwasilisha maudhui na wahusika katika kazi za fasihi na kinapaswa kufasiriwa kimuktadha ili kuimarisha mawasiliano. Utafiti unapendekeza kuwa watafiti wa lugha watumie kinaya kama nyenzo ya kuwasilisha masuala yanayodhihirika katika jamii. Utafiti huu unanuiwa kuwanufaisha watafiti wa fasihi ya Kiswahili, wanafunzi, waandishi wa riwaya na watunzi wa tamthilia ili kubainisha dhima ya mitindo ya kifasihi kama vile kinaya katika kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa na mwandishi.

## ABSTRACT

Irony is a critical literary device that is often used by novelists and playwrights to communicate their messages in literary works. The purpose of this study was, therefore, to investigate the use of irony as a literary device in the development of themes and characterization in two Kiswahili literary texts namely: Assumpta K. Matei's novel *Chozi la Heri* and Pauline Kea's play *Kigogo*. The objectives of the study were: one, to identify and categorize different kinds of irony in literary works; two, to explain how irony is useful in the development of themes in the two Kiswahili literary texts, and; three, to explain how irony is used in the development of characterization in the two selected Kiswahili literary works. The study was guided by Stylistic Theory. The novel *Chozi la Heri* and the play *Kigogo* were purposively sampled on the basis of their richness in irony. To get insights into the study, the researcher read books, thesis, and journals related to the topic of study. The study employed descriptive research design. Focus group discussion, which involved four participants inclusive of the researcher, was used to collect data from the selected Kiswahili texts. Data was thematically analysed on the basis of the study objectives. The study notes that there are different types of irony in literary works. These are: Situational, dramatic, verbal, cosmic, and Socratic irony. The research also reveals that situational, verbal, and dramatic ironies are fundamental in the development of themes and characterization in the two selected Kiswahili literary texts. The study concludes that irony is resourceful in conveying themes and characterization in literary works and should be contextually interpreted to enhance communication. The study recommends that language researchers should employ irony as a tool of conveying issues that are evident in society. The research is intended to benefit Kiswahili literary researchers, students, novelists, and playwrights to conceptualize the role of literary styles such as irony in communicating the author's intended message.

## TABARUKU

Naitabaruku tasnifu hii kwa mume wangu mpendwa, Peter Mwari, kwa kunionyesha upendo na kunitia moyo wakati wa kuandaa kazi hii; wanangu Prince Luke, Princess Jayne, Roy Shem na wazazi wangu niwapendao Stephen Mwaniki na Ann Wairimu.

## SHUKRANI

Namshukuru Mungu kwa kunipa nguvu na mwongozo katika kila hatua ya maisha yangu na kunipa uwezo wa kufanya utafiti huu.

Nawashukuru wasimamizi wangu Prof. Joseph Nyehita Maitaria na Dkt. Peter Kinyajui Mwangi kwa kunipa mwongozo na kutumia wakati wao mwingi ili kuhakikisha kuwa kazi ya tasnifu hii imefanywa vilivyo.

Vile vile, nakishukuru Chuo Kikuu Cha Karatina kwa kunipa nafasi ya kuendeleza masomo yangu ya shahada ya uzamili.

## MAELEZO YA ISTILAHI

| | |
|---|---|
| FASIHI: | Ni sanaa inayotumia lugha kiubunifu. |
| KINAYA: | Ni kipengele cha mtindo wa uandishi ambacho huonyesha maana iliyo kinyume na matarajio. |
| MAUDHUI: | Ni jumla ya yaliyomo katika tamthilia, yanayoibuka kuliendeleza wazo kuu. |
| DHAMIRA: | Ni lengo la mwandishi katika kazi yake. |
| KUANGAZIA: | Kuzingatia |

**ORODHA YA VIFUPISHO**

| | |
|---|---|
| n.k | na kadhalika |
| Ashu | Ashua |
| u.k | ukurasa |

## YALIYOMO

UNGAMO ... ii
IKISIRI ... iii
ABSTRACT ... iv
TABARUKU ... iv
SHUKRANI ... vi
MAELEZO YA ISTILAHI ... vii
ORODHA YA VIFUPISHO ... viii
SURA YA KWANZA ... 1
1.0 UTANGULIZI ... 1
1.1 USULI ... 1
1.2 TATIZO LA UTAFITI ... 8
1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI ... 8
1.4 MASWALI YA UTAFITI ... 9
1.5 SABABU YA KUCHAGUA MADA ... 9
1.6 UPEO NA MIPAKA ... 10
1.7 MSINGI WA NADHARIA ... 11
1.8 DHANA YA KINAYA ... 13
1.8.1 MAANA YA KINAYA ... 14
1.8.2 AINA ZA KINAYA ... 14
1.8.2.1 KINAYA CHA HALI ... 14
1.8.2.2 KINAYA CHA MAZUNGUMZO ... 14
1.8.2.3 KINAYA CHA DRAMA AU MAIGIZO ... 15
1.8.2.4 KINAYA CHA KISOKRATIA ... 15
1.8.2.5 KINAYA CHA KILIMWENGU ... 15
1.9 MBINU ZA UTAFITI ... 16
1.9.1 MUUNDO WA UTAFITI ... 16
1.9.2 MAHALI PA UTAFITI ... 16
1.9.3 SAMPULI LENGWA ... 16

1.9.4 UKUSANYAJI WA DATA ... 17
1.9.5 UCHANGANUZI WA DATA ... 17
1.9.6 UWASILISHAJI WA DATA ... 17
SURA YA PILI ... 18
2.0 UTANGULIZI ... 18
2.2 HITIMISHO ... 27
SURA YA TATU ... 28
3.0 UTANGULIZI ... 28
3.1 MIFANO YA KINAYA CHA HALI KATIKA *CHOZI LA HERI* ... 28
3.2 MIFANO YA KINAYA CHA MAZUNGUMZO KATIKA RIWAYA YA *CHOZI LA HERI* ... 37
3.3 MIFANO YA KINAYA CHA HALI KATIKA TAMTHILIA YA *KIGOGO* ... 39
3.4 MIFANO YA KINAYA CHA MAZUNGUMZO KATIKA TAMTHILIA YA *KIGOGO* ... 41
3.5 KINAYA CHA DRAMA KATIKA *CHOZI LA HERI* ... 44
3.6 KINAYA CHA DRAMA KATIKA TAMTHILIA YA KIGOGO ... 65
SURA YA NNE ... 86
4.0 Utangulizi ... 86
4.1 KINAYA KUENDELEZA MAUDHUI KATIKA RIWAYA YA *CHOZI LA HERI* NA TAMTHILIA YA *KIGOGO* ... 86
4.1.1 KINAYA KATIKA UFISADI KATIKA *CHOZI LA HERI* ... 86
4.1.2 KINAYA KATIKA UFISADI KWA KIGOGO ... 92
4.1.3 KINAYA KATIKA UONGOZI MBAYA ... 94
4.1.4 KINAYA KATIKA UONGOZI MBAYA KWA CHOZI LA HERI ... 94
4.1.5 KINAYA KATIKA UONGOZI MBAYA KWA *KIGOGO* ... 99
4.1.6 KINAYA KATIKA UKATILI KWA *CHOZI LA HERI* ... 104
4.1.7 UKATILI KATIKA TAMTHILIA YA *KIGOGO* ... 108
4.1.8 UNAFIKI KATIKA KINAYA KWA *CHOZI LA HERI* ... 110
4.1.9 KINAYA KATIKA UNAFIKI KWA *KIGOGO* ... 115
SURA YA TANO ... 119
UTANGULIZI ... 119
5.1 WAHUSIKA KUBAINISHA KINAYA KWA *CHOZI LA HERI* ... 119

5.1.2 SIFA ZA SAUNA KUBAINISHA MAUDHUI KATIKA CHOZI LA HERI ................ 120
5.1.3 SIFA ZA PETE KUBAINISHA KINAYA KATIKA RIWAYA YA CHOZI LA HERI .................................................................................................................... 121
5.2 SIFA ZA WAHUSIKA KUBAINISHA KINAYA KWA KIGOGO .................................. 123
5.2.1 SIFA ZA MAJOKA KUDHIHIRISHA KINAYA ........................................................ 123
5.2.2 SIFA ZA KENGA KUDHIHIRISHA KINAYA............................................................ 130
5.2.3 SIFA ZA HUSDA KUDHIHIRISHA KINAYA ........................................................... 133
5.2.4 SIFA ZA MAMAPIMA KUDHIHIRISHA KINAYA ................................................... 135
SURA YA SITA ............................................................................................................. 138
MUHTASARI NA MATOKEO YA UTAFITI.......................................................................... 138
6.1 UTANGULIZI .............................................................................................................. 138
6.1 MUHTASARI WA TASNIFU ........................................................................................ 138
6.2 MATOKEO YA UTAFITI .............................................................................................. 139
6.3 MCHANGO WA UTAFITI............................................................................................. 140
6.4 CHANGAMOTO.......................................................................................................... 140
6.5 MAPENDEKEZO......................................................................................................... 141
6.6 HITIMISHO................................................................................................................. 141
7.0 MAREJELEO ............................................................................................................. 144
KIAMBATISHO 1............................................................................................................ 148
KIAMBATISHO2............................................................................................................. 149
KIAMBATISHO III: LESENI YA UTAFITI ......................................................................... 150

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 USULI

Kinaya ni mbinu ambayo hueleza mambo kinyume na matarajio ya wahusika au jamii. Kwa mujibu wa Wamitila (2000) kinaya hutokea wakati maneno yanayotumiwa huleta mkinzano kimaana katika muktadha tofauti na ilivyokusudiwa na msomaji. Maelezo haya yanaashiria kuwa kinaya huhitaji muktadha fulani ili kuifafanua kwa nia ya kuleta maana iliyokusudiwa. Ndiposa Kamusi ya Tuki (2006) inasisitiza muktadha kama kigezo maalum ili kufafanua kinaya. Kinaya kinaelezwa kuwa ni maneno yanayotumiwa kwa mkinzano na maana inayohitajika katika muktadha maalum au inavyokusudiwa na mwandishi, msemaji na mtumiaji.

Kwa mujibu wa Mbatiah (2000) kinaya ni usemi wenye maana iliyo kinyume na kile kinachosemwa. Kinaya huangazia utata wa maisha kwa kubainisha mwanya uliopo baina ya jinsi ambavyo mambo yanaonekana na jinsi yalivyo sasa (uhalisia wake).

Kinaya ni mojawapo ya vipengele vya mtindo wa uandishi. Hutumiwa na watunzi katika riwaya na tamthilia kuonyesha maana iliyo kinyume na matarajio ya watu. Aidha, kinaya huchukua nafasi kubwa sana si tu katika mazungumzo ya kila siku, bali pia jinsi ambavyo mwanadamu anavyotoa mawazo yake. Ni mojawapo ya mbinu zinazotawala maongezi ya mwanadamu hasa kutokana na uwezo wake wa kuficha hisia, maoni,na mitazamo yetu sahihi.

Utafiti huu utazingatia vile kinaya kinatumika katika kubainisha maudhui mbalimbali katika tamthilia ya Kigogo iliyoandikwa na Kea (2016) na riwaya ya Chozi la Heri iliyoandikwa na Matei (2017). Kwa mmujibu wa Wamitila (2008), kinaya ni tamathali ya usemi ambayo inahusisha ukinzani kati ya hali ilivyo na inavyosemekana kuwa. Aidha ni matumizi ya maneno katika kelezea hali kwa maana inayokinzana na anachodhamiria msemaji kwa kuyatumia maneno hayo. Matei na Kea wameshughulikwa masuala yanayopatikna katika maendeleo ya utunzi wa riwaya na tamthilia za Kiswahili.

Masinde (2007) anaeleza kuwa yale yanayoendelea katika jamii humwathiri mtunzi na kumpa tajriba, mguso na ile hamu ya kutunga kwa namna fulani. Zile athari alizopata katika mazingira hujitokeza katika tungo zake kupitia mbinu za lugha anazotumia na ujumbe anaowasilisha. Mojawapo ya mbinu zinazoweza kutumiwa ni kinaya. Aidha, aina za lugha anazotumia mtunzi hutegemea sababu na lengo lake. Kwa misingi hii, utafiti huu ulifanywa kuangazia vile Matei na Kea walivyotumia mbinu hii katika kudhihirisha hali duni wanazopitia wananchi, mikononi mwa wenzao na vile vile miongoni mwa viongozi waliowateua. Matei na Kea wanawasilisha maudhui mbalimbali kwa kinaya kuwakejeli wananchi barani Afrika ambao, licha ya kudai kuwa huru baada ya wakoloni kuacha kuwatawala, wanaendelea kudhulumiwa na viongozi waliowateua kuwaongoza katika harakati zao za ukombozi na pia kudhihirisha maovu wahusika wengine huwafanyia wenzao, jambo ambalo ni kinyume cha matarajio yao.

Mtindo katika fasihi ni mbinu ambazo mwandishi hutumia kuwasilisha mawazo yake ambayo ndiyo maudhui kulingana na Leech na Short (2007). Mtindo na maudhui ni vitu vinavyokamilishana na kutegemeana kwa kuzingatia kwamba mwandishi hawezi kuwa

na mtindo bila ya kuwa na cha kueleza na pia hawezi kuwa na cha kueleza bila mtindo. Utafiti huu umedhihirisha jinsi kinaya kimetumika katika kuendeleza maudhui ya uongozi mbaya barani Afrika kwa kurejelea riwaya na tamthilia za Kiswahili ambazo ni *Chozi la Heri* (2017) na *Kigogo* (2016) mtawalia. Matei na Kea ni waandishi wanaowasilisha maudhui ya uongozi mbaya kwa kinaya, kuwakinaya waAfrika licha ya kudai kuwa huru baada ya wakoloni kuacha kuwatawala, bado wao wanaendelea kudhulumiwa na viongozi waliowateua kuwaongoza katika harakati zao za ukombozi. Riwaya na Tamthilia hizi zimeteuliwa kwa msingi kuwa, Matei na Kea wanaandika kazi hizi katika juhudi zao za kudhihirisha uongozi mbaya unaoendelezwa na viongozi barani Afrika baada ya kunyikakulia uhuru miaka sitini iliyopita. Yaani waAfrika wanakumbwa na matatizo mbalimbali kama ilivyokuwa wakati wa utawala wa wakoloni. Wataalamu wengi wamezungumzia dhana za mtindo, maudhui na kinaya, maelezo ambayo yatahusika katika utafiti huu kama vile:

Kilonzo na Masaku (2017) wanasema kuwa, mtindo katika fasihi huhusisha mbinu za lugha na za uandishi ambazo hutambulikana baada ya kusoma sentensi kadhaa kama vile hotuba, ushairi na nyimbo. Nazo mbinu za lugha au tamathali za usemi hutambulikana bila kusoma sentensi moja tu. Mifano ya mbinu za lugha ni kama vile methali, tashihisi, kinaya, tashbihi na istiari. Nyingi za hizi tulizotaja hutambulika baada ya kusoma sentensi moja.

Wamitila (2000) anasema kwamba, mtindo ni jumla ya mbinu zinazomsaidia mwandishi katika kuwasilisha ujumbe wake. Kwa mfano anaweza kutumia chuku pale ambapo anaongezea sifa zaidi kwa jambo analolizungumzia na tashbihi pale ambapo analinganisha vitu kwa kutumia maneno ya ulinganishi kama vile kama, mfano wa na ja.

Utafiti huu umedhihirisha vile kinaya kimetumika kuelezea mambo ambayo ni kinyume cha matarajio ya watu.

Miriji na Mwangi (2005) wameshughulikia vipengele vya mtindo na fani katika tamthilia za Kiswahili. Wamejadili kwa ujumla kuhusu mtindo na fani. Wanasema kwamba mtindo ni mbinu za lugha na uandishi zinazotumiwa na waandishi katika kuboresha kazi zao. Wanaendelea kusema kuwa, fani ni mbinu anazotumia msanii kuwasilisha maudhui kama vile: Ploti, wahusika, nyimbo, fantasia na utendaji. Utafiti huu umejikita kwenye mbinu ya kinaya vile imetumika katika uendelezaji wa maudhui mbalimbali barani Afrika katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *kigogo.* Pia umeangazia vile kinaya kimetumika katika usawiri wa wahusika pale ambapo utafiti huu umeonyesha sifa hasi wanazoendeleza ambazo ni kinyume cha matarajio ya watu.

Leech na Short (2007) wanasema ya kwamba mtindo ni namna lugha inavyotumiwa na mtu fulani, kwa malengo fulani katika muktadha Fulani. Pia mtindo hutofautisha msanii mmoja na mwingine kwa kuonyesha vile msanii anavyotumia lugha. Tena inategemea vile anavyoteua msamiati na namna anavyosimulia hadithi yake, kwa kutumia nafsi ya kwanza, ya pili na ya tatu. Utafiti huu umeonyesha jinsi waandishi Matei na Kea walivyotumia lugha kwa umahiri mkubwa kwa kutumia lugha ambayo si ya moja kwa moja wanapozungumzia maovu ya wahusika.

Kwa mujibu wa Wafula na Njogu (2007) wanasema kuwa kifasihi, mtindo unaelezwa kwa kuainishwa na madhumuni ya msanii. Maelezo haya yanafaa utafiti huu kwa kuwa mbinu ya kinaya imeainishwa kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti huu kwa mfano, kwa kuonyesha vile mbinu ya kinaya inavyotumika kuendeleza maudhui mbalimbali

katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* na jinsi mbinu hii inavyotumiwa katika usawiri wa wahusika katika riwaya na tamthilia hizi.

Kulingana na Njogu na Chimerah (2014), mtindo ni ufundi wa kupanga na kupangua. Pia wanasema kuwa ni ujuzi wa kujieleza kwa mwandishi. Kutokana na maelezo haya, utafiti huu umeonyesha jinsi waandishi wa riwaya ya *Chozi la Heri na* tamthilia ya *Kigogo* yaani Kea na Matei vile wametumia kinaya kupitisha ujumbe wao. Kwa mfano kwa kuonyesha jinsi wahusika walioaminiwa na watu kuwatawala vyema, walivyogeuka na kuwa na tabia hasi kama vile kuwaangamiza watu, kuwa wabinafsi, wasaliti, katili na hata wadhalimu.

Naye Wamitila (2003) anaeleza kwamba, mtindo ni jumla ya mbinu au sifa zinazomsaidia mwandishi kuwasilisha ujumbe wake. Maelezo haya yameufaa sana utafiti huu kwa kuwa umeonyesha jinsi waandishi wa riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* walivyotumia kinaya katika kuwasilisha ujumbe wao. Kwa mfano, wameonyesha sifa hasi za viongozi kwa kutumia kinaya pale ambapo wahusika waliokuwa wanadhaniwa ni wawajibikaji na wale watu waliowachagua, wanadhihirisha hulka zao hasi za kuwakandamiza raia kama vile kuwa fisadi na katili jambo ambalo ni kinyume cha matarajio yao.

Kulingana na Senkoro (1982) mtindo katika kazi yoyote iwayo ya fasihi ni ile namna ambayo msanii hutunga kazi hiyo kwa kutumia dhana ya mtindo na maudhui kudhihirisha sheria zilizofuatwa. Kwa maoni yake Senkoro, mtindo ni upangaji wa fani na maudhui katika kazi ya fasihi kwa njia inayoonyesha upekee wa mtunzi wa kazi hiyo. Utafiti huu umeonyesha vile kinaya kimetumika katika kuendeleza maudhui katika riwaya na tamthilia teule za Kiswahili.Kinaya hutegemea mazingira ya mwandishi,

falsafa yake, nyakati na aina ya ujumbe anaonuia kuwasilisha. Pia kinahusu namna ya kuitumia lugha ili kufikia ujumbe unaotaka kutolewa, na mara nyingine kuifikia maana au ujumbe huo pamoja na taathira fulani kama kipengele cha ziada katika matumizi ya lugha. Utafiti huu umedhihirisha maelezo ya Matei na Kea katika kuonyesha vile kinaya kimetumika katika kuendeleza maudhui kwa kazi ya fasihi.

Maudhui ni jumla ya fikra, mawazo, mitazamo na ujumbe muhimu unaowasilisha mwandishi katika kazi yoyote ya fasihi. Ni mambo ambayo kwake mwandishi hudhamiria kumuasa, kumuonya, kumwelimisha, kumzindua na kumfichulia msomaji uhalisia wa ulimwengu unaomzunguka. Hii ina maana kwamba, maudhui ni mafunzo au ujumbe uliomo kwa minajili ya jamii kwa jumla. Msanii hutumia maudhui kadhaa kuwasilisha dhamira yake. Katika fasihi, maudhui huweza kubainika kupitia kwa maelezo ya mwandishi. Mwandishi anaweza kusimulia kwa kufafanua yale waliyotenda wahusika katika kazi husika huku yakimwongoza msomaji kubaini jinsi wahusika hao wanavyotagusana na jamii yao. Aidha hupatikana kupitia kwa mazungumzo baina ya wahusika, kwa mjadala au uzungumzi nafsi. Katika mazungumzo wahusika husema wanavyoamini, waliyotenda, wanayowania kutenda au waliyoona wenzao.

Maudhui pia hupatikana kupitia vitendo vya wahusika. Kwa mfano maudhui kama vile mapenzi hujitokeza zaidi katika vitendo vya mhusika dhidi ya mwingine kuliko kupitia masimulizi tu. Utafiti huu umeonyesha pia kuwa, mbinu za lugha hususan kinaya zinaweza pia kutumika katika kuendeleza maudhui mbalimbali katika kazi za kifasihi. Katika kuandika, wasanii hushughulikia mambo ambayo yanaikera jamii au kuiletea adha na masumbuko yasiyofaa. Haya hushughulikiwa kwa mapana na marefu. Utafiti huu umeangazia maudhui ambayo huendelezwa na mbinu ya kinaya na ambayo yanaikera

jamii kwa vile wanatendewa mambo ambayo ni kinyume cha matarajio yao. (Msokile, 2013) anafafanua maudhui kuwa ni mawazo, fikra na ujumbe uliomo katika kazi ya fasihi.

Kwa mujibu wa Wamitila (2008), kinaya ni tamathali ya usemi ambayo inahusisha ukinzani kati ya ilivyo na inavyosemekana kuwa. Aidha ni matumizi ya maneno au kauli kwa maana inayokinzana na anachodhamiria msemaji kwa kuyatumia maneno hayo. Maelezo haya yamefaa sana katika utafiti huu kwa kuwa riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* zimeangazia viongozi wanaoteuliwa na watu ili wawajibikie. Baadaye, wanawadhulumu na kuwarudisha nyuma kimaendeleo kama vile ilikuwa tu wakati wa ukoloni.

Kinaya hujengwa kwenye msingi wa kuwepo na msigano au mgongano fulani kati ya hali halisi na matarajio ya wanaohusika, pale ambapo matukio yanatendeka kinyume cha matarajio ya watu. Pia ni mbinu ambayo inatumiwa sana katika mazungumzo ya kila siku tunapokumbana na matatizo ya maisha. Katika kipindi hiki cha maisha, baadhi ya wanafalsafa wanakieleza kama kipindi cha kinaya ambapo mambo yaliyokubaliwa yamebadilishwa na kugeuzwa kwa njia isiyofaa. Utafiti huu umejikita katika kinaya ili kudhihirisha matatizo yanayowakumba waKenya miaka sitini baada ya kupata uhuru.

Riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* ndizo zitaangaziwa kwa kuwa waandishi hawa wawili wanazungumzia masuala ambayo yanafanana. Tena Matei anaendeleza mawazo ya Kea pale ambapo anazungumzia vile waKenya wanavyodhulumiwa na viongozi wanaoendeleza ukoloni mamboleo nchini. Riwaya na tamthilia hizi zimeonyesha vile baada ya miaka hamsini ya uhuru bado watu hawana maendeleo yoyote ya kufurahia. Tamthilia hizi zimeteuliwa kwa msingi kuwa watafiti wengi wametafitia

mbinu za kimtindo kama vile istiari na jazanda vile zimeendeleza maudhui lakini kinaya hakijatafitiwa vile kimeendeleza maudhui katika riwaya na tamthilia teule. Utafiti huu basi umetumika katika kujaza pengo hili. Utafiti huu pia umeonyesha vile mbinu ya kinaya imetumika katika usawiri wa viongozi ambao wanaendeleza uongozi mbaya nchini kenya baada ya uhuru.

## 1.2 TATIZO LA UTAFITI

Utafiti huu umeangazia vile kinaya kama mbinu ya kimtindo kimetumika katika uendelezaji wa maudhui mbalimbali katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo*. Mtindo ni mbinu zinazomsaidia mwandishi katika kuwasilisha ujumbe wake na huelezea jinsi mwandishi alivyoiunda kazi yake. Kipengele cha kinaya husaidia mtunzi katika kuwasilisha ujumbe wake kwa njia ya kipekee. Utafiti huu umetathmini na kuchanganua mifano ya matumizi ya lugha ya kinaya katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo*. Uchanganuzi wa kinaya katika riwaya na tamthilia teule umewezesha kubaini iwapo matumizi ya mbinu hii yamefanikisha kazi za watunzi.

## 1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI

Utafiti huu umekuwa na malengo haya:

(i) Kufafanua aina mbalimbali za kinaya katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo.*

(ii) Kujadili vile waandishi wa riwaya na tamthilia lengwa wametumia kinaya katika kubainisha maudhui mbalimbali.

(iii) Kueleza vile mbinu ya Kinaya ilivyotumika katika usawiri wa wahusika katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo.*

## 1.4 MASWALI YA UTAFITI

Utafiti huu umeongozwa na maswali yafuatayo:

(i) Je, ni aina zipi za kinaya zimejitokeza katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo*?

(ii) Mbinu ya kinaya imetumika vipi katika kubainisha maudhui mbalimbali katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo*?

(iii) Wahusika wamesawiriwa vipi kupitia kinaya katika riwaya ya *Chozi la Heri na* tamthilia ya *Kigogo?*

## 1.5 SABABU YA KUCHAGUA MADA

Kushughulikiwa kwa mada hii kulichochewa na sababu nyingi. Kwanza kazi yoyote ya fasihi hulenga kupitisha ujumbe kwa hadhira. Kea katika tamthilia ya *Kigogo* anaeleza matatizo ambayo WaKenya walipitia wakati wa utawala wa wakoloni. Ameonyesha jinsi walivyopigania uhuru na wakaweza kujikomboa kutoka kwa utawala wa wakoloni. Baadaye waliwateua viongozi wenzao wakiwa na matumaini ya kujiendeleza kiuchumi na kihali. Kinaya ni kwamba wanadhulumiwa na viongozi hao kama vile kuuawa bila hatia na mashamba yao kunyakuliwa kama vile ilivyokuwa wakati wa ukoloni.

Matei katika *Chozi la Heri* anaendeleza kazi yake Kea pale ambapo anaonyesha vile waKenya baada ya kujinyakulia uhuru miaka sitini iliyopita, bado wanaendelea kuteseka kwa njia mbalimbali kama vile mauaji ya watu bila hatia na pia mali yao kuteketezwa kiholela. Uchunguzi wa mtindo ni muhimu katika kuielezea kazi ya fasihi. Mawazo haya yanaungwa mkono na Mbatiah (2000) anayesema kuwa, tangu mwanzoni mwa karne ya ishirini na moja, watunzi wa kimagharibi wanatukuza mtindo. Maelezo haya yamefaa

utafiti huu kwa kuwa umeonyesha jinsi Matei na Kea walivyotumia mtindo wa mbinu ya kinaya katika kuonyesha taswira halisi ya Wakenya baada ya mkoloni kusalimu amri na kuondoka nchini. Bado wanaendelea kukumbwa na matatizo mengi kama ilivyokuwa wakati wa mkoloni jambo ambalo ni kinaya kwao kwa kuwa wanadai wako huru.

Mara nyingi dhana ya mtindo huwakanganya wanafunzi na hata baadhi ya wachambuzi wa riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo.* Utafiti huu umewasaidia wachambuzi na wanafunzi kuelewa matumizi ya kinaya katika riwaya na tamthilia hizi. Utafiti huu utawafaidi pia watunzi wa riwaya na tamthilia kuhusu jinsi ya kuteua mitindo. Pamoja na hayo, utafiti huu ni muhimu kwa wasomi na watafiti kwa sababu ni mfano bora wa namna ya kuhakiki kazi ya fasihi. Utafiti huu pia utawanufaisha wakuza mitaala kwa sababu utaongeza maarifa kuhusu uchambuzi wa riwaya za Kiswahili.

Lugha ya kinaya inapotumiwa ipasavyo katika kazi ya fasihi,huipa mvuto mkubwa kazi hiyo na kuifanya ya kupendeza. Matei na Kea ni waandishi wenye tajriba kubwa na wametumia lugha isiyo ya moja kwa moja kudhihirisha maovu yanayoendelezwa na viongozi nchini. Utafiti huu umedhihirisha jinsi walivyotumia kinaya katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* kukejeli viongozi wa Kenya ambao hawajawajibika katika kazi zao.

## 1.6 UPEO NA MIPAKA

Ufiti huu umejikita katika kuitalii mbinu ya kinaya kama ilivyotumika katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo.* Utafiti huu umeonyesha mifano mbalimbali ya kinaya katika riwaya na tamthilia hizi, kuonyesha jinsi kinaya kimetumika katika kuendeleza maudhui mbalimbali na jinsi mbinu hii ya kinaya imetumika kuwasawiri viongozi katika riwaya na tamthilia hizi. Eneo la utafiti huu ni maktabani pale ambapo

mtafiti alihudhuria maktaba kadhaa kama vile maktaba ya Chuo Kikuu cha Kenyatta, Karatina na Nairobi.

## 1.7 MSINGI WA NADHARIA

Wamitila (2003) anaeleza kuwa nadharia hutumiwa kumaanisha kauli za kijumla zinazomwongoza msemaji katika ufasaha wa maana uliopo katika fasihi kwa mfano, katika kuelewa maudhui katika kazi ile ya fasihi. Anaendelea kusema kuwa nadharia ni njia ya kisayansi inayohusika na kanuni za kijumla na zinazohusika katika utatuzi wa swala fulani katika kazi ya fasihi. Maelezo haya yamefaa sana kwa utafiti huu kwa kuwa utadhihirisha vile Matei na Kea waliepuka kuelezea dhuluma ya viongozi kwa watawaliwa kwa njia ya moja kwa moja. Badala yake wakatumia kinaya kuendeleza maudhui mbalimbali katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo*.

Nadharia ambayo imeongoza utafiti huu ni ile ya uhakiki wa kimtindo pale ambapo imeonyesha jinsi kinaya kimetumika katika kuendeleza maudhui mbalimbali katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo.* Miongoni mwa waasisi muhimu wa nadharia hii ni (Coombes

1953) anayeeleza kuwa, ili kuchanganua fasihi kwa undani hatuna budi kuzingatia matumizi ya lugha. Coombes anasema kwamba ili kuchanganua mtindo katika kazi fulani, lazima vipengele vinavyofanya kazi hiyo vivutie ili vizingatiwe. Anaendelea kuzungumzia vigezo kama vile matumizi ya taswira, wazo la kishairi, hisia zinazoibuliwa, uteuzi wa maneno, urari wa vina na mahadhi ya shairi.

Leech na Short (2007) wanaendeleza nadharia hii ya kimtindo pale pale wanasisitiza kuwa nadharia hii ya kimtindo inajikita kwenye uchunguzi wa lugha kwa kiasi kikubwa. Wanaendelea kusema kuwa uchunguzi huu wa lugha unapania kubainisha ubunifu uliopo

kwenye lugha hiyo na husaidia katika uelewekaji wa matini ya kazi ya fasihi. Maelezo haya yamefaa sana utafiti huu kwa kuwa nadharia hii ya mtindo imedhihirisha vile Kea na Matei walitumia kinaya katika kuonyesha vile viongozi nchini Kenya wanadhulumu raia wanaowaongoza hata baada ya kupata uhuru miaka sitini iliyopita.

Wamitila (2008) anaendeleza nadharia hii ya kimtindo pale anasisitiza kwamba, nadharia hii inadhamiria kufanikisha uchunguzi wa kina wa matumizi ya lugha katika fasihi. Kimsingi, anaashiria kuwa uhakiki wa mtindo huhusu kuchanganua vipengele vya fasihi na pia vya isimu. Hii inamaanisha kuwa tunapohakiki mtindo katika fasihi, hatuwezi kupuuza matumizi ya vipengele vya kiisimu kwa kuwa hutumiwa kuonyesha sifa za kimtindo za kazi au matini ya kifasihi.

Nadharia hii imeongozwa na mihimili kama vile kwanza uhakiki wa mtindo hujihusisha na uchunguzi wa kinachosemwa ambacho ni ujumbe na kinavyosemwa ambacho ni mtindo. Mhimili huu umeufaa utafiti huu kwa kuwa umeonyesha jinsi kinaya kinadhihirisha ujumbe wa waandishi wa riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya na *Kigogo* yaani Kea na Matei. Pia umeonyesha vile kinaya huendeleza maudhui katika riwaya na tamthilia hizi na jinsi viongozi wamesawiriwa katika kutenda matendo ambayo ni kinyume cha matarajio ya jamii.

Nadharia ya uhakiki wa kimtindo pia husisitiza kuwa, kila kazi ya fasihi ina ubunifu fulani ambao unapochanganuliwa kwa undani husaidia uelewekaji wa undani wa matini za fasihi kulingana na madai ya Simpson (2004). Mhimili huu umefaa utafiti huu kwa kuwa umeonyesha vile waandishi wa riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* walivyotumia ubunifu katika kazi zao. Kwa mfano walitumia kinaya katika kuwasilisha maudhui potovu yaliyoibuliwa na wahusika waliokuwa wanadhaniwa kuwa wenye hulka

nzuri lakini wakatenda mambo ambayo ni kinyume cha matarajio ya jamii.

Tatu,fasihi haiwezi kujadiliwa bila kuzingatia kuwa ina matumizi maalum ya lugha kulingana na Chapman (2012). Haya maoni yanaungwa mkono na Senkoro (1982) anaposema kwamba uteuzi wa maneno si huru na msanii hulazimika kuwa makini ili kazi yake ikubalike na walengwa au hadhira yake. Maelezo haya yanafaa utafiti huu kwa kuwa umeonyesha vile waandishi wa riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* walivyotumia umahiri wao katika uteuzi wa lugha katika kazi zao. Kwa mfano kwa sababu hawakuwa wanataka kudhihirisha maovu ya viongozi moja kwa moja, waliteua kinaya kinachotumika kama kioo kwa jamii kuona na kuelewa mambo yanayotendwa na viongozi hawa yaliyo kinyume cha matarajio yao.

Nne, lugha ndicho kigezo muhimu cha kupimia ufanisi wa kazi ya fasihi kulingana na Ngara (2011). Kazi ya fasihi huwa na sehemu kama dhamira, maudhui na wahusika. Hata hivyo bila lugha, vipengele hivi haviwezi kuwasilishwa vilivyo, sehemu hizi hupewa umbo kupitia kwa lugha. Maelezo haya yamefaa utafiti huu kwa kuwa yameonyesha vile lugha ya kinaya imewasawiri viongozi katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* vile kimetumika kuainisha maudhui mbalimbali na kutekeleza dhamira ya waandishi Kea na Matei.

## 1.8 DHANA YA KINAYA

Utafiti huu umeangazia maana ya kinaya pamoja na aina zake na vile kinaya kimetumika kubainishia maudhui. Isitoshe utafiti huu umeangazia sifa za wahusika vile zinajidhihirisha katika riwaya na tamthilia teule.

### 1.8.1 MAANA YA KINAYA

Kinaya ni mbinu ambayo hueleza mambo kinyume na matarajio ya wahusika au jamii. Kwa mujibu wa Mbatiah (2000) kinaya ni usemi wenye maana iliyo kinyume na kile kinachosemwa. Kinaya huangazia utata wa maisha kwa kubainisha mwanya uliopo baina ya jinsi ambavyo mambo yanaonekana na jinsi yalivyo sasa (uhalisia wake).

### 1.8.2 AINA ZA KINAYA

Kinaya huwa ni mbinu ya lugha ambayo hujitokeza kwa aina tatu kama ifuatayo:

#### 1.8.2.1 KINAYA CHA HALI

Kinaya cha hali ni kinaya kinachodhihirisha vile hali hujitokeza kinyume na matarajio ya watu na maelezo haya yanaungwa mkono na Senkoro (1982) anayesema kuwa kinaya cha hali hutokea pale ambapo hali inakuwa kinyume na matarajio ya wahusika. Kwa mfano watu kuchagua kiongozi ambaye wanadhania kuwa atashughulikia matatizo yao lakini anawapuuza waliomchagua kwa kuwa na ubinafsi na tamaa na hivyo kutenda kinyume cha matarajio ya watu.

#### 1.8.2.2 KINAYA CHA MAZUNGUMZO

Kinaya cha mazungumzo ni kinaya ambacho mzungumzaji anatoa taarifa ambayo maana yake ni tofauti kabisa na maana ambayo inaonyeshwa waziwazi. Maelezo haya yanaungwa mkono na Wamitila (2003) anayesema kuwa kinaya cha mazungumzo hujitokeza pale ambapo mzungumzaji anafanya mambo kinyume na taarifa anayoitoa. Kwa mfano, kama ni kiongozi, anazembea kazini na kukosa kutimiza ahadi alizoahidia watu. Isitoshe, kuna viongozi wanaowaahidia wananchi usalama lakini wanakuwa katika mstari wa kwanza kutekeleza mauaji ya kiholela na kuwadhulumu wananchi.

#### 1.8.2.3 KINAYA CHA DRAMA AU MAIGIZO

Hiki ni kinaya kinachojitokeza wakati msomaji anapojua jambo muhimu kuhusu hadithi ambalo mhusika mmoja au zaidi katika hadithi hawalijui. Maelezo haya yanaungwa mkono na Mbatiah (2000) anayesema kwamba, kinaya cha drama hujitokeza pale ambapo mhusika fulani katika hadithi haelewi jambo muhimu ambalo msomaji analielewa.

#### 1.8.2.4 KINAYA CHA KISOKRATIA

Hiki ni kinaya ambacho mhusika mmoja anajifanya haelewi lolote kuhusu mhusika mwingine na kumuuliza maswali kuhusu matukio yaliyokuwa yametokea ili kumfanya mjinga na kutaka kujua kama atamdanganya. Maelezo haya yanaungwa mkono na Simpson (2004) anayesema kuwa mhusika mmoja katika hadithi humfanya mwingine mjinga kwa kumuuliza maswali kuhusu matukio yaliyokuwa yametokea.

#### 1.8.2.5 KINAYA CHA KILIMWENGU

Hiki ni kinaya ambacho wahusika katika fasihi hujitokeza wakiwa wacha mungu sana lakini kinaya ni kwamba, mungu hawasaidii wakati wana matatizo mengi na kinaya cha matarajio ni kwamba, wanaendelea kumuabudu mungu. Maelezo haya yanaungwa mkono na Wamitila (2000) anayesema kuwa katika hadithi kuna wahusika ambao hujitokeza wakiwa wacha mungu sana na wakati wanapatwa na matatizo wanajitokeza wakimwomba mungu ili awasaidie. Kinaya cha matarajio ni kuwa, Mungu huwa hawasaidii na wanaendelea kuweka imani yao kwa mungu hata kama hakuwasaidia wakati wa shida.

## 1.9 MBINU ZA UTAFITI

### 1.9.1 MUUNDO WA UTAFITI

Utafiti huu ulikuwa wa aina ya kimaelezo ya kina kuhusu namna watunzi wametumia kinaya katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo.* Matokeo ya utafiti yametolewa kwa maelezo ambapo mtafiti amepambanua jinsi mbinu ya kinaya imetumiwa na Kea na Matei katika kuendeleza maudhui mbalimbali katika riwaya na tamthilia teule. Pia ulihusisha kusoma makala muhimu ambayo yalihusiana na mada na tafiti zilizotangulia.

### 1.9.2 MAHALI PA UTAFITI

Utafiti huu ulifanywa maktabani kwa kusoma kwa makini riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo.* Pia udurusu wa tasnifu mbalimbali zinazohusiana na mada hii ulifanywa ili kupata maoni ya waandishi mbalimbali yanayohusiana na mada hii na ambayo yanaweza kutumika katika utafiti huu.

### 1.9.3 SAMPULI LENGWA

Kinacholengwa katika utafiti huu ni mbinu ya kinaya vile imetumika kuendeleza maudhui kwa riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo.* Riwaya na Tamthilia hizi zimeteuliwa kimaksudi kwa kuwa zina data ya kutosha ambayo ilihitajika katika utafiti huu. Kwa mfano riwaya na tamthilia hizi zimesheheni mbinu ya kinaya pale ambapo viongozi katika Kenya walioteuliwa na watu wanageuka na kuwatendea unyama kama vile kuwanyang'anya mashamba yao kama ilivyokuwa wakati wa ukoloni.

### 1.9.4 UKUSANYAJI WA DATA

Data ilikusanywa kutoka maktabani kupitia usomaji wa kina wa riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo,* tasnifu za waandishi wengine na kufafanua bayana vile kinaya kimetumika katika kubainisha maudhui mbalimbali katika riwaya na tamthilia teule. Mbinu nyingine iliyotumiwa ni udondoaji wa sehemu za vitabu vinavyozungumzia kuhusu mbinu ya kinaya. Isitoshe palikuwa na mjadala wa kundi lililohusisha washiriki wane na pia mtafiti. Kundi hili liliteuliwa kwa msingi kwamba washiriki wane hawa wamehitimu katika uzamili kwa kitengo cha fasihi na wanaelewa vyema mbinu zote za mtindo haswa kinaya. Walitumia mbinu ya kusoma vitabu vyote vinavyohusu kinaya na pia kujadiliana vile mbinu ya kinaya imetumika katika kubainisha maudhui mbalimbali katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo.*

### 1.9.5 UCHANGANUZI WA DATA

Baada ya kukusanya data, iliainishwa. Uainishaji huo umefanywa kwa njia ya kimaelezo kwa kufafanua vile kinaya kinaendeleza maudhui mbalimbali katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* zilizoandikwa na Matei na Kea Kisha, uchanganuzi umefanywa kwa kuzingatia maswali ya utafiti, pengo, mihimili ya nadharia, sababu za kutumia kinaya katika utunzi, umuhimu na mchango wake.

### 1.9.6 UWASILISHAJI WA DATA

Data imewasilishwa kwa njia ya kimaelezo, pale ambapo imefafanuliwa kwa kutoa mifano ya kinaya katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo*. Pia kueleza jinsi kinaya kimetumika katika uendelezaji wa maudhui mbalimbali na vile kimetumika katika usawiri wa wahusika katika riwaya hizi. Maelezo haya yamejenga sura mbalimbali za tasnifu hii.

# SURA YA PILI

# YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

## 2.0 UTANGULIZI

Sura hii imeongozwa na mhimili wa nadharia ya kimtindo unaodokeza kwamba, fasihi haiwezi kujadiliwa bila kuzingatia kuwa ina matumizi maalum ya lugha kulingana na Chapman (2012). Utafiti huu umeshughulikia vile waandishi mbalimbali wametumia mtindo kwa kutafitia aina tofauti za mbinu za lugha na sura hii imedhihirisha pengo ambalo limezibwa na utafiti huu la kuangazia vile kinaya kimetumika katika kubainisha maudhui mbalimbali katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo.* Watafiti waliozingatiwa ni kama wafuatao:

Haji (2022) katika utafiti wake amechanganua kipengele cha mtindo ambacho ni sitiari katika tamthilia za *Kivuli Kinaishi* (1990) na *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2000). Katika utafiti wake, ameangazia aina mbalimbali za sitiari ambazo ni sitiari fifi, sitiari shehenezi, sitiari fiche na sitiari za kimajazi. Pia, ameangazia umuhimu wa sitiari katika kuendeleza maudhui katika tamthilia teule. Utafiti wake ni tofauti na huu kwa sababu Haji amejadili sitiari lakini sisi tunajadili mbinu ya kimtindo ya kinaya.

Dhana ya fani ina maana mbili- Kwanza, ni jumla ya vipengele vya kimtindo na kisanaa katika kazi ya kifasihi vinavyojenga kiunzi cha kubebea ujumbe au maana mahususi. Pili, ni kategoria ya fasihi kama drama, ushairi na tamthilia. Maelezo haya yanaungwa mkono na Mbatiah (2000). Kijelezi cha kwanza kuwa fani ni vipengele vya kimtindo na kisanaa vinavyojenga kiunzi cha kubebea ujumbe na maana mahususi, kinamaanisha kuwa fani ni zile mbinu ambazo msanii anatumia ili kuufanikisha ujumbe wake kwa hadhira lengwa. Kimsingi, kazi za kifasihi huwa zimegawika katika sehemu mbili kuu yaani fani na

maudhui. Maelezo haya yamefaa utafiti huu kwa vile uliangazia vile kinaya kimetumika katika kuendeleza maudhui mbalimbali katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo.*

Mbatiah (2000) na Wamitila (2003) wanadai kuwa wahusika ni watu, wanyama, na ndege wanaotumiwa na watunzi katika utendaji na upitishaji wa ujumbe. Kutokana na matendo na mazungumzo yao, wanatudokezea kuhusu ujumbe wa kazi inayohusi. Kila mhusika hupenyezwa katika nafasi yake maalum ili kutimiza majukumu maalum ya msanii hata kama anapewa nafasi ndogo sana. Wahusika wengine hushirikishwa kwa kupewa nafasi ya kutenda ,kusema, kujiwasilisha na kujitambulisha kwa hadhira.

Maudhui hujitokeza katika taasisi ya uongozi katika jamii. Maneno haya yameungwa mkono na Mahero (2002) pale ambapo amejadili maono ya jamii katika tamthilia za *Nyaigoti Chacha,* pale ambapo ameegemea upande wa maudhui ya uongozi katika kazi yake. Tamthilia za Chacha ambazo ameshugulikia ni: *Wingu Jeusi* (1987), *Hukumu* (1992), *Mke Mwenza* (1982) na *Marejeo* (1986). Katika uhakiki wake, Mahero amejishughulisha na ubainishaji wa maono ya taasisi ya uongozi katika jamii na jinsi inavyojitokeza katika tamthilia za mwandishi Chacha. Anafafanua kuwa mazingira ya msanii pamoja na tajriba yake, katika maisha huathiri kwa kiasi kikubwa jinsi anavyouona na kuusawiri ulimwengu. Utafiti huu umefaa sana kazi hii kwa sababu ulikuwa wa manufaa katika kuelewa athari za mazingira na tajriba katika kazi ya mtunzi.

Mtindo ni jumla ya mbinu zinazomwezesha msomaji kurejelea sifa maalumu za mwandishi au mazoea ya mwandishi fulani ambayo hujionyesha kwenye fani yake. Mazoea hayo ya mwandishi ya kuandika, kuteua msamiati, tamathali za semi, taswira na uakifishaji wa sentensi ndiyo yanayomtofautisha mwandishi huyo na wenzake. Maelezo

haya yalichangiwa katika fasihi na Wamitila (2001). Ujumbe huu unatofautiana na kazi hii kwa kuwa yeye ameshughulikia mtindo kwa jumla na utafiti huu umeangazia mbinu ya kinaya.

Kwa kauli hii ya Wamitila, tunaweza kusema kwamba mtindo wa mtunzi huonekana baada ya kuandika kazi zake kadhaa. Maoni haya yana ukweli kwa kuwa ni vigumu kuelewa mbinu za mwandishi bila kusoma kazi yake. Kwa hivyo, mtindo (upekee) wa mwandishi huweza kubainishwa baada ya kupitia kazi zake kadhaa. Kwa ufupi mtindo ni ule upekee alionao mtunzi wa kazi ya fasihi katika kuipa kazi yake sura fulani kifani na kimaudhui. Mtindo huambatanishwa na tabia ya utungaji ambayo humpambanua mtunzi mmoja kutokana na mwingine.

Mtindo ni mbinu zinazotumiwa na mwandishi katika kuwasilisha ujumbe au maudhui na maelezo haya yalishughulikiwa na Miriji (2005). Utafiti wake unafanana na huu kwa sababu unaangazia mtindo katika fasihi lakini unatofautiana kwa kuwa huu umejikita katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* vile kinaya kimetumika katika kuendeleza maudhui mbalimbali kaika fasihi.

Katola (2006) na Kisiroche (2008) wameangazia wahusika wanawake katika tamthilia za Kiswahili vile wanadhulumiwa kwa kudharauliwa, kutusiwa na kunyimwa haki. Utafiti huu ni tofauti na kazi hii kwa sababu huu umeshughulikia kinaya katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo.*

Uhakiki wa tamthilia umeshughulikiwa na Wafula na Njogu (2007) pale ambapo wamejikita katika historia na maendeleo yake. Utafiti wao umeshughulikia vile tamthilia zinaendelea kuwazindua watu kuhusu matatizo yanayowaathiri maishani kama vile umaskini na jinsi wanavyojaribu kujikomboa kutoka kwenye matatizo hayo. Utafiti wao

unatofautiana na huu kwa kuwa umejikita katika ri\waya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo*. Yaani umeonyesha jinsi kinaya kimetumika katika kuendeleza maudhui mbalimbali nchini Kenya.

Pia yale yanayoendelea katika jamii humwathiri mtunzi na kumpa tajriba, mguso na hamu ya kutunga kwa namna fulani kulingana na Masinde (2007). Anaendelea kusema kwamba zile athari alizopata katika mazingira yake hujitokeza katika tungo zake kupitia mbinu za lugha anazotumia na ujumbe anaowasilisha. Mojawapo ya mbinu zinazoweza kutumiwa ni kinaya. Aidha,aina za lugha anazotumia mtunzi hutegemea sababu na lengo lake. Kwa msingi huu utafiti umefanywa kwa kuangazia matumizi ya kinaya na jinsi kinavyotumiwa katika kuendeleza maudhui mbalimbali. Kwa hivyo, utafiti huu umeonyesha matumizi ya kinaya katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo*, kukuza na kuendeleza maudhui mbalimbali. Kazi ya fasihi huwasilishwa kupitia lugha, mtunzi huteua lugha yenye mvuto vile vile humsaidia mtunzi ambayo husheheni ujumbe mzito ili kuipa kazi yake umbo mahususi. Aidha, kazi ya fasihi haiwezi kueleweka bila lugha kwani lugha ndicho kifaa muhimu cha kupima ufanisi wake. Lugha ya kinaya ni kipengele muhimu sana cha lugha kwani huipa mvuto kazi ya fasihi.

"Unyonge wa Uchumi" uliomo katika tabaka la chini katika jamii umeshughulikiwa na Kamunde (1983) katika tasnifu yake. Aidha, anajadili kiburi cha watukufu katika riwaya ya *Asali Chungu* (1978), *Utengano* (1980), na *Dunia Mti Mkavu* (1980). Utafiti wake unafanana na huu kwa kuwa unashughulikia maudhui lakini ukatofautiana kwa kuwa wake unajadili maudhui ya utabaka na wetu unashughulikia maudhui ya ufisadi, ukatili na unafiki.

Hussein (1971) ameuhakiki "Ufundi wa Abdulla (1960) katika *Mzimu wa Watu wa Kale."*Kwanza, alieleza mbinu ya maelezo inayotoa picha kamili ya kinachoelezwa. Kwa mfano, Abdulla (1960) anapoeleza kuhusu chumba huandika kama anayekiona chumba chenyewe huku akiandika. Anasema hii humfanya msomaji akione chumba mbele yake. Mbinu hii huleta raha ya usomaji. Utafiti wake unafanana na huu kwa kuwa ameshughulikia mtindo lakini ukatofautiana na huu kwa kuwa yeye anajadili kuhusu taswira lakini wetu unaangazia kinaya.

Vitabu vya fasihi kwa kiingereza vya Ezekiel Alembi kwa kuzingatia "mtindo na upokezi" Vilichambuliwa na Weche (2012) na akatoa maoni kwamba, vitabu hivyo vina ufundi mkubwa katika uandishi na hivyo kuwavutia watoto. Kazi yake imetufaa hasa kwa upande wa uhakiki wa kimtindo. Tofauti ya kazi yake na hii ni kwamba ameshughulikia fasihi ya kiingereza, ilhali utafiti huu umeshughulikia waandishi wa fasihi ya Kiswahili.

Mbinu za ubunifu na uhamishaji wa maana zimechunguzwa na Kamau (1992) pale ambapo amezingatia "Ufundi katika riwaya za Mohammed Said Abdulla." Utafiti huu umefaa utafiti huu kwani umezingatia mbinu za lugha ambazo hutumika kuelezea mtindo wa mwandishi na kutuelekeza kujua mbinu za uandishi kwenye riwaya na tamthilia.

Methali katika riwaya za Suleiman Mohammed zimehakikiwa na Osore (1994) na kuelezea vile methali husaidia katika kuendeleza maudhui na mwishowe akalinganisha mitindo ya waandishi katika riwaya zote. Utafiti huu ulifaa kazi hii kwa kuiongoza kwa mtindo alioutumia mtafiti.

Wanyama (2007) ameshughulikia maudhui na mtindo katika utendi wa Wabukusu "Khuswala Kumuse." Alibainisha mtindo wa uwasilishaji katika utendi huo. Utafiti huu umetufaa tulipochunguza mtindo wa uwasilishaji aliotumia mwandishi Shafi Adam Shafi

kuwasilisha maudhui yake. Utafiti wake ni tofauti na huu kwani ulichunguza utendi nao huu umezingatia riwaya na tamthilia.

Nadharia ya kimtindo ilitafitiwa na Kairu (2007) juu ya mtindo wa Ken Walibora katika fasihi ya watoto. Utafiti wake ulitufaa kama marejeleo muhimu ya Nadharia ya Kimtindo. Utafiti wake. Utafiti wake na huu unatofautiana kwa kuwa wake unaangazia mtindo katika fasihi ya watoto na wetu unashugulikia mbinu ya kinaya vile kinaendeleza *maudhui* katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo.*

Fasihi inahusisha matumizi ya lugha yenye usawa wa maneno kwa njia yenye mvuto, usanifu na adabu kulingana na Njogu (2008). Kwa mujibu wa hayo, lugha ya fasihi inatakiwa iwe fasaha na yenye uteuzi wa msamiati ufaao na matumizi ya misemo inayosadifu. Pia wanaongezea kwamba uteuzi wa lugha ifaayo huifanya kazi ya fasihi iwe na mvuto zaidi na pia matumizi ya tamathali mbalimbali huipa uhai kazi husika. Haya yametusaidia katika kuchunguza matumizi ya kinaya katika uwasilishaji wa mashairi na kutufahamisha sifa za lugha ambayo ni kinaya.

Udhalimu dhidi ya wahusika wa kike katika tamthilia za Kiswahili umeshughulikiwa na Katola (2008). Ameonyesha jinsi wanawake wanavyonyimwa haki zao kama vile kunajisiwa na pia kutumiwa kama vyombo vya mapenzi na wanaume. Utafiti wake ni tofauti na huu kwa kuwa umeshughulikia kinaya katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* vile kimetumika katika kuendeleza maudhui mbalimbali nchini.

Sarara (2011) amejadili maudhui katika tamthilia tatu za S.A. Mohamed. Tamthilia ambazo amezishughulikia ni: *Amezidi* (1995), *Pungwa* (1988) na *Kivuli Kinaishi*. Katika uhakiki wake, amechunguza matatizo katika jamii, chanzo cha matatizo na jamii mpya inayotarajiwa kutokana na mageuzi hayo. Sarara alilenga kuyafafanua na kuyaweka wazi

mawazo mazito na muhimu yanayoikumba jamii. Utafiti huu wa Sarara unatofautiana na wangu kwa sababu yeye amejikita katika suala la maudhui ilhali huu umejikita katika mtindo,wa kipengele cha kinaya.

Maudhui ya mitindo ya lugha inayotumiwa kuwasilisha mafunzo ya tashbihi na matumizi ya ishara kulingana na kukuza vijana katika misingi ya kiuana yameshughulikiwa na Kibutu (2013). Ameangazia mitindo ya lugha akizingatia maudhui, misemo na jamii za Kiafrika. Utafiti wake ni tofauti na huu kwani kazi hii imechunguza matumizi ya kinaya katika kuendeleza maudhui mbalimbali katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo.* Ingawa wake unafanana na huu kwa sababu umeshughulikia kipengele cha mtindo vile mafumbo yanavyoendeleza maudhui na unatofautiana kwa sababu huu umejikita katika kinaya vile kinatumika katika kuendeleza maudhui mbalimbali katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo.*

Okwena (2013) alifanya utafiti wake kuhusu jazanda katika tamthilia tatu za arege kama zifuatazo: *Mstahiki Meya (*2019), *Kijiba Cha Moyo* (2019), *Chamchela* (2007). Katika utafiti wake ameonyesha matumizi ya jazanda katika tamthilia teule. Utafiti huu ulitusaidia kuelewa kipengele cha jazanda na nadharia ya kimtindo. Utafiti huu unatofautiana na kazi hii kwa kuwa umejikita katika kipengele cha mtindo ambacho ni kinaya.

Uhakiki wa fani katika ngano tano za Kiswahili umeshughulikiwa na Oyoyo (2013). Ngano hizi ni: *Kisa cha Binti Matlai Shamsi*- Ngano za Mazimwi, *Kisa cha Cheche na sungura*- Hekaya, *Migani ya Fumo Liyongo*, *Sungura na simba*- hurafa na *Ndovu na Binadamu*- Ngano ya kimafumbo. Katika utafiti wake, amebainisha na kuchanganua vipengele mbalimbali vya fani vinavyoingiliana na kukamilishana katika ujenzi wa umbo

la ngano, ametathmini mchango wa vipengele vya fani katika kuwasilisha maana katika ngano zilizoteuliwa na ametathmini kufana au kutofana kwa msanii katika muundo wa ngano teule za Kiswahili. Utafiti wake unatofautiana na huu kwa sababu ulijikita katika kinaya vile kimetumika katika kuendeleza maudhui mbalimbali katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo.*

Matumizi ya takriri na sitiari katika *Utenzi wa Rasi'Ighuli* yamechambuliwa naNdumbu (2012). Ameonyesha vile mbinu ya takriri imetumika kwa kurudia rudia maneno na silabi na kutolea mifano. Tena ameonyesha jinsi sitiari imetumika pale ameonyesha maneno ambayo yametumiwa kwa kuyalinganisha na mengine bila kutumia maneno ya ulinganishi katika *Utenzi* huu. Utafiti wake unatofautiana na huu kwa kuwa umejikita katika mbinu ya kinaya vile kimeendeleza maudhui ya uongozi mbaya katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo.*

Kinaya kimechambuliwa na Ali (2015) vile kimetumika katika ushairi wa Kithaka wa Mberia kama mtindo wa kuwasilisha ujumbe ambao ni kinyume cha matarajio ya watu katika ushairi. Utafiti wake unafanana na huu kwa kuwa pia umeangazia kinaya lakini unatofautiana kwa kuwa wake umejikita katika ushairi na huu umejikita katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo.*

Lugha ya kimafumbo imechanganuliwa na Nyanchama (2007) katika riwaya za *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995) inayojumuisha istiari, tashbihi, jazanda, majazi, methali na nahau. Utafiti wake umebainisha lugha ya kimafumbo inavyotumiwa katika usawiri na uainishaji wa wahusika katika riwaya hizi. Utafiti huu wa Kamachu unafanana na kazi hii kwa sababu umeangazia mbinu ya kimtindo ya fasihi na ukatofautiana kwa sababu yeye ameangazia mafumbo na huu umeangazia kinaya.

Musembi (2008) ameshughulikia matumizi ya taswira na ukinzano kama kichocheo cha zinduko katika riwaya za G.K. Mkangi *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995). Utafiti huu wa Musembi unafanana na wetu kwa kuwa umeangazia mbinu ya kimtindo lakini ukatofautiana kwa vile huu umejadili kinaya na wake ukajadili taswira.

Taswira na ishara zimeshughulikiwa na Nyanchama. M. (2004) katika *Sauti ya Dhiki*. Utafiti huu unafanana na wetu kwa kuwa umejikita katika mbinu ya kimtindo lakini ukatofautiana na huu kwa kuwa unajadili mbinu ya taswira na wetu mbinu ya kinaya.

Kilonzo na Masaku (2017) katika utafiti wao wameshughulikia tamthilia ya *Kigogo* kwa ujumla pale ambapo wameelezea kuhusu wahusika na sifa zao, maudhui na mbinu zile zimejitokeza kwenye tamthilia. Utafiti wao ni tofauti na huu kwa kuwa huu umejikita katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* pale ambapo umedhihirisha vile mbinu ya kinaya kimetumiwa na waandishi wake yaani Kea na Matei. Wanaonyesha vile waKenya baada ya kujikomboa kwenye minyororo ya wakoloni, bado wanaendelea kudhulumiwa na viongozi waliowateua na kuwarudisha nyuma kiuchumi.

Kinaya kimeshughulikiwa na Oiko (2017) katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* vile kimetumika katika kudhihirisha uovu katika vyombo vya dola na dini. Utafiti wao unatofautiana na huu kwa kuwa wao umejikita katika tamthilia ilhali huu utajikita katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo*. Kinaya kilifafanuliwa vile kinaendeleza maudhui mbalimbali nchini Kenya baada ya kupata uhuru miaka hamsini iliyopita.

Mtindo humtambulisha mtunzi wa kazi ya fasihi na watu hupenda kazi ya msanii fulani kwa sababu mtindo anaoutumia huwavutia wasomaji wake. Ndicho kipengele kinachotenganisha kazi nyingine za kisayansi au za kawaida. Bila mtindo, kazi za kifasihi

zisingepata mashabiki wengi. Kwa hivyo,  mtindo ndio huibua hisia na kuwafanya wapende zaidi kusoma kazi za msanii husika. Tunapozungumzia dhana ya mtindo, tunakuwa tunarejelea mwandishi husika, kwa maana  kwamba ubinafsi wake ndicho kile kinachoonekana kwenye kazi yake. Kwa mantiki hiyo, dhana ya mtindo inaonekana kwa namna mtunzi anavyopanga kazi yake kifani na kimaudhui, yaani namna anavyotumia lugha, anavyopanga visa na matukio, uteuzi wa mandhari, falsafa anavyowasilisha na ujumbe anaoudhamiria.

## 2.2 HITIMISHO

Katika mapitio ya waandishi wengine ni bayana kwamba kipengele cha kinaya katika kuendeleza maudhui mbalimbali katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* hakijatafitiwa. Utafiti huu umeziba pengo hili pale ambapo umedhihirisha jinsi viongozi nchini Kenya wanavyoendeleza uongozi mbaya baada ya mkoloni kuondoka.

# SURA YA TATU

## AINA ZA VINAYA KATIKA RIWAYA YA *CHOZI LA HERI* NA *KIGOGO*

### 3.0 UTANGULIZI

Sura hii imezingatia mhimili wa nadharia ya kimtindo unaodokeza kwamba lugha ndicho kigezo muhimu cha kupimia ufanisi wa kazi ya fasihi kulingana na Ngara (2011). Utafiti huu unadhihirisha vile Matei mwandishi wa riwaya ya *Chozi la Heri* na Kea mwandishi wa tamthilia ya *Kigogo* walivyofanikiwa kutumia aina mbalimbali za vinaya katika kazi zao. Vinaya hivi ni: kinaya cha hali, mazungumzo na drama. Aidha utafiti huu haukuangazia kinaya cha kilimwengu na cha kisokratia kwa kuwa havijajitokeza kwenye riwaya na tamthilia teule.

### 3.1 MIFANO YA KINAYA CHA HALI KATIKA *CHOZI LA HERI*

Kinaya cha hali ni kinaya ambacho hali hutokea kinyume cha matarajio ya watu. Maelezo haya yanaungwa mkono na Senkoro (1982) ambaye anasema kuwa kinaya cha hali hutokea pale ambapo wahusika hujitokeza wakikumbwa na hali ambazo hawakuwa wanatarajia. Katika riwaya ya *Chozi la Heri* tunapata kinaya cha hali kama ifuatavyo:

Neno Heri lina maana ya fanaka au maendeleo na katika riwaya ya *Chozi la Heri* tunapata msitu wa Heri. Tunatarajia mahali hapo ambapo wakimbizi walikuwa wanaishi pawe na mafanikio. Kinyume cha matarajio, wakimbizi wanakumbwa na matatizo chungu nzima kama vile njaa, vifo na mahali hapo hapakuwa na misala ya watu kutumia kwenda haja na walikuwa wanatumia sandarusi. Kaizari anasema,

"*Ni sandarusi ambazo hutumiwa kama misala bwana*" (u.k 28).

Sandarusi hizi walikuwa wanazitafuta kwenye milima ya taka zinazotolewa huko waishio waheshimiwa kuja kutupwa huko kwenye mtaa wa mabanda wa Sombera. Jambo hili linadhihirisha hali ya umaskini ya wakimbizi waliokuwa wanaishi kwenye msitu huu wa Heri (u.k 28). Kinaya kinajitokeza pale tungetarajia viongozi wao wawasaidie kwa kugharamia mahitaji yao ya kimsingi kama vile kuwajengea misala lakini wanawapuuza.

Mfano mwingine ni pale tungetarajia wafanyakazi wawe waaminifu kwa waajiri wao. Katika riwaya ya *Chozi la Heri*, tunampata mhusika anayeitwa Sauna. Alikuwa akimfanyia Lunga Kiriri kazi ya kuwalea watoto wake na alikuwa anajifanya mwaminifu kwake. Baadaye anawateka nyara watoto wake ambao ni Dick na Mwaliko na kuwauza kwa Buda na madanguroni mtawalia. Msimulizi anasema:

*"Sauna alikuwa chui ambaye hakupigwa na mshipa kujifanya mwema kwa waajiri wake ili aaminiwe, naye apate fursa ya kuwaiba watoto na kuwapeleka kwa bibi mmoja ambaye aliwatumia katika biashara ya nipe nikupe, na katika ulanguzi wa dawa za kulevya*" (u.k 98).

Hiki ni kinaya kwa kuwa hatungetarajia mfanya kazi Sauna ambaye ameaminiwa sana na waajiri wake kuwatorosha watoto wao.

Tena katika nchi ya Wahafidhina, wananchi wanakosa chakula na kufa njaa ilhali walikuwa na viongozi ambao walikuwa wamewaahidi vyakula. Katika kambi ya wakimbizi ni dhahiri kuwa njaa ilikuwa ikiwakumba wananchi waliokuwa wanaishi hapo. Mfano ni pale tunampata Ridhaa ambaye hapo awali alikuwa daktari akila mizizi ya miti. Pia inajitokeza kwamba watoto wachanga walikuwa wanaugua ugonjwa wa utapia mlo. kaizari anasema:

"*…Mipaka ya kitabaka imebanwa. Kwa kweli haipo kwani hata sasa nisemapo nang'ang'ania chakula, uji hasa na aliyekuwa Waziri wa Fedha miaka mitano iliyopita."* (u.k 28).

Hiki ni kinaya kwa kuwa viongozi walioteuliwa kuiongoza nchi hii ya Wahafidhina, hawawapatii msaada wowote na wanaishia kufa njaa kwa sababu ya ukosefu wa chakula.

Mfano mwingine ni pale polisi wanatatua mizozo midogomidogo kwa kutumia bunduki. Apondi anasema:

"*Suala la polisi na wanajeshi kutatua mizozo midogomidogo kwa makeke na bunduki ni jambo ambalo limepitwa na wakati; Raia wanahitaji zaidi ushauri badala ya vipigo. Kutatua tofauti zetu kwa vita ni kama kufukuta moto zaidi, na amani tulioazimia kupata haipatikani" (u.k*113). Hiki ni kinaya kwa kuwa polisi wanafaa kuwalinda wananchi lakini tunawaona wakiwaangamiza badala ya kuwasaidia kutatua mizozo baina yao.

Tena, tunapata wanandoa wakisimangwa na kutengwa na jamii kwa kukosa watoto. Jambo hili lilisababishwa na utamaduni pale ambapo Wahafidhina walikuwa wanaamini kwamba sharti wanandoa kupata watoto. Wale walikosa watoto waliathirika kisaikolojia kwa sababu ya hali zao. Katika *Chozi la Heri,* tunapata mhusika Mwangemi akimwambia mkewe Neema:

"*Tumejaribu kupata mtoto, huu ni mwaka wa tano sasa"* (u. k 159).

Hiki ni kinaya kwa kuwa hatungetarajia jamii ya Wahafidhina kuwasimanga kwa ukosefu wao wa watoto. Mwishowe wanaishia kupanga mtoto Mwaliko ili waweze kukubalika katika jamii yao.

Pia tunampata mhusika ambaye ni mkarimu kwa wahusika wale wengine lakini wao wanaishia kumtendea maovu. Mfano tunamwona Ridhaa ambaye alikuwa amemtendea jirani yake mzee Kedi utu. Kwa mfano alimpatia mtoto wa mzee Kedi aliyeitwa Kombo na ambaye alikuwa mhandisi asimamie ujenzi wa nyumba yake. Pia akawafadhili wapwa wa mzee Kedi masomo yao lakini kinyume cha matarajio yake, Mzee kedi anateketeza familia yake.

"Mimi mwenyewe nimeyadhamini masomo ya wapwaze wawili." (u.k 11)

Tungetarajia viongozi wawalinde wananchi ambao waliwateua katika uchaguzi. Katika riwaya ya *Chozi la Heri,* tunaona kwamba hakuna usalama kwani wapinzani wa Mwekevu wanachomea watu magari yao, maduka na nyumba zao. Pia wananchi wanaumizwa bure kwa mfano kukatwa kwa sime na pia wasichana kubakwa ovyo ovyo. Kaizari anasema: "*Baadaye genge hili la mabarobaro watano lilifululiza hadi walipokuwa maskini mabinti wangu wawili, Lime na Mwanaheri. Sikuweza kuvumilia kuona unyama waliotendewa "* (u.*k* 25).

Hapa kinaya kinajitokeza pale ambapo mabinti wawili wa Kaizari yaani Lime na Mwana Heri walibakwa na vijana wahalifu. Tungetarajia walinda usalama kuwazuia wahalifu katika kutekeleza uhalifu wao lakini kinyume cha matarajio tunapata hakuna usalama katika nchi ya Wahafidhina.

Ni dhahiri shahiri kuwa Wahafidhina wanakataa kufuata maagizo ya walinda usalama. Katika *Chozi la Heri*, Selume anasema:

*"Msukamano ulianza hadi pale bwana mmoja aliyevaa mavazi rasmi ya walinda usalama alipojitokeza na kutusihi kuwa watulivu. Tulianza kunung'unika. Wengine*

*tulikumbuka jinsi waungwana hawa walivyotuacha kuhasiriana na waungwana wenzao huko nyumbani… Waliokuwa nyuma walianza kurusha makombora ya matusi. Askari aliinamisha kichwa na kurudi nyuma, nayo hasira ya umati uliokuwa tayari kumpatiliza mja huyu ikapoa*. (U.k 33). Hapa kinaya kinajitokeza pale tungetarajia watu waliokuwa wakipigania chakula kutulia na kunyamaza walipoagizwa na askari lakini wanapuuza maagizo hayo.

Mfano mwingine ni pale tunapata viongozi wakiwa mstari wa mbele kutekeleza ubinafsi. Wao wana uwezo wa kugharamia mahitaji yao ya kimsingi ukiwalinganisha na maskini lakini wanapigania chakula na maskini. Selume anasema*:*

*"Kuna familia, kama vile ya aliyekuwa diwani wetu hapo awali, Bwana Kute, zilizofanya ujanja ili kupata mafungu zaidi*" (u.k 33).

Hapa kinaya kinajitokeza pale bwana Kute ambaye alikuwa diwani, akiwanyanyasa maskini kwa kujigawia chakula kingi kuliko maskini wale walikuwa wamepanga foleni.

Tena, nchi ambazo zimepata uhuru zinashindwa kujitegemea. Tila anamwambia baba yake:

"*Baba, umewahi kumwona mtoto wa miaka hamsini ambaye hajasota; Sikwambii kusimama dede?*" (u.k23)

Hapa kinaya kinajitokeza pale hatungetarajia mtu wa miaka hamsini aitwe mtoto na tena awe hana uwezo wa kutembea. Tila alikuwa anamaanisha kuwa kuna nchi ambazo zimepata uhuru lakini zinashindwa kujitegemea. Hiki ni kinaya kwa kuwa hatungetarajia nchi hizo kukosa kujitegemea.

Pia, tungetarajia akina mama wajawazito wakijifungua watoto wawalee lakini katika riwaya ya *Chozi la Heri* tunaona mama ambaye alijifungua na kutupa kitoto kwenye biwi la takataka. (u.k 159). Hapa ni kinaya kwa kuwa tunawapata wamama wengine wanaokosa watoto wakisikitika kwa sababu ya hali yao ya utasa na hivyo basi tungetarajia wale wanapata wawatunze watoto wao..

Isitoshe, tungetarajia mtu akinywa dawa ya panya aage dunia. Pete anasema:

"*Asubuhi hii fikira zilikuwa zimenijaa kifua tele, nikaona kwamba ni heri niyaangamize maisha yangu. Nilimwambia jirani yangu anichungie wanangu, nikaacha karatasi chenye anwani ya bibi yangu juu kimeza kidogo katikati mwa chumba change na kuondoka… hii ya kuulia panya haitashindwa kunifisha mimi pamoja na kilicho tumboni"* (u.k 152)

Hapa kinaya kinajitokeza pale tunapata kuwa Pete hakufa baada ya kunywa dawa ya panya na yale matatizo alikuwa anataka kuyaepuka yakaendelea kumwandama.

Tungetarajia vijana wakienda ng'ambo na kupata masomo kurudi kwao nyumbani na kusaidia nchi zao. Songoa Kifungua mimba wa Kiriri aliyekuwa anasomea ng'ambo anasema,

"*This country has nothing to offer. Nchi ambayo hata walio na shahada tatu bado wanalipwa mishahara ya mkia wa mbuzi. Mimi sitakufa maskini. Acha niwekeze huku mbali ambako sina hofu ya mali yangu kuibwa au kuchomwa na waivu"* (u.k 72).

Hapa kinaya kinajitokeza kwa pale ambapo Songoa anapoenda ng'ambo na kumaliza kusoma, tungetarajia arudi katika nchi yake kufanya kazi huko lakini kinyume cha matarajio yetu anakataa kata kata kurudi katika nchi yake.

Katika nchi ya Wahafidhina, wanaume hawatetei wake zao mbele ya wazazi wao. Wanatusiwa na wakwe zao na pia kufukuzwa nyumbani na bwana zao wananyamaza bila kuwatetea. Kinaya kimejitokeza pale, Kaizari hakumtetea Subira mkewe dhidi ya masimango ya mamake hata kwa kuitwa mwizi wa mayai na kuku ndiye anafuga. Subira anaamua kutoroka nyumbani na mwishowe anajitoa uhai kwa kunywa sumu. (u.k 98).

Tena, waajiri wanakuwa wazinzi kwa wafanyakazi wanaowaajiri. Katika riwaya ya *Chozi la Heri* tunampata Nyangumi anayemwajiri Pete katika biashara yake ya kuuza nguo. akimshurutisha Pete kufanya mapenzi naye na wakati Pete anakataa tunaona akimfuuta kazi (u.k 151). Hiki ni kinaya kwa kuwa tungetarajia Nyangumi awe na heshima kwa wafanyakazi wake na asiwafute kazi.

Mfano mwingine ni pale kwamba hatungetarajia msichana kujiamulia kupashwa tohara kinyume na hata wazazi wake. Katika riwaya hii ya *Chozi la Heri* tunampata msichana Tuama anajificha na kwenda kupashwa tohara hata ingawa babake alikuwa anaipinga mila hiyo. Hiki ni kinaya kwa kuwa hatungetarajia Tuama kwenda kupashwa tohara bila idhini ya baba yake na baada ya kupashwa tohara anavunja damu na kupelekwan(u.k 144).

Pia wanafunzi wa shule ya upili wanalewa tembo kwa madai kwamba wanajiepusha na matatizo wanayokumbana nayo. Katika *Chozi la Heri*, tunampata kipanga kijana mdogo akianza kunywa Kangara akiwa kidato cha pili ili kujiepusha na matatizo (u.k 143). Hiki ni kinaya kwa sababu alijiingiza kwenye matatizo zaidi ya uraibu wa pombe.

Isitoshe, tunamwona kijana wa mtaani akimsaidia Umu aliye na matatizo kwa kuwa hata kama yeye yumo katika kinamasi cha ukata. Katika riwaya ya *Chozi la Heri*

tunapata kuwa, kijana wa mtaani anayeitwa Hazina ndiye anayemsaidia Umu wakati familia yake ilipoangamizwa Na mzee Kedi. (u.k 89).

Mfano mwingine unajitokeza pale Naomi anmtelekeza mumewe na wanawe katika kipindi ambacho watoto wake (Umulkheri, Dick na Mwaliko) walimhitaji katika malezi yao (u.k 54). Yeye anadai kuwa anaenda kuwatafutia msaada lakini alikuwa anamtorokea mumewe kwa kuwa alikuwa amefutwa kazi na na kushindwa kumsaidia Naomi katika malezi ya watoto.

Pia, hatungetarajia umati wa watu kuangamiza watu wasio na hatia. Katika *Chozi la Heri*, tunampata Lemi akiuawa na watu kwa singizio kwamba, alikuwa amemwibia mama aliyekuwa akipiga unyende simu na yeye hakuwa amefanya hivyo. Hiki ni kinaya kwa kuwa Lemi hakuwa ameeiba simu na alikuwa anaenda nyumbani. Msimulizi anasema:

"*Umati wa watu uliokuwa umesikia kamsa ya mama huku uliwaelekea akina Lemi,unataka kuwavaa kwa mawe na tairi. Nyuma Lemi alisalimiwa kwa mawe na mateke. Baadaye alivikwa pete ya tairi kiunoni. Muda si muda alimwagiwa petroli na kutiwa moto.*' (U.k 124).

Mfano mwigine unajitokeza pale tunapata kuwa kuna wazazi ambao wana uwezo wa kuwasaidia watoto wao wanapokuwa wajawazito wakiwa katika shule za upili lakini wanakataa kuwasaidia. Zohali alipoambulia ujauzito wazazi wake wanamwambia:

"*Umeipaka mashizi familia hii, Kaa hapa nyumbani uilee mimba yako, ukiisha kujifungua, utamtafuta baba mtoto msaidiane malezi… Baba alisema kwamba hakuwa na pesa kumlipa kijakazi tena. Kazi za nyumbani zikaniangukia mimi*" (u.k 100-101).

Hapa kinaya kinajitokeza pale tunaona kuwa wazazi wa Zohali walikuwa na uwezo wa kumsaidia lakini wanakataa kumsaidia. Mama yake alikuwa mwalimu mkuu katika shule ya upili na baba yake alikuwa mkurugenzi mkuu katika shirika la mawasiliano lakini kinyume cha matarajio yetu ni pale tunawaona wakimwambia kuwa yeye ndiye atakuwa kijakazi wao kwa sababu ya kuambulia uja uzito akiwa shule ya upili.

Pia inajitokeza kuwa bwana ambaye ameoa na ana watoto anafanya ufuska na wanawake wengine. Tena mbele ya macho ya watoto wao. Chandachema anasema:

"*Usiniulize niliyaona na kuyasikia mangapi katika chumba hiki ambacho kiligeuka danguro wakati Bi. Kimi alipokuwa ameenda mashambani. Wakati huu Bwana Tenge angeamua kumleta mwanamke mmoja baada ya mwingine, hapo hapo, mbele ya macho ya wanawe, hadi siku ya kurudi kwa Bi. Kimai" (*u.k 106).

Hiki ni kinaya cha hali kwa kuwa hatungetarajia bwana Tenge ambaye ameoa, kubadilika na kuwa mkware kwa sababu ya kuwa na uhusiano na wanawake wengine wakati Bi. Kimai anapokuwa amesafiri kwa shughuli za kazi.

Tena, inajitokeza kwamba, mwalimu ana uhusiano wa kimapenzi na mwanafunzi wake. Katika riwaya hii ya *Chozi la Heri,* tunamwona mwalimu Fumba ambaye ana uhusiano wa kimapenzi na mwanafunzi wake Rehema na wakapata mtoto aitwae Chandachema (u.k 103). Kinaya ni kwamba, tungetarajia mwalimu Fumba kumwelekeza mwanafunzi wake Rehema dhidi ya kutokuwa na uhusiano wa kimapenzi na wavulana. Kinaya kinajitokeza pale ambapo Rehema alipojifungua mtoto msichana anayeitwa Chandachema, mwalimu Fumba anakataa majukumu ya ulezi wa mtoto huyu. Kinaya ni kwamba alimpagaza mama yake kitoto hiki amsaidie kukilea.

Pia tunaona kwamba mama anawafuata watoto wake ng'ambo na kuacha mumewe na kupuuza rai za mumewe. Katika riwaya ya *Chozi la Heri,* kinaya kinajitokeza pale Annette anawafuata watoto wake ng'ambo na kwenda kukaa huko na kupuuza rai za mumewe Kiriri anapomsihi asiende. Msimulizi anatwambia:

*"Wanawe walipokwenda kusomea ng'ambo kama wafanyavyo wana wa viongozi ambao wanaiona elimu ya humu kama isiyowahakikishia mustakabali mwema raia wake, yeye alistaafu mapema akapewa kile kibunda cha mkupuo mmoja aimaarufu Golden Handshake, akachukua Greencard na kuwafuata. Moyo wake haukupigishwa mshipa na rai ya mume mtu akae naye waondoleane upweke*' (u.k 65).

### 3.2 MIFANO YA KINAYA CHA MAZUNGUMZO KATIKA RIWAYA YA *CHOZI LA HERI*

Kinaya cha mazungumzo ni kinaya ambacho mzungumzaji hutoa taarifa ambayo maana yake ni tofauti kabisa na maana ambayo inaonyeshwa waziwazi. Maelezo haya yanaungwa mkono na Wamitila (2003) anayesema kuwa mhusika anaweza kuzungumza jambo ambalo maana yake ni tofauti na maana ambayo inaonyeshwa bayana.

Mfano ni kwamba hatungetarajia watu wakipita barabarani na kupata mtoto ambaye ametupwa, kukakataa kumsaidia na wakiona mja ambaye anataka kunusuru hicho kitoto wanamwambia aachane nacho na kumfisha tamaa kwa kumwambia kuwa anaweza kushtakiwa kama mlanguzi wa binadamu. Neema anasema:

"*Sauti ya mpitanjia menzangu ikaniambia, Usijitie kubeba mzigo ambao si wako*" (u.k161).

Hiki ni kinaya kwa sababu tungetarajia mpita njia huyu kumtia moyo Neema kwa kukisaidia kitoto hicho.

Tena mja anajigamba kuwa anaogopwa sana na watu kwa vile amesoma ilhali hana kazi na anaishi kwa uhawinde. Katika riwaya ya *Chozi la Heri*, Shamsi anajigamba kwamba yeye anaogopwa kwa sababu ya kusoma ilhali elimu hiyo haikumsaidia kwa chochote. Ni mlevi wa kupindukia. Katika wimbo wake anasema:

*"Chuoni nilipohitimu*

*Kwa bashasha za ujana*

*Misuli imetuna nguvu*

*Kulihudumia taifa* ( u.k 132).

Tena mfano mwingine unajitokeza pale tunampata mzazi akimnajisi mtoto wake. Katika riwaya hii ya *Chozi la Heri*, tunaona msichana anayeitwa Sauna akibakwa na baba yake. Badala ya mama yake kumsaidia, anamwambia kwamba asimpake baba yake tope na anyamaze na hali hiyo katika moyo wake (u.k 154). Hapa kinaya kinajitokeza pale mama yake Sauna anakosa kumchukulia mumewe hatua za kisheria kama vile kumshtaki katika mahakamani kutokana na uhalifu wake wa kumbaka mtoto wake.

Isitoshe, kiongozi wa dini anapoagiza watu kufanya jambo, tunatarajia watu kufuata maagizo hayo. Katika riwaya ya *Chozi la Heri,* tungetarajia kiongozi wa kidini kuwasaidia wakimbizi waliokuwa na matatizo chungu nzima. Badala yake anawaambia wawe na amani wakati walikuwa wakisikitika kwa kufukuzwa makwao, wasichana wao wanabakwa na wahalifu na pia wanakula mizizi ya miti na matunda mwitu kwa sababu ya kukosa chakula. (u.k 31)

Mfano mwingine unajitokeza pale ambapo mtu anayewahutubia watu jinsi ya kuhifadhi misitu hata yeye kuanza kuharibu misitu hiyo. Katika riwaya ya *Chozi la Heri*, Lunga Kiriri anaharibu misitu baada ya kufutwa kazi kama mkurugenzi katika kampuni ya uuzaji wa mahindi. Anaenda katika msitu wa Mamba na kuangusha miti na kufungua mashamba makubwa. Hiki ni kinaya kwa kuwa hapo mbeleni alikuwa akiwashauri watu wahifadhi misitu lakini sasa anaiharibu. (u.k62).

### 3.3 MIFANO YA KINAYA CHA HALI KATIKA TAMTHILIA YA *KIGOGO*

Tungetarajia nchi ambazo zimepigania uhuru na kupata ukombozi wa kujitawala, kujitegemea na viongozi wao kuwatawala kwa demokrasia bila kuwanyanyasa. Kinaya kinajitokeza pale Wanasagamoyo wanasherehekea miaka sitini ya uhuru lakini chembechembe za ukoloni zingali katika jimbo hilo. Kwa mfano viongozi wanafunga soko kwa madai kuwa ni chafu na litaharibu sifa ya Sagamoyo na kuwa ni kisoko cha maskini. Baada ya soko kufungwa, linasafishwa kwa ajili ya kujengewa hoteli ya kifahari. (u.k 6) Hapa hatungetarajia Kiongozi Majoka na Kenga kuwafungia maskini soko pale walikuwa wanapata mtaji wao.

Mfano mwingine ni kwamba, tungetarajia wanafunzi wakisomea katika shule zinazomilikiwa na viongozi wapite na wajitegemee aushini mwao. Kinaya kinajitokeza pale wanafunzi katika shule inayomilikiwa na viongozi kama vile Majoka wanaishia kuwa makabeji (wanaathirika kiakili) baada ya kujidunga sumu ya nyoka yaani kutumia mihadarati (u.k 16).

Hatungetarajia viongozi kuwatia watu mbaroni bila makosa. Kinaya kinajitokeza pale tunapata Majoka akiamrisha askari wamfunge Ashua korokoroni kwa kuwa alikataa kujihusisha naye kimapenzi, huku wenye kuiba mali za umma na kulangua dawa za

kulevya kama vile Kenga na Majoka wakiwa huru (u.k 26). Tena tunawaona viongozi wakiamrisha askari kutumia nguvu zaidi kwa waandamanaji wanaotetea hali ya juu ya maisha. Majoka anamwambia Kenga:

*"Tangaza kuwa maandamano hayo ni haramu kasha uwaamuru maafisa wa polisi watumie nguvu zaidi*. (u.k 76)

Kinaya kinajitokeza pale jeshi la polisi linalopaswa kuwalinda raia wake ndio wanawaangamiza raia.

Isitoshe, tunawaona wasomi wenye shahada katika jimbo la Sagamoyo wakiishia kufanya kazi duni kama vile kuuza matunda (uchuuzi anaofanya Ashua) . Tunaona Majoka akimwambia Ashua, "*Ulipofuzu nilikupa kazi katika Majoka and Majoka Academy kaukataa.. Shahada yako ya ualimu ukataka iozee huko sokoni. Sasa ungekuwa mwalimu mkuu katika mojawapo ya shule zetu za kifahari. Maisha yako yangekuwa tofauti kabisa"* (u.k 26).

Kinaya kinajitokeza pale tunaona kwamba Ashua alikuwa na shahada lakini anakosa kazi ya kiserikali. Pia Sudi anachonga vinyago sokoni Sagamoyo na amesoma hadi chuo kikuu lakini akakosa kazi.

Ni jambo la kushangaza kumwona mwanamume akiringia biashara ya mkewe. Katika tamthilia ya *Kigogo*, Boza anaringia biashara ya uokaji wa keki wa mkewe Asiya aliyokuwa amepewa kandarasi na Majoka (u.k 64). Hapa kinaya kinajitokeza pale ambapo tunaona kwamba mkewe Asiya alikuwa anafanya uzinzi na Ngurumo ili apewe kandarasi hiyo.

Mfano mwingine unajitokeza pale ambapo viongozi wanawapatia watu vibali vya kuuza pombe haramu iliyokuwa ikiwaangamiza na kufanya wengine kuwa vipofu (u.k 61). Katika tamthilia ya *Kigogo,* tunampata Majoka akimpatia Mama pima kibali cha kuuza pombe haramu. Hiki ni kinaya kwa kuwa, tungetarajia kiongozi Majoka awalinde wananchi wa Sagamoyo lakini tunapata kwa anahatarisha maisha yao.

Pia, katika tamthilia ya *Kigogo,* tunampata mwanamume anayemwita mkewe nyanya yake. kinaya kinajitokeza pale tunamwona Majoka akimfikiria Husda kuwa ni nyanya yake, na kumweleza udhaifu wake kwa kumwambia kwamba anapenda mali yake akifikiria kuwa alikuwa anaongea na nyanya yake. Anamwambia mkewe Husda:

*"Nyanya tafadhali Husda hanipendi. Anazipenda mali zangu. Hayo si mapendo ya dhati'*. (u.k 97).

Tena hatungetarajia kiongozi kuharibu misitu kwa kukata miti ovyoovyo. Katika tamthilia hii ya *Kigogo*, kinaya kinajitokeza pale Majoka analegeza sheria za misitu na kuharibu mazingira badala ya kuidhibiti. Siti anamwambia Hashima,

"*Na Kigogo amefungulia biashara ya ukataji miti tena*.' ( U.k 56)

### 3.4 MIFANO YA KINAYA CHA MAZUNGUMZO KATIKA TAMTHILIA YA *KIGOGO*

Hatungetarajia mhusika ambaye anadharauliwa na kiongozi kusema kwamba huyo kiongozi anamheshimu. Mfano Sudi anamwambia Kenga: "*Samahani sana. Sikujua Mzee Majoka ananiheshimu sana hivyo'*. (u.k 13). Maneno haya alimwambia wakati Kenga alisema kuwa kiongozi Majoka wa Sagamoyo alikuwa amemtuma kwake ili akubali kumchongea kinyago. Usemi huu wa Sudi ni kinaya kwa kuwa Majoka hakuwa anamheshimu kwa kuwa alikuwa anapinga utawala wake. Isitoshe, tunamwona Majoka baadaye akimtia mbaroni mkewe Sudi anayeitwa Ashua.

Tena hatungetarajia kiongozi kumhadaa maskini kwamba anaweza kumpatia kila kitu anachohitaji. Katika tamthilia ya *Kigogo,* Majoka anamwambia Ashua anaweza mpatia kila kitu katika maisha yake. Anasema:

"*Naweza Ashua. Naweza kila kitu. Niangalie, niambie, ni nini nisicho nacho mimi katika milki yangu isipokuwa wewe?*". (u.k21)

Maneno haya ya Majoka ni kinaya kwa kuwa wakati Ashua anaenda katika ofisi yake, tunaona yeye Majoka anakataa kumsaidia kwanza anataka kujihusisha naye kimapenzi na anpokataa, anatiwa mbaroni bila makosa yoyote.

Pia, tunagundua kuwa wake wa viongozi hukisia kuwa akinamama wakienda ofisini mwa wanaume wao kuwa ni hawara. Wakati Ashua anaenda kwa ofisi ya Majoka kuomba msaada, Husda anatishia Ashua kuwa atamuua kwa kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mumewe. Anasema:

*"Leo nitaua mtu mie. Nitakumaliza Ashua. Majoka haonekani kwake, kisa na maana ni wewe. Huwezi kunitoa tonge kinywani hivi hivi. Umenizidi nini kwani*?' (u.k 27). Hiki ni kinaya kwa kuwa Ashua alikuwa amekataa rai za Majoka za kufanya mapenzi naye na wakati Husda anamwita hawara hiki ni kinyume cha matarajio yetu.

Isitoshe hatungetarajia kiongozi akimwita mpinzani wake muungwana. Kwa mfano tunaona Kenga akimwita Sudi Muungwana. MajpAnamwammbia:

"*Nawe muungwana wamchonga nani?"* (u.k 10).

Hiki ni kinaya kwa kumwita muungwana kwa kuwa Sudi alikuwa anapinga utawala wa Majoka  Kenga alikuwa mshauri mkuu wa Majoka naye Sudi alikuwa mwanaharakati aliyekuwa anaongoza maandamano kupinga uongozi wa Majoka.

Tena, kuna viongozi wanaosema watawafundisha wapinzani wao. Mfano katika tamthilia ya *Kigogo* Majoka anasema kwamba atamfundisha Tunu ambaye alikuwa mpinzani wake. Anasema:

" *Nitamfundisha Tunu mambo ambayo hakufundishwa nyumbani na mamake wala chuoni na maprofesa wake. Hivi vishahada vyao wanavyovipata siku hizi vinawavimbisha vichwa. Mtu anaitwa daktari na hata kazi ya maana hana"* (u.k 32).

Hapa kinaya kinajitokeza pale tungetarajia Majoka kumfundisha Tunu mambo ya kisiasa lakini tunaona kwamba anapanga njama ya kuuawa kwake.

Pia, tungetarajia kwamba nchi ambazo zinategemea nchi zingine kwa mikopo na msaada mwingine, zisijitanue kwamba zinajiweza. Kwa mfano ni kinaya kwa Majoka kusema kwamba Sagamoyo wanajiweza. Anasema,

"*Na hawa wafadhili wao nao lazima wavunje kambi zao. Sagamoyo twajiweza'*. (u.k 33).

Hiki ni kinaya kwa kuwa wanaSagamoyo hawajiwezi kwa kuwa  wanakopa pesa kutoka mataifa ya kigeni ili kujikimu.

Isitoshe viongozi wanawakaribisha wapinzani wao katika ofisi zao na kuwaita waungwana. Mfano, Sudi na Tunu wanapofika katika ofisi ya Majoka, yeye anasema:

"*Karibuni waungwana ; Viongozi wa usoni wa Sagamoyo*" (u.k 39).

Hapa kinaya kinajitokeza hapa kwa kuwa Majoka hata alikuwa amepanga njama ya kumwangamiza Tunu kwa kuwa alikuwa amegundua kuwa alikuwa na wafuasi wengi kumshinda.

### 3.5 KINAYA CHA DRAMA KATIKA *CHOZI LA HERI*

Hiki ni kinaya kinachojitokeza wakati msomaji anapojua jambo muhimu kuhusu hsdithi ambalo mhusika mmoja au zaidi katika hadithi hawalijui. Maelezo haya yanaungwa mkono na Mbatiah (2001) anayesems kwamba mhusika anaweza kuelewa jambo la mhusika mwingine ambaye halielewi.

Mfano, katika riwaya ya *Chozi la Heri* tunapata daktari ambaye amesoma na akapata shahada ya udaktari akiamini mambo ya ushirikina. Wakati familia ya Ridhaa ilipoteketezwa na jirani yake mzee Kedi, tunaona Ridhaa akianza kuwazia mambo ya ushirikina kama vile mwandishi anavyoelezea kama vile:

*Anakumbuka kupepesa kwa jicho lake la kulia kwa muda wa wiki mbili mtawalia. Anakumbuka anguko ambalo alianguka sebuleni mwake, akatafuta kilichomfanya kujikwaa asikione. Anakumbuka mavune yaliyouandama mwili wake na kunyong'onyeza kwa muda hata pasi na kuudhili kwa kazi yoyote ya haja. Anakumbuka jeshi la kunguru lililotua juu ya paa la maktaba yake ya nyumbani adhuhuri ya juzi ile. Anakumbuka mlio wa kereng'ende na bundi usiku wa kuamkia siku hii ya kiyama.(u.k1)*

Maelezo haya yanaonyesha jinsi Ridhaa alivyokuwa akiamini mambo ya ushirikina jambo ambalo hatungetarajia kutoka kwake kwani alikuwa daktari. Msomaji wa riwaya hii anaelewa fika kuwa familia ya Ridhaa iliteketezwa kutokana na uhasama ya kisiasa

pale ambapo alikuwa anasingiziwa kuwa alimteua kiongozi mwanamke Mwekevu badala ya kumteua Mwanzi ambaye alikuwa mwanamume.

Tena tunaona nyanya ya Ridhaa akimwambia kuwa hafai kulia wakati familia yake ilipoteketezwa. Yeye anamwambia:

*"Ridhaa mwanangu,mwanamume hufumbika hisia.Machozi ya mwanamume hayapaswi kuonekana hata mbele ya majabali ya maisha. Huku ni kujiumbia hasa. Unyonge haukuumbiwa majimbi; ulitunukiwa makoo."(*u.k 2*)*

Hapa kinaya kinajitokeza pale tunaelewa kuwa Ridhaa alifaa kulia kwa sababu ya kuteketezwa na ikaangamia kwa hivyo nyanya yake hakuwa akimaanisha kuwa Ridhaa hafai kulia.

Pia, Ridhaa anamsikia marehemu Becky akimwita na hatungetarajia Becky kumwita babu yake kwa kuwa alikuwa amefia kwenye mkasa wa moto. Mwandishi anasema:

" *Anamsikiia mjukuu wake, Becky, akimwita…"* (u.k 5).

Hapa kinaya kinajitokeza pale mwandishi anatwambia kuwa Ridhaa anaongea na mjukuu wake ilhali msomaji anaelewa fika kuwa mjukuu wake Becky alikuwa amefariki na kuwa hawezi ongea na babu yake.

Tena, Tila anamwambia baba yake kuhusu mtoto wa miaka hamsini ambaye hajui kusimama. Tila anamuuliza  baba yake:

"*Baba, umewahi kumwona mtoto wa miaka hamsini ambaye hajasota; sikwambii kusimama dede?"* (u.k 5).

Hapa kinaya kinajitokeza pale tunamwona baba yake hakuwa anaelewa vile Tila alikuwa akimuuliza lakini msomaji anaelewa fika kuwa mtoto wa miaka hamsini ni nchi ambazo zilipata uhuru  miaka hamsini iliyopita lakini bado ziko nyuma kimaendeleo na bado zinazidi kutegemea nchi zingine.

Pia katika riwaya ya *Chozi la Heri,* tunaona kuwa mwanamume mwenye wake wengi alihesabiwa kuwa mkwasi kwelikweli. Mzee Mwimo Msubili ana wake kumi na wawili na madume ishirini. Ardhi yake ilikuwa haitoshi kuyalelea madume yake ishirini. Iligawanywa hadi ikawa vikataa, ikalimwa na kupaliliwa mpaka ikachoka. Hatimaye mzee Mwimo Msubili alijiona amekabiliwa na kibarua kigumu cha kuvilisha vinywa hivi kutokana na zao dogo alilolipata (u.k 8). Kinaya kinajitokeza pale tunamwona huyu mzee Mwimo Msubili akiwahamishia wake wawili wwa mwisho Msitu wa Heri au ughaishu.

Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale mzee Mwimo Msubili anajitaja kuwa mkwasi kutokana na kuwa na wake wengi lakini tunaona kuwa anashindwa kuilisha familia yake lakini msomaji anaelewa kuwa  mzee Mwimo Msubili alikuwa maskini hohe hahe kwa kuwa alishindwa kuilisha familia yake na hata akaihamishia kwa msitu wa Heri au ughaishu.

Tena tunaona kinaya cha drama kinachojitokeza pale ambapo baada ya Ridhaa kujiunga na shule moja huko ughaishu, mwanafunzi mmoja anamwita mfuata mvua na kuwa ndiye anawaimbia kalamu zao pia kuwa ameenda katika shule hiyo kuwashinda katika mitihani yote. (u.k 10) Hiki ni kinaya cha drama kwa kuwa wanafunzi wake Ridhaa hawakuwa wanajua kuwa mama yake Ridhaa alikuwa amehamishiwa kwenye msitu wa Heri kwa kuwa kwao walikuwa wanabanana kwa kuwa walikuwa wake kumi na wawili wa mzee Mwimo Msubili na ndiposa alipelekwa katika shule hiyo. Hawa wanafunzi walikuwa

wanamsingizia kuwa alikuwa na nia ya kuwashinda katika mitihani yao na kwamba ndiye huwa anawaibia kalamu zao.

Mfano mwingine ni pale tunamwona Ridhaa anashindwa kuelewa kwa nini mzee Kedi aliteketeza familia yake na anajiuliza maswali yafuatayo:

*"Lakini ni kipi kilichosababisha hali hii?. Mzee Kedi ndiye aliyenisaidia kupata shamba hili. Mwanawe, Mhandisi Kombo, ndiye aliyeusimamia ujenzi wa jumba hili. Mkewe na mke wangu wamekuwa kama ndugu wa wa toka nitoke. Mimi mwenyewe nimeyadhamini masomo ya wapwaze wawili. Sehemu hii, hasa shamba hili, kaniuzia dadake Kedi, likiwa jangwa. Mimi binafsi nimefanya juu chini kuhakikisha kijiji kizima kimepata maji ya ambomba. Eneo ambalo awali likiitwa Kalahari sasa limetwaa rangi ya chanikiwiti*. (u.k 12)

Kutokana na maelezo haya inajitokeza kuwa Ridhaa hakuwa anajua kwamba familia yake iliteketezwa kutokana na uhasama wa kisiasa kwa kuwa yeye alimteua mwanamke Mwekevu ambaye alikuwa anapingwa na wahafidhina ambao walikuwa wamemteua kama kiongozi wao lakini msomaji anaelewa hivyo.

Tena, katika mtaa wa Tononokeni tunaona mabwanyenye ambao wamejenga majumba katika mahali ambapo pametengwa kwa ujenzi wa barabara, mengine yalikuwa yamejengwa chini ya vigingi vya nyaya za stima. Wakati wizara ya Ardhi na Makao ikishirikiana na wizara ya Uchukuzi na mawasiliano, kupitia kwa halmashauri ya kitaifa ya Barabara, ilikuwa imewapa notisi mabwanyenye wanaoyamiliki majumba wengi wao walipuuza notisis hii. Wengine walionekana wakitoa milungura hadharani, wengine wakatishia kuishtaki wizara husika kwa kile walichokiita ukuikaji wa haki za umiliki mali. (u.k 13)

Hapa kinaya kinajitokeza pale tunaona mabwanyenye haya wakidai kuwa wananyimwa haki za umiliki wa mashamba lakini msomaji anaelewa kuwa mabwanyenye hawa ni wafisadi na wanamiliki mashamba haya kwa njia za kifisadi.

Isitoshe, tunaona Kaizari akiuliza kama anaweza kumwita Subira mke wake. (u.k 16). Hapa kinaya kinajitokeza pale ambapo tunamwona Kaizari ni kama hajui mke wake lakini msomaji anajua kuwa huyo ndiye mke wake kwa kuwa wlikuwa wameoana na wakawa na watoto watatu ambao ni Umu, Dick na Mwaliko.

Mfano mwingine ni pale tunamwona Kaizari akisema kuwa kiongozi mwanamke hafai kuongoza jamii ya Wahafidhina. Kaizari anasema:

*"Siku ile baada ya kutawazwa kwa kiongozi mpya, kiongozi ambaye kulingana na desturi za humu mwetu hakustahili kuiongoza jamii ya Wahafidhina, kisa na maana, alikuwa mwanamke, mbingu zilishuka. Watu walishika silaha kupigania uhuru wao; Uhuru ambao walidai hawakupewa, walijinyakulia kwa viganja vyao*." (u.k 16)

Hapa kinaya kinajitokeza pale tunaona kuwa Baadhi ya wahafidhina wanamteua kiongozi Mwanamke kwa jina Mwekevu na msomaji anaelewa kuwa Mwekevu alikuwa kiongozi shupavu aliyekuwa na uwezo wa kuongoza Wahafidhina.

Pia, tunawaona wapinzani wa Mwekevu wakiimba nyimbo za kumsifu Mwanzi ambaye alikuwa ameshindwa katika uchaguzi. Kaizari anasema:

*"Kilichofuata maneno haya kilisikitisha. Niliwaona mabarobaro wamebeba mabango yaliyochorwa picha za mpinzani wa kiume ambaye alishindwa na Mwekevu. Wote walikuwa wakighani mkarara huu: Tawala wahafidhina tawala, Mwanzi wetu tawala Wahafidhina tawala."* (u.k 20)

Hapa kinaya kinajitkeza pale tunaona ya kwamba wapinzani wa Mwekevu wanamwimbia Mwanzi kuwa ndiye alikuwa kiongozi wao ilhali msomaji anaelewa ya kwamba Mwanzi hakuwa kiongozi kwa kuwa alikuwa ameshindwa na Mwekevu.

Istoshe, tunawaona viongozi wakiwaambia vijana warudi mashambani wakalime ilhali vijana hawana mashamba ya kulima. Kijana mmoja anayeitwa Hitman anasema:

*"... Wapo viongozi wanaopita wakipayuka, "Vijana turudini mashambani. Maeneo gatuzi yenu yanahitaji mabarobaro kama nyinyi kulisukima gurudumu la maendeleo.' Hapa ndipo unashangaa utarudi kwenye shamba lipi na tangu hapo familia yako uliiacha ikiishi kwa msaada wa wale wale waliotoka mbali kule walikotoka, wakapewa maelfu kwa maelfu ya ekari, wakajenga viwanda na maduka ya biashara, wengine wakalima mashamba makubwa makubwa huku wakidai kuwa ni njia ya kuwahakikishia wenyeji hali ya kujitosheleza kwa chakula…". (u.k 22)*

Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale msomaji anaelewa kuwa viongozi hawa wanaambia vijana waende mashambani ilhali hao hao viongozi wamenyakua mashamba yao na vijana hawana mahali pa kulima.

Pia, tunaona wakongwe ambao wanapowaomba vijana ili wawasaidie katika kupiga kura hao vijana wanateua viongozi ambao hao wakongwe hawataki. Hitman anasema:

"*Tunawasaidia vikongwe wasiojua kusoma na kuandika kumchagua kiongozi afaaye! 'Mama, unataka KIBOKO, au PAPA?' Tunamuuliza ajuza mmoja pale kijijini. 'Mimi simtaki huyu Kiboko, namtaka Papa. Kiboko hata chumvi hatoi. Afadhali Papa, amepita hapa mara tatu akatugawia kila mtu shilingi mia mia na vibaba viwili viwili vya unga,' Mama anajibu. 'Basi tia alama X kwenye picha ya Kiboko kuonyesha humtaki kabisa,'*

*anaambiwa kisha kusaidiwa kutia alama hiyo bila kujua kuwa kamchagua huyo huyo Kiboko! Sasa miaka kumi hii, tungali tunabisha hodi kwenye afisi za mabwana wakubwa, si ndugu sasa.*" (u.k 23)

Hapa kinaya kinajitokeza pale tunaona kuwa vijana wanakubali rai za vikongwe kuwasaidia katika kupiga kura na hivyo vikongwe wanafurahia kuwa wamechagua viongozi wawapendao. Kinyume cha matarajio ni kwamba msomaji anaelewa kuwa vijana wanawalazimisha hawa vikongwe kuwasaidia viongozi wasiopenda kwa kutumia udanganyifu.

Tena, kuna viongozi ambao wanawahadaa vijana kuwa wakiwateua wakati wa uchaguzi watawaajiri kazi wazipendazo. Hitman anasema:

"*Wengine tulikuwa tumeahidiwa makubwa wakati wa vuguvugu la kuwania nafasi za uongozi. Mara, 'Ubalozi wa Emirates unahitaji kijana aliyesomea shahada ya uzamifu katika mahusiano ya kimataifa kama wewe. Utakuwa wa kwanza kufikiriwa kwa nafasi hii chama chetu kitakapochukua usukani…"* (u.k23)

Hapa tunagundua kuwa viongozi walitumia njia za uongo kuwahadaa vijana ili waweze kuwachagua na baadaye wakichaguliwa wanawasahau hawa vijana. Kinaya cha drama kinajitokeza pale tunawaona vijana wakiamini uongo wa viongozi lakini wasomaji wanaelewa kuwa huo ni uongo wa viongozi ili vijana wakubali kuwachagua.

Tena, tunawaona vijana ambao walikuwa wakiandamana kwa sababu ya viongozi kukosa kuwapatia nafasi za kazi kuuawa na polisi na tunaambiwa kuwa walikufa kifo cha kishujaa. Tunaona vile vijana walisema yale yalitokea kama ifuatavyo:

*“Hatung’atuki, walisema huku wameinua mikono yao juu. Baada ya muda mfupi vifua vyao vilikabiliana na risasi zilizorzshiwa vifua hivyo kama marashi, vifua vikawa havina uwezo dhidi ya shaba, vijana wakaanguka mmoja baada ya mwingine, wamekufa kifo cha kishujaa, wamejitolea mhanga kupigania uhuru wa dhati kama walivyouita. (u.k 24)*

Hapa kinaya kinajitokeza pale tunaona ya kwamba vijana wakisema kwamba wanapigania uhuru wa dhati lakini msomaji anajua vyema kuwa katika nchi ya wahafidhina polisi wanawaua watu ovyoovyo kama tunavyoona vijana hawa wakiuawa kinyama kwa kupigwa risasi kwa vifua vyao. (u.k24)

Tena tunaona ya kwamba katika riwaya ya *Chozi la Heri* Kaizari akitumia dini vibaya. Yeye anasema:

*“Miujiza ya Musa ilikuwa njiani. Siku ya nne baada ya mapinduzi, tulisikia hodi mlangoni. Mke wangu Subira, ndiye alikwenda kufungua. Alisalimiwa kwa kofi kubwa….Baadaye genge hili la mabarobaro watano lilifululiza hadi walipokuwa maskini mabinti wangu wawili, Lime na Mwanaheri. Sikuweza kuvumilia kuona unyama waliotendewa. Nilijaribu kwa jino na ukucha kuwaokoa lakini likawa suala la mume nguvuze! Mahasimu hawa walitekeleza unyama wao na kuniacha bila kunigusa, niuguze majeraha ya moyo. (u.k 25)*

Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale ambapo tunaona Kaizari akizungumzia kuhusu miujiza ya Musa ambayo katika bibilia ilikuwa ya heri lakini hapa msomaji anaelewa kuwa katika kisa hiki miujiza hii ilikuwa ya shari.

Mfano mwingine ni pale tunapata Selume akiondoka kwake kwa sababu ya kusimangwa na wakweze kuwa alimteua kiongozi mwanamke. Ridhaa anasema:

*"Selume alikuwa mke wa jirani yetu aliyekuwa mpinzani mkuwa wa Mwekevu. Yeye sasa ameondoka kwake kwa sababu ya kuhitilafiana kimsimamo na wakwe zake. Wakweze walidai kuwa yaya alimuunga mkono Mwekevu, kwamba yeye alikuwa mwiba ambao ulitishia kuuletea ukoo wao fedheha. Selume alishindwa kuvumilia shutuma hizi, akafunga virago vyake na kutokomea kokote kule."* (u.k 30)

Hapa tunaona ya kwamba Selume alikuwa anasingiziwa jambo la uongo. Kinaya cha drama kinajitokeza pale ambapo wakweze walikuwa wanaamini kuwa Selume alikuwa amemteua Mwekevu lakini msomaji anaelewa kuwa Selume alikuwa mpinzani wa Mwekevu.

Tena tunaona kwamba kuna wakimbizi ambao wakati waliletewa chakula cha msaada, kuna wale walijigawia mara tatu. Ridhaa anasema:

*Magunia ya mahindi na maharage, bandali za unga na madebe ya mafuta ya kukaangia yaligawiwa kila familia kwa vipimo sawa. Kuna familia moja ilijigawa, ikazaa familia nyingine mbili., zikawa familia tatu tofauti! Hatimaye Kute na aila yake waliishia kupata mara tatu ya posho ambayo wengine tulipata…"* (u.k 33)

Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale tunaona Ridhaa akisema kuwa magunia ya mahindi na maharage, bandali za unga na madebe ya mafuta ya kukaangia yaligawiwa familia kwa vipimo sawa lakini msomaji anajua kwamba kuna watu kama vile Kute ambaye alijigawia mara tatu kwa kugawanya familia yake mara tatu.

Pia tunaona kuwa wakimbizi walipoambiwa warudi kwao tunaona kwamba hawakufurahia. Mwandishi anasema:

"*Asubuhi hiyo ya kuhawilishwa kutoka msitu wa Mamba, Ridhaa alihisi kama anayetoka kanaani kwenda misri. Hakuwa na matumaini ya maisha bora, … Siku walipoambiwa kuwa watarudishwa kwao ilikuwa siku ya hisia mseto kwa wengi*. (u.k 34)

Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale ambapo tunaona wakimbizi wanapoambiwa warudi kwao wanahuzunika lakini msomaji angetarajia wawe na furaha wakati wanarudi kwtunaona Tena Mwangeka alipokuwa mtoto anajifanya kuwa daktari. Mwandishi anasema:

*"Siye baba ambaye Mwangeka kwa utundu wake wa kitoto, angemnyang'anya stethoskopu yake, na kuitia kwenye shingo yake yeye Mwangeka , kisha anamlaza baba yake juu ya kochi; baba ni mgonjwa wa Dkt. Mwangeka! Daktari anausikiliza mpigo wa moyo wa muwele wake. Baba mtu akijaribu kufurukuta anatishiwa kudungwa sindano*…" (u.k 48)

Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale tunaona Mwangeka akijifanya kuwa daktari kwa kuwa alikuwa mtoto mdogo lakini msomaji anaelewa fika kuwa Ridhaa baba yake ndiye alikuwa daktari lakini sio yeye.

Mfano mwingine ni pale tunaona Ridhaa akifikiria baba yake ni mwehu. Anajiuliza maswali yafuatayo:

*"Je, kwani baba yangu amekuwa Mwehu? Kwa nini hata hakushikana na majirani akachimba mass grave na kuyazika majivu haya?" alijiuliza Mwangeka*." (u.k 52)

Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale tunamwona Mwangeka akifikiria kuwa baba yake amekuwa mwendawazimu ilhali msomaji anaelewa fika kuwa Ridhaa hakuwa

mwehu ila alikuwa akifikiria kuhusu familia yake iliyokuwa imeteketezwa na mzee Kedi kila wakati.

Tena tunapata kuwa msitu wa Mamba uligeuka na kuwa nyumbani kwa maelfu ya watu waliogura kwao bila tumaini la kurudi kwao. Mwandishi anasema:

*"Msitu wa Mamba uligeuka kuwa nyumbani kwa maelfu ya watu waliogura kwao bila tumaini la kurudi…Matokeo ya uamuzi huu yalikuwa kukata miti kwa ajili ya kupata mashamba ya kupandia vyakula, na kwa ajili ya ujenzi; polepole mioshi ikaanza kuonekena ikifuka kutoka kwenye msitu ambao tangu hapo ulikuwa marufuku kwa binadamu".*(u.k 62)

Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale ambapo wakimbizi wanasema kwamba msitu wa Mamba ni makao yao lakini msomaji anaelewa kuwa msitu unafaa kunadhifisha mazingira na haufai kuwa makao ya binadamu. Tena tunawaona hawa wakimbizi wakikata miti ovyoovyo kwenye msitu huu na msomaji anaelewa kuwa miti katika msitu huu wa Mamba inafaa kuhifadhiwa.

Tena tunaona Annette akifuata watoto wake ng'ambo na kumwacha mumewe Kiriri katika upweke. Alimwambia mumewe kuwa amemwachia watumishi na vimada wake (u.k 65). Hiki ni kinaya cha drama kwa sababu Annette anadai kuwa mumewe ana uhusiano wa kimapenzi na watumishi wao wasichana. Msomaji anaelewa kuwa Kiriri mumewe Annette ni mwaminifu na hana uhusiano wa kimapenzi na wanawake wengine na hivyo basi alikuwa anasingiziwa ukware na mkewe Annette.

Pia, Lunga Kiriri anafutwa kazi na bwana Kalima anayemwambia katika barua kuwa amesimamiswa kazi kutokana na gharama ya uzalishaji mali ambayo inaendelea kupanda

kila uchao na kwamba shirika hiyo limekumbwa na changamoto kubwa ya kifedha (u.k72). Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale bwana Kalima anasema kuwa hakuwa amemfuta kazi lakini msomaji anaelewa kuwa Lunga Kiriri alikuwa amefutwa kazi kutokana na utetezi wake kwa maskini ili wasiuziwe mahindi na shirika hilo ambayo yalikuwa ya njano na hatari kwa usalama wa panya sambuse kwa binadamu.

Mfano mwingine wa kinaya cha drama ni pale tunaelezwa kuwa viongozi walipoona vile Lunga na wakimbizi wengine walivyokata miti na kulima mimea katika msitu wa Mamba, kisa hiki kiliwafungua macho vionngozi wakatanabahi kuwa kwa kweli wakazi hawa walikuwa wakiishi hapa kiharamu na vyombo vya habari havikukawia kutoa wito kwa chama tawala kuwatafutia watu hawa mahali kwingine (u.k 75). Baada ya wakimbizi hawa kutoka kwa msitu huu, usiku wa manane kulianza kusikika milio ya malori na matrekta yakibeba shehena za mbao, makaa na mahindi. Hiki ni kinaya cha drama kwa kuwa viongozi ndio walikuwa wanasema kuwa wanataka kutunza msiti huu wa Mamba. Baada ya wakimbizi hawa kuhama, viongozi hawa ndio wanaendelea kuharibu msitu huu.

Mfano mwingine wa kinaya cha drama unajitokeza pale ambapo Billy alimjengea mpenzi wake Sally kasri ili akukubali amuoe. Baadaye tunaona sally akilidharau kasri hilo na kusema:

"*This ia a nest. I cannot live here, not now, not ever"*.(u.k 80)

Hiki ni kinaya cha drama kwa kuwa Billy alikuwa akidhani kuwa mpenzi wake Sally atafurahia Kasri alilomjengea na hivyo basi akubali kuolewa naye lakini kinyume cha matarajio yake, Sally

Anakataa kuolewa naye akidai kuwa alikuwa amejengewa kiota na mpenzi wake Billy.

Tena tunaona kuwa Naomi mkewe Lunga Kiriri akimtoroka Lunga alipofutwa kazi. Katika barua yake kwa Lunga anasema:

*"Nimeondoka. Acha nitambe na ulimwengu, huenda nikaambulia cha kukusaidia kuikimu familia. Nasikitika kwa uchungu nitakaokusababishia wewe na wanao.Kwaheri" Naomi. (u.k 81)*

Tunaona kinaya cha drama hapa kwa kuwa Naomi anamtoroka Lunga wakati ambao alimhitaji sana. Msomaji anaelewa kuwa Naomi anamtoroka Lunga wakati alimhitaji sana na singizio lake la kumsaidia Lunga ni uongo mtupu.

Tena tunamwona Sauna akijitia uchangamfu ili aajiriwe na watu kama mfanya kazi wa nyumbani, kisha anawateka nyara watoto wa waajiri wake na kuwafanya wasichana kufanya biashara ya nipe nikupe na wavulana wanatumiwa katika biashara ya ulanguzi wa dawa za kulevya. Umu anasema:

*"Auntie Sauna! Kumbe ile imani na uchangamfu wako na ahadi ya kututunza baada ya kifo cha baba ilikuwa siasa ya kutuondoa hofu, tukuamini na kukupa fursa ya kutenda*". (u.k 84)

Hapa tunaona kwamba Sauna aliaminiwa sana na familia ya Lunga lakini akawateka nyara watoto wa Lunga yaani Mwaliko na Dickson. Kinaya cha drama kinajitokeza pale Sauna anaaminiwa sana na waajiri wao lakini msomaji anaelewa kuwa alikuwa mlanguzi wa watoto na hivyo basi hakustahili kuaminiwa na waajiri wake.

Mfano mwingine ni pale tunaona kuwa wakati Umu walikuwa na mama yake mtaani, wanakutana na mtoto mmoja wa mtaani aliyeitwa Hazina. Wakati anawaomba msaada mama yake Umu anasema:

*"These aere pretenders. They have been sent by their stinking rich relatives . I can't give them a penny"*. (u.k 8)

Katika maelezo haya kinaya cha drama kinajitokeza pale mama Umu alikuwa anawachukia watoto wa mitaani na msomaji anajua kuwa si watoto wote wa mitaani huwa wanafiki.  Kuna wale ambao wazazi wao huaga dunia na wengine kutengwa na familia zao. Kinaya cha drama kinajitokeza pale ambapo tunatarajia mama Umu amsaidie omba omba huyo lakini alikataa. Umu ndiye alimsaidia kwa kumpatia shilingi mia mbili.

Tena tunaona Hazina ambaye alikuwa  omba omba wakati anasaidiwa na Umu akimwahidi kuwa siku moja atamsaidia. Yeye alisema:

*"Poa sana sistee, we ni mnoma. Siku moja nitakuhelp hata mimi*. (u.k 86)

Hapa ni pale tunaona kuwa Umu na mama yake hawakuamini kuwa Hazina ambaye alikuwa omba omba mtaani anaweza kuwasaidia lakini msomaji anakuja kugundua kuwa Hazina alimsaidia Umu wakati alikuwa na matatizo ya kutorokwa na mama yake, baba yake akaaga dunia na ndugu zake Dick na Mwaliko kutekwa nyara na Sauna.

Mfano mwingine ni pale tunaona Mwanaheri akisimulia kuhusu mama yake. Yeye anasema:

"*Nyanya alimwona mama kuwa chanzo cha kuharibiwa kwa mali yetu, kwamba ndiye aliyewafanya majirani zetu kutuchomea boma ili watuondolee gugu ambalo liliutia najisi utambulisho wetu."*. (u.k 95)

Hapa tunaona kuwa nyanya yake Mwanaheri alikuwa akimsingizia Subira ambaye alikuwa mama yake kuwa ndiye chanzo cha matatizo waliyoyapitia lakini msomaji anaelewa kuwa vita vilitokana na wapinzani wa Mwekevu ambao walikuwa wanashambulia wafuasi wa Mwekevu kwa kuwa kiongozi Mwanzi waliokuwa wakimuunga mkono alishindwa na Mwekevu.

Pia, Subira anatoroka kwake kwa sababu ya chuki kutoka kwa mama mkwe. Katika barua yake kwa Mwanaheri anasema:

*"Nimechoka. Nimechoka kukilovya kifua change kwa machozi kila mara. Nimechoka kuitwa mwizi wa mayai ambayo kuku wenyewe watagao nimewafuga mimi! Nimechoka kupigania penzi la mwenzi na mavyaa, na mwenzi mwenyewe haoni ananipagaza machungu.*" (u.k 96)

Hapa kinaya kinajitokeza pale ambapo hatungetarajia mama mkwe wa Subira kumchukia bure. Msomaji anaelewa kuwa Subira kuitwa mwizi wa mayai ya kuku anazotaga ni kumaanisha kuwa mamamkwe alikuwa na chuki kwake.

Mfano mwingine ni pale tunaona kuwa Chandachema akiwaambia wanafunzi wenzake wasimuulize yale aliyaona. Yeye anasema:

*"Usiniulize niliyaona na kuyasikia mangapi katika chumba hiki ambacho kiligeuka danguro wakati Bi. Kimai alipokuwa ameenda mashambani. Wakati huu bwana Tenge angeamua kumleta mwanamke mmoja baada ya mwingine, hapo hapo, mbele ya macho*

*ya wanawe, hadi usiku wa kuamkia siku ya kurudi kwa Bi. Kimai. Mara mojamoja Bi. Kimai angerudi bila kutarajiwa na kumshika ugoni mke mwenzake! Mwaka mmoja, miwili, mitatu…"* .(u.k 106)

Kinaya kinajitokeza pale ambapo msomaji anatarajia wanafunzi wenzake Chandachema wamuulize yale aliyoyashuhudia kwa bwana Tenge lakini anawaambia kuwa wasimuulize kuhusu ukware wa bwana Tenge.

Tena, tunaona ya kwamba Dick baada ya kuuzwa kwa Buda na kulazimishwa kuuza dawa za kulevya akitamauka na kusema:

*"Potelea mbali, lisilo budi hutendwa. Hii ndiyo riziki niliyoandikiwa na mwenyezi mungu. Ikiwa kweli haya siyo niliyoumbiwa, kwa nini Mungu akaamua baba yangu mpendwa? Kwa nini akampagaza mama yangu ubinafsi na wazimu uliomfanya kuiacha familia yake? Kwa nini akamtuma kijakazi Sauna kuja kuisambaratisha familia ya baba? Haya ndiyo aliyoyataka mungu kwani, tangu nitoswe kwenye dimbwi hili, hakujatokea isimu ya mtu, hata dada yangu mpendwa Umu , kuja kunitafuta…*" (u.k 123)

Hapa kinaya cha drama kinajitokeza mara mbili. Ya kwanza Dick anasema kuwa hiyo ndiyo riziki aliyoandikiwa na mwenyezi mungu. Msomaji anaelewa kuwa hiyo si riziki yake kwa kuwa alitekwa nyara na kijakazi Sauna na akalazimishwa kulangua dawa za kulevya. Kinaya cha drama tena kinajitokeza pale tunaona kuwa Dick anasema kuwa hata dada yake Umu hakumtafuta na msomaji anaelewa kuwa Umu alikuwa anamtafuta kila mahali na hata akaripoti kwenye kituo cha polisi.

Tena tunaona Dick akiongea na nafsi yake kama ifuatavyo:

*"Dick, hii kazi ni ya kujiumbua. Jitazame hapo ulipo. Umepata pesa nyingi katika umri mbichi. Lakini je, una utulivu?  Ni mara ngapi umeponea tundu la sindano kunaswa na mashine za forodha? Je, isingekuwa mwajiri wako kuvilainisha viganja vya maafisa wa forodha,wewe na wenzako msingekuwa mmeozea kwenye magereza ya kitaifa na kimataifa kama wengine wengi wanavyofanya?..."* (u.k123)

Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale ambapo tunaona ya kwamba Dick amepata pesa nyingi lakini msomaji anaelewa kuwa amepata pesa hizo kutokana na biashara haramu aliyokuwa akilazimishwa kufanya na Buda ya kulangua dawa za kulevya.

Pia tunamwona Shamsi anapolewa  anatembea usiku wa manane akiimba wimbo ufuatao:

*"Chupa yangu, najua wananicheka hawa*

*Wachunguliao kwenye madirisha*

*Walio kwenye roshani zao*

*Wakipunga pepo baada ya*

*Kujaza matumbo yao*…''(u.k 130)

Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale tunaona kwamba ni usiku wa manane na Shamsi anafikiria kuwa kuna watu wanamchungulia wakiwa kwenye Roshani zao. Msomaji anaelewa kuwa hakuna mtu ambaye alikuwa anamchungulia kwa kuwa walikuwa wamelala usiku huo wa manane.

Tena katika wimbo wa Shamsi tunapata yeye na wafanya kazi wengine wanaajiriwa kazi ambayo wanalipwa mishahara duni. Wanapoomba waajiri wao wawaongezee mishahara yao ili iimarike, wanaambiwa:

*"Nyinyi ni unskilled labourers,*

*Mishahara mlonayo*

*Ni kufu yenu*". (u.k 133)

Kinaya cha drama kinajitokeza pale tunaona kwamba Shamsi na wenzake walikuwa wanadhani kwamba wataongezewa mishahara yao lakini msomaji anaelewa kuwa hawangeongezewa mishahara yao.

Pia tunampata msichana anayeitwa Tuama ambaye anaunga mkono upashwaji wa tohara kwa wasichana. Yeye anasema:

"*Kupashwa tohara si mila iliyopitwa na wakati. Bila tohara mwanamke hubakia kuwa mtoto. Nisingepashwa tohara nisingeolewa. Msiba uliowapata wenzangu ni bahati mbaya tu.*" (u.k 144)

Hapa kinaya kinajitokeza pale tunampata Tuama akiwa hospitalini kwa sababu ya kuvuja damu nyingi baada ya kupashwa tohara. Yeye anaendelea kuunga mkono upashwaji wa tohara kwa wasichana lakini msomaji anaelewa kwamba kupashwa tohara kwa msichana kuna madhara mengi kama vile tatizo la kuvuja damu.

Tena tunamwona Pete akinywa sumu ya kuulia panya akiwa na matumaini ya kuaga dunia baada ya panda shuka za maisha. (u.k 152) Kinaya cha drama kinajitokeza pale Pete anatarajia kuaga dunia lakini haikuwa hivyo kwa sababu tunamwona katika hospitali akitibiwa na daktari na akapata nafuu.

Mfano mwingine ni pale tunampata Sauna akiwa amebakwa na babake na baada ya kupata uja uzito na kumpasulia mamake mbarika kuwa alinajisiwa na babake yeye anamwambia:

*"Mwanangu usimpake tope baba yako. Amekulea kwa miaka yote hii kama mwanawe, japo kwa kweli hakukuzaa wewe. Ndiye alinivua kutoka kwenye umaskini alionipakaza baba yako mzazi baada ya kujizika kwenhy unywaji wa dengelua mitaani na kujisababishia kupigwa kalamu. Msamehe bwana Maya. Hakuna mja aliyekamilika."* (u.k 155). Hapa kinaya kinajitokeza pale tunamwona Sauna akimshtaki baba yake kwa mama yake kuwa ndiye alikuwa amemnajisi na akaambulia uja uzito. Sauna alikuwa anafikiria kuwa mamake angemchukulia baba yake hatua kali lakini yeye anamsaidia Sauna kuavya mimba hiyo na kukosa kumchukulia baba yake hatua kali.

Tena, Sauna anasema vile kabla ya kuingilia biashara ya ulanguzi wa watoto alikuwa anaami niwa na watu waliokuwa wanamnunulia maji ambayo yalikuwa chafu. Yeye anasema:

*"Asubuhi moja mbichi ilinipata kwenye baraste kuu; nimeamua kutamba na ulimwengu. Nimefanya kazi katika machimbo yam awe, nimewahudumia waungwana kwa namna zote katika majumba ya kuuzia pombe, nimeuza maji ya mito na madimbwi yaliyotiwa kwenye chupa zenye vibandiko vya kuvutia, ati ni mineral water…" (u.k 156)*

Kinaya kinajitokeza pale Sauna alikwa anawauzia watu maji ambayo hayakuwa safu. wanaouziwa maji na Sauna wanafikiria kuwa ni safi bila kujua kuwa hayo maji yalikuwa yamechotwa kwa mito na madimbwi halafu yakatiwa kwenye chupa zenye vibandiko vya kuvutia ati ni 'mineral water.' (u.k 156)

Mfano mwingine wa kinaya cha drama kinajitokeza pale mwandishi anatwambia kuwa hatimaye Sauna alijiingiza katika ulanguzi wa binadamu na tukio hilo likageuka kuwa ngozi yake. Kulingana na msomaji, ulanguzi wa binadamu ni tukio ambalo linadhihirisha ukatili wa Sauna lakini Sauna anaona likiwa jambo nzuri. (u.k 165)

Tena tunapata kuwa wamama wanapata watoto na kuwatupa ovyo ovyo. Neema anapokuwa akipita njiani alipata mtoto ambaye alikuwa ametupwa. Yeye anasema:

"*Hapo hapo katikati mwa kilima hiki cha taka, niliona karatasi ya sandarusi ikifurukuta katikati ya fondogoo la kila aina. Kufurukuta huku kuliandamana na kilio kile hafifu. Moyo uliniambia nijipitie kama walivyofanya wenzangu, hata baada ya kuniona nikichunguza kilichosetiriwa na mchafukoge huu wa vitu*." (u.k 161)

Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale tunawaona wamama wakijifungua watoto kisha kuwatupa njiani na wanaona jambo hilo kama linafaa sana lakini msomaji anaelewa kwamba huo ni ukatili.

Tena tunaona mpita njia mmoja akimwambia Neema asikiokote kitoto kilichokuwa kimetupwa. Neema anasema:

"*Sauti ya mpitanjia mwenzangu ikaniambia, "Usijitie kubeba mzigo ambao si wako. Je, umepata vijusi vingapi hapahapa vimetupwa, vikajifia? Je, iwapo huu ni mtego wa kukupagaza wizi wa binadamu, utakuwa mgeni wa nani*? (u.k 161)

Hapa tunaona kinaya pale tunaona ya kwamba mpitanjia mmoja akimwambia Neema kuwa asikiokote kitoto hicho lakini kwa msomaji ni bayana kuwa anaelewa fika hicho kitoto kinafaa kuokotwa na kulindwa vyema.

Mfano mwingine ni pale tunapata kuwa mwanamke anapokosa mtoto katika nchi ya Wahafidhina hata kama ana elimu anaonekana kama hajakamilika. Neema anasema:

"*Kumbe hata mja akafanikiwa vipi kielimu na kitaaluma, maisha yake huwa ombwe bila mwana, awe wa kuzaa au wa kulea?" (u.k 165)*

Hapa kinajitokeza pale msomaji angetarajia mja ambaye amesoma aheshimiwe hata kama hana mtoto kwa kuwa kuna wale ambao wana maumbile ambayo hawawezi kupata watoto.

Pia tunawaona wanaume wanaoamini kuwa wakipatana na wanawake asubuhi hiyo ni nuksi.

Kwa mfano Ridhaa anasema:

*"Nau (Baba) husema kwamba kumwona mwanamke asubuhi ni nuksi kwa kuwa mtu hafanikiwi kwa atakalo.*" (u.k 184)

Hapa kinaya kinajitokeza pale ambapo tunaona kuwa wanaume wanaamini mambo ya ushirikina kwa kuwa wanaamini kuwa wakipatana na wanawake asubuhi hiyo ni nuksi. Msomaji anaelewa kuwa kupatana na wanawake asubuhi ni jambo la kawaida tu na hakuna nuksi yoyote.

Tena, tunaona kuwa wanaume wanapowaajiri wanawake katika biashara zao, wanawarai kuwa wawe na uhusiano wa kimapenzi nao na wakati wanakataa wanafutwa kazi. Mfano tunaona Kimbaumbau alipomwajiri Naomi akimrai wawe na uhusiano wa kimapenzi ili aendelee kumdumisha katika biashara yake. Wakati Naomi anakataa, anafutwa kazi. Kinaya cha drama kinajitokeza pale ambapo Kimbaumbau anaonelea kuwa ni vyema awe

na uhusiano wa kimapenzi na anapokataa anafutwa kazi. Msomaji anaelewa kuwa si vyema Kimbaumbau kumrai Naomi kuwa na uhsiano wa kimapenzi naye ili amdumishe kwa kazi.

## 3.6 KINAYA CHA DRAMA KATIKA TAMTHILIA YA KIGOGO

Mfano ni pale tunaona Boza ambaye alikuwa anasema hapo awali kuwa hakuna maembe matamu kama ya Ashua akisema kuwa maembe hayo ya Ashua kuwa yananuka fee. (u.k 1) Kinaya cha drama kinajitokeza pale tunaona ya kwamba Maembe ya Ashua yananuka lakini kwa msomaji anaona kuwa yalikuwa matamu kwa kuwa Sudi anakula bila kulalamika.

Tena, Kombe anaposema kuwa wanalipa kodi na viongozi hawawashugulikii, Boza anamwambia kuwa aache kulalamika kwa kuwa ni jukumu la viongozi kukusanya kodi na anamwambia Boza kuwa ni jukumu lake kulipa kodi. Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale ambapo msomaji anaelewa kuwa Wanasagamoyo wanalipa kodi lakini soko lao pale ambapo huwa wanafanyia biashara zao pahali penye uchafu na uvundo na hivyo basi ni dhahiri shahiri kuwa ile kodi wanalipa ni kazi bure kwa sababu inatumiwa na viongozi kujitajirisha na wao wanaendelea kuwa fukara na pia wanakosa mazingira safi.

Isitoshe tunaona mjumbe akitangaza kuwa watu washerehekee uhuru kwa mwezi mmoja. Yeye anasema:

*"Yafuatayo ni matangazo maalumu. Wananchi watukufu wa Jimbo la Sagamoyo mnatangaziwa kuwa kipindi cha mwezi mzima wa kusherehekea uhuru wetu kitaanza*

*kesho. Katika kipindi hiki adhimu, mnatakikana kuwakumbuka majagina wetu wa uhuru; waliopigana ili kutunasua kutoka kwenye silisili za utumwa*. (u.k 4)

Kinaya kinajitokeza pale ambapo tunapata kuwa, Wanasagamoyo wanaambiwa kuwa washerehekee uhuru kwa mwezi mmoja. Msomaji anaelewa fika kuwa wao ni maskini hohe hahe na hawawezi kukosa kufanya kazi zao kwa mwezi mmoja wakisherehekea uhuru.

Pia tunamwona mjumbe akisema kwamba, Wanasagamoyo wanajivunia kuwa na kampuni kubwa zaidi ya uzalishaji sumu ya nyoka barani. (u.k 4) Hiki ni kinaya cha darma kwa kuwa msomaji anaelewa kuwa hii kampuni ni ya kutengeneza dawa za kulevya na hivyo haifai kusherehekewa kwa kuwa imewafanya vijana wengi wafe na wengine kupofuka kwa sababu ya kutumia dawa za kulevya.

Mfano mwingine ni pale tunaona kuwa mjumbe anacheza wimbo wa kizalendo kama ifuatavyo:

*"Twajivunia Saga ni jimbo letu tukufu,*

*Jimbo tunalolipenda, daima...*

*Sagamoyo tunalilinda, daima…*

*Twamtukuza Ngao kiongozi wetu shupavu,*

*Kwake Ngao tunasujudu, daima...*

*Ngao wetu twakuhusudu, daima…"* (u.k 5)

Katika wimbo huu tunaona kinaya cha drama kwa kuwa msomaji anaelewa kuwa watu hawajivunii Sagamoyo kwa kuwa kuna mauaji ya watu wengi kiholela bila makosa yoyote. Pia uchafu umejaa Sagamoyo kwa kuwa viongozi hawalisafishi soko la Sagamoyo ilhali watu wanalipa kodi. Tena soko lao walilokuwa wanategemea la Chapakazi limefungwa na Majoka ili ajenga hoteli la kifahari.

Pia tunaona Boza akimsingizia Sudi kuwa ana uhusiano wa kimapenzi na Tunu. Boza anamwambia Sudi:

*"Si huyo Tunu wako. Una mke na bado mnafuatana kama mtu na kivuli chake…eti watetezi sijui wa nini*"*…* (u.k 5)

Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale msomaji anaelewa fika kwamba Sudi ana mke anayeitwa Ashua na hana uhusiano wa kimapenzi na Tunu na hivyo basi alikuwa anasingiziwa kuwa ana uhusiano wa kimapenzi na Tunu. Tena msomaji anajua kuwa Sudi na Tunu ni watetezi wa haki za Wanasagamoyo na wanawakomboa Wanasagamoyo kutoka kwa minyororo ya utumwa wa kiongozi Majoka kwa kumteua Tunu kama kiongozi wao.

Pia tunamwona Kombe akiwaambia wachonga vinyago wenzake:

*"Punguzeni joto… Hamjasikia kuwa tunasherehekea uhuru*?" (u.k 6)

Kinaya cha drama kinajitokeza pale ambapo Kombe anasema kuwa wanasherehekea uhuru. Msomaji anaelewa kuwa Wanasagamoyo hawasherehekei uhuru kwa kuwa bado wanaendelea kudhulumiwa na viongozi tawala. Kwa mfano tunaona kuwa viongozi wa Sagamoyo wanakata miti na kuharibu misitu. Mvua inapokosa kunyesha wao wanajichimbia visima na kuwaacha Wanasagamoyo wakiteseka kwa kukosa maji.

Tunaona kuwa siku iliyokuwa imepangwa na Majoka ili Wanasagamoyo washerehekee, watu wanakosa kusherahekea kwa kususia mkutano walioandaliwa na Majoka na wakaenda kumsikiliza Tunu kwa lango kuu la Sagamoyo.

Mfano mwingine ni pale tunaona Boza akiwaambia Sudi na Kombe kuwa Majoka ambaye ni kiongozi wa Sagamoyo amepanga kutoa chakula cha kutosha kwa wale wasiojiweza. (u.k 6) Hiki ni kinaya cha drama kwa kuwa kiongozi wa Sagamoyo ambaye kwa jina ni Majoka hakuwa anamaanisha kwamba anaweza kupatia maskini chakula kwa kuwa wakati Ashua alienda ofisini mwake kumuomba chakula alimwambia kwamba lazima ajihusishe naye kimapenzi ili amsaidie na hivyo msomaji anaelewa kwamba Majoka hawezi kupatia wasiojiweza chakula na kwamba huo ulikuwa uuongo mtupu.

Tena tunaona Kombe ambaye alikuwa mchonga vinyago akisema kuwa anajiweza. (u.k 6). Hiki ni kinaya cha drama kwa kuwa Kombe hakuwa akimaanisha kwamba anajiweza kwa kuwa yeye ni maskini na tunaona akimtegemea Majoka amsaidie hata ampatie kandarasi ya kumchongea kinyago.

Pia, mfano mwingine ni pale tunapata Asiya na Ngurumo wakimhonga Husda ili wapate kandarasi ya kuoka keki ya uhuru. Boza anasema:

*"Aikose? Asiya ni mwanamke halisi bwana! Amemweka Bi Husda hapa. Yeye na Ngurumo walimwandama Bi. Husda hadi wakapewa kandarasi*." (u.k 7)

Kinaya cha drama kinajitokeza pale Boza anasema kwamba Asiya ni mwanamke halisi lakini msomaji anaelewa kwamba Husda alikuwa fisadi kwa kuwa anatoa hongo kwa Asiya ili apewe kandarasi hiyo ya uokaji wa keki ya uhuru.

Mfano mwngine ni pale tunaona kwamba Majoka kupitia kwa mjumbe, wanatangaza kuhusu mashujaa waliopigania uhuru. Sudi anasema:

*"Hizo taarifa za Majoka zitakufaa vipi? Hazikuongezei tonge! Eti wanawatangaza mashujaa, mashujaa gani? Tunahitaji kuiandika historia yetu upya.* (u.k 8)

Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale tunaona kwamba Majoka anasema kwamba mashujaa washerehekewe lakini msomaji anaelewa kuwa hakuna mashujaa waliopigania uhuru Sagamoyo kwa kuwa wale ambao wanatangazwa sio mshujaa halisi. (u.k 8)

Isitoshe washauri wa viongozi wanachukiwa na raia. Katika tamthilia ya *Kigogo*, tunampata sudi akimwambia Kenga:

*"Mshauri mkuu na binamuye Majoka amelitembelea soko la walalahoi . Lo! Sasa ninaamini kuwa tunasherehekea miaka sitini tangu uhuru.*"

Kinaya cha drama kinajitokeza pale ambapo Sudi anamwita Kenga mshauri mkuu wa Majoka. Msomaji anaelewa kuwa Kenga alikuwa anamshauri Majoka vibaya kwa mfano akamshauri Majoka kumtoa uhai mpinzani wake Jabali na akauawa. Tena Sudi anasema kuwa Kenga amewatembelea katika soko la walalahoi na hapa msomaji anaelewa kuwa hiki ni kinaya cha drama kwa kuwa kulikuwa na utabaka kati ya walalaheri na walalahoi na Kenga kuwatembelea kilikuwa ni kinaya.

Tena, kinaya cha drama kinajitokeza pale Kenga anamuuliza Sudi:

*"Nawe muungwana wamchonga nani*? (u.k 10)

Hapa kinaya kinajitokeza pale Kenga anamwita Sudi muungwana kwa kuwa Kenga alikuwa mshauri mkuu wa Majoka na Sudi alikuwa anashirikiana na mpinzani mkuu wa Majoka kwa jina Tunu. Msomaji anaelewa kuwa Kenga alikuwa anamkinaya Sudi kwa kuwa alikuwa amekataa kumchongea Majoka kinyago na hata Majoka alikuwa ametia mke wake mbaroni kwa jina Ashua ili kumshurutisha Sudi kumchongea kinyago.

Pia,tunaona Kenga akimrai Sudi kumchongea Majoka kinyago kwa kumwambia:

*"Malipo yake mazuri Sudi. Mradi huu utayabadilisha maisha yako. Jina lako litashamiri. Utapata tuzo nyingi pia. Kuna likizo ya mwezi mzima ughaibuni; wewe na familia yako. Ninavyokujua wewe kazi hiyo kwako ni mteremko. Na ni nani ajuaye watakapoiona kazi yako wageni wetu pengine…*" (u.k 12).

Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale ambapo msomaji anaelewa vyema kuwa Kenga alikuwa anamdanganya Sudi kwa kuwa Majoka hangetimiza ahadi hizo zote kwa kuwa alikuwa anataka tu sudi amchongee kinyago.

Mfano mwingine unajitokeza wakati Kenga anampatia Boza keki. Boza anaipokea akichekacheka na kusema:

*"Keki, keki ya taifa. Imeokwa na mke wangu mwenyewe! Karibuni"* (u.k 13)

Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale tunaona kwamba hiyo keki Kenga alikuwa akisherehekea sio keki ya uhuru bali ilikuwa hongo ambayo Kenga alikuwa amewaletea ili Sudi akubali kumchongea Majoka kinyago.

Mfano mwingine, ni pale ambapo tunaona kuwa wakati Tunu anaambia raia wenzake kuwa mzee Kenga anapanga njama fulani chini ya mbuyu na kwamba wanafaa kutoroka, Boza anasema:

"*Haya yanatuhusu vipi?"* (u.k 15)

Hapa hatungetarajia Boza aulize swali hili kwa kuwa Kenga alikuwa anapanga njama ya kuwaangamiza wapinzani wote wa Majoka. Kwa mfano tunaona kwamba Tunu analemazwa na Ngurumo mfupa wa muundi. Kinaya cha drama kinajitokeza pale Boza alikuwa anajifanya kuwa upande wa Tunu lakini tunaona akigeuka na kuunga mkono kiongozi Majoka.

Tena tunaona kuwa wakati baadhi ya Wanasagamoyo wanatetea haki zao kuna wale wanaona ni kama utoto. Kwa mfano, wakati siti analalamikia kuhusu bei ya chakula kwenye kioski cha kampuni vile imepanda maradufu tangu soko lilipofungwa Boza anamjibu kuwa huo ni utoto anaongea. Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale msomaji anatarajia Boza kuunga mkono malalamishi ya Boza lakini yeye anasema kuwa huo ni utoto. (u.k 17)

Mfano mwingine ni pale tunaona kuwa Ashua anapoenda kwa Majoka kuomba msaada wa chakula, Majoka anasema:

*"Enhe! Ni kukumbuka asali na kufuata nhuki, sio? Tangu hapo nikikuambia kwa Majoka kwakupendeza!* (u.k 19)

Hapa Majoka anamrai Ashua kujihusisha naye kimapenzi ili amsaidie na chakula cha kupelekea watoto wake. Hapa kinaya kinajitokeza pale ambapo Majoka anasema kwamba Ashua anampenda lakini msomaji anaelewa kuwa hapakuwa na uhusiano

wowote wa kimapenzi kati ya Majoka na Ashua. Wakati Majoka anamwambia Ashua awe na uhusiano wa kimapenzi naye, Ashua anakataa na kumwambia kuwa hawezi kuisaliti ndoa yake na Sudi na tunaona kuwa Majoka alikataa kumsaidia na msaada wa chakula.(u.k20)

Mfano mwingine unajitokeza pale ambapo baada ya Ashua kumuuliza swali kama anaweza kumuoa anamjibu:

*"Naweza Ashua. Naweza kila kitu. Niangalie, niambie, ni nini nisicho nacho mimi katika milki yangu isipokuwa wewe tu?"* (u.k 20)

Hapa kinaya kinajitokeza pale ambapo Majoka anamwambia Ashua kuwa anaweza kumuoa lakini msomaji anaelewa kuwa Majoka alikuwa na mke anayeitwa Husda na ana mtoto anayeitwa Ngao Junior na hivyo basi alikuwa anadanganya tu.

Mfano mwingine ni pale tunanaona kuwa Wazee hawataki kuambiwa kuwa wamezeeka. Katika tamthilia ya *Kigogo* tunamwona Majoka akikasirika anapoitwa na Ashua mzee anasema:

*"Mzee ni nani hapa? Nimekukanya mara ngapi usiniite mzee? Eeh? Nakuuliza. Mara ngapi ? Usizoee kubembea kwa kamba ambayo yaelekea kukatika Ashua. Subira yangu imeanza kufunganya virago sasa*!" (u.k 20)

Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale amababpo Majoka hapendi kuitwa mzee ilhali yeye ni mzee.

Pia tunawapata viongozi wakisema kuwa haja za wananchi ni haja zao. Mfano ni pale tunampata Majoka akimwambia Ashua kuwa haja zake Ashua ni zake. Yeye anasema:

“Usijali Ashua. Haja zako ni haja zangu, shida zako ni shida zangu, na kiu yangu ni kiu yako,” (u.k 23)

Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale tunamwona Majoka akimhadaa Ashua kuwa haja zake ni zake kwa kuwa wakati Ashua anaenda kwake ofisini kumwomba msaada wa chakula msomaji anaelewa fika kuwa yeye alikataa kumsaidia na chakula.anakataa kumsaidia.

Tena wakati Ashua alikataa kujihusisha kimapenzi na Majoka na kumwambia kuwa hawezi kwa kuwa alikuwa ameolewa na mume mmoja aliyekuwa anaitwa Sudi, yeye Majoka alimwambia kuwa hataacha kuwa na uhusiano na wanawake wengine hata kama ameoa na ana mke ambaye anaitwa Anaitwa Husda.

Mfano mwingine ni pale tunaona kwamba wakati viongozi wanafunga soko pale ambapo maskini huwa wanafanyia biashara zao. Kwa mfano Majoka anafunga soko la Chapakazi pale ambapo akina Ashua wale ambao hawana kazi walikuwa wanafanyia biashara zao. Alifunga soko hili ili ajijengee hoteli ya kifahari. Anapoombwa na Ashua alifungue soko hili, yeye anasema:

“*Ha-ha-ha-ha…Soko halifunguliwi ng’o! Limefungwa milele.” (u*.k 25)

Hapa msomaji anaelewa kuwa kicheko cha Majoka hakikuwa cha wema bali alikuwa anawachekelea Wanasagamoyo maskini ambao walikuwa wafanyabiashara kwa kuwa alikuwa amewafungia soko lao.

Pia, tunaona viongozi ambao wanakosa kushughulikia malalamishi ya raia wao. Kwa mfano katika tamthilia ya *Kigogo* tunaona kiongozi kwa jina Majoka akiyapuuza malalamishi ya Wanasagamoyo. Anamwambia Ashua:

*"Kuna miradi ya hadhi ya kushughulikiwa kuliko hivyo visoko vya kichochole. Najenga hoteli ya kifahari hapo."* (u.k 25)

Hapa msomji anaelewa kuwa Majoka hakuwa na miradi mingine bali alikuwa anawapuuza Wanasagamoyo ambao alikuwa amewaahidi ahadi nyingi hata za kuwatatulia matatizo yao lakini tunaona kwamba anaendelea kuwanyanyasa.

Mfano mwingine ni pale tunaona wanawake wanawasingizia wanawake wengine kuwa wana uhusiano wa kimapnzi na wanaume wao mpaka wanataka kuwaangamiza. Mfano mmoja unajitokeza pale ambapo Husda anamwambia Ashua kuwa atamwangamiza kwa kuwa ana uhusiano wa kimapenzi na Majoka ambaye alikuwa mumewe. Husda anasema:

*"Leo nitaua mtu mie. Nitakumaliza Ashua. Majoka haonekani kwake, kisa na maana ni wewe! Huwezi kunitoa tonge kinywani hivi hivi. Umenizidi nini kwani?* (u.k 27)

Hapa msomaji anaelewa kuwa hayo maneno ya Husda hayakuwa ya ukweli kwa kuwa Ashua hakuwa na uhusiano wowote wa kimapenzi na Majoka bali kulikuwa tu na umbeya baina ya wanawake ambao walikuwa wanamsingizia Ashua kuwa alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Majoka bila ukweli wowote.

Mfano mwingine ni pale tunaona kuwa Husda anmwambia Majoka kwamba:

*"Basi yaishe lakini mwambie huyu kimada wako akome udhabidhabina. Mwangalie! Kazi ni kuchana vichochoro kuwinda waume wa watu. Wangu humpati, utamaliza…*" (u.k 27)

Hapa kinnaya cha drama kinajitokeza pale tunamwona Husda akimwambia Majoka kwamba Ashua ni kimada wake lan[kini msomaji anaelewa kuwa Ashua hakuwa na uhusiano wowote na Majoka bali alikuwa anaenda ofisini mwake kumwomba msaada kwa kuwa alikuwa maskini hohe hahe.

Tena tunamwona Ashua akimwambia Majoka kuwa mambo yake na Husda huwa hawataki yajulikane na watu wengine lakini mambo yake Ashua wanayasambaza kila mahali. Ashua anasema:

*"Si wayasikia hayo? Ya wenziwe hadharani, yake faraghani. Nani asiyemjua mkeo huyu mdaku, Msambazaji wa kanda za umbeya kwenye vikao vya masengenyo?"*

Hapa kinaya kinajitokeza pale ambapo msomaji anagundua kuwa Husda ndiye alikuwa mdaku na alikuwa anaeneza uongo kuwa Ashua alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Majoka jambo ambalo lilikuwa la uongo.

Mfano mwingine ni pale tunaona kwamba washauri wa viongozi wanawashauri vibaya. Kwa mfano, katika tamthilia ya Kigogo tunampata Kenga ambaye anamshauri vibaya Majoka. Yeye anamwambia:

*"Kubali pendekezo letu la kufungwa kwa soko… huoni kuwa hii ni fursa nzuri ya kulipiza kisasi kwa huyo Sudi kumnasa Ashua? Najua umekuwa ukimmezea mate…akija ofisini mwako, mtumie mkeo ujumbe aje ofisini… bila shaka, kutatokea patashika na papo hapo, amuru askari wamtie Ashua nguvuni kwa madai ya kuzua vurugu katika ofisi ya serikali.*" (u.k 29)

Hapa ni dhahiri kuwa Kenga alikuwa akimshauri vibaya majoka. Anamshauri Majoka kulifunga soko la Chapakazi ili Ashua afungwe na ili aachiliwe huru lazima mumewe

Sudi akubali kumchongea Majoka kinyago. Hapa msomaji anaelewa fika kuwa hatungetarajia Majoka kufuata ushauri mbaya na tunaona kwamba alimpeleka Ashua jela bila makosa yoyote.

Tea, tunaona viongozi wakitia raia jela bila makosa yoyote. Kwa mfano tunaona Majoka akiwafumanisha Husdaa na Ashua ofisini mwake na tunaona kuwa wanaanza kupigana. Baadaye anawaita Mwango na Chopin a kusema:

*"Wachukueni hawa wawili mwafungie ndani. Msiwachanganye na washukiwa wengine*." (u.k 29)

Hiki ni kinaya kwa kuwa msomaji anaelewa fika kuwa Ashua hakuwa na makosa yoyote na hatungetarajia kuwa aambiwe afungwe jela na Majoka bila hatia yoyote. Baadaye tunaona kuwa Majoka anaagiza mkewe Husda atolewe jela lakini Ashua aendelee kukaa ndani. Msomaji anaelewa kuwa Ashua anabaki ndani na hakuwa na makosa bali Husda ndiye anafaa kubaki kwa jela kwa kuwa ndiye alianzia kumchapa Ashua bila makosa yoyote.

Mfano mwingine unajitokeza pale tunaona pale Majoka anasema:

*"Nitanfundisha Tunu mambo ambayo hakufundishwa nyumbani na mamake wala chuoni na maprofesa wake. Hivi vishahada vyao wanavyovipata siku hizi vinawavimbisha vichwa! Mtu anaitwa daktari na hata kazi ya maana haya."* (u.k 32)

Wakati Majoka anasema kuwa atamfundisha Tunu msomaji anaelewa kuwa Majoka hakuwa anamfundisha Tunu mambo ya siasa lakini alikuwa anapanga njama ya kumwangamiza kwa kuwa alikuwa mpinzani wake.

Tena tunaona Majoka akisema kuwa atawafurusha wafadhili wa Tunu kwa kuwa Sagamoyo wanajiweza. (u.k 33)

Msomaji anaelewa fika kuwa Sagamoyo hawajiwezi kwa kuwa Majoka anaendelea kukopa madeni kutoka wafadhili kutoka nchi zingine na hivyo basi alikuwa na wivu kwa Tunu kwa kuwa alikuwa mpinzani wake na alikuwa amemshinda kwa kura cha uchaguzi kulingana na maoni ya Wanasagamoyo.

Pia tunaona kuwa viongozi wanawaangamiza wapinzani wao. Mfano katika tamthilia hii ya *Kigogo* tunaona kuwa Majoka ambaye ni kiongozi wa Sagamoyo na Kenga ambaye alikuwa mshauri wake wanamwangamiza Jabali ambaye alikuwa mpinzani wa Majoka. Katika mazungumzo ya Majoka na Kenga, Majoka anasema:

*"Ha-ha-ha-ha… Wamesahau vipi wasilolijua? Wewe Kenga ni hatari. Hata hicho chama chake cha Mwenge kilimfuata huko akhera*." (u.k 35).

Hapa tunaona kinaya cha drama pale ambapo tunaona kwamba anacheka kwa kuwa Jabali mpinzani wake ameaga dunia na msomaji anaelewa fika kwamba Majoka kama kiongozi hakufaa kuwaangamiza watu ilhali anafaa kuwahahakishia usalama.

Mfano mwingine ni pale Majoka anamwambia Kenga:

*"Hivyo vipembe vyao niwachie mimi profesa wa siasa. Michezo ya kitoto huchezwa kitoto. Hatutatumia bomu kuulia mbu. Hawa ni watu wadogo. Usiichoshe akili bure. Dawa yao ninayo".* (u.k 35)

Hapa tunaona kuwa Majoka anajiita profesa wa siasa lakini msomaji anaelewa kuwa Majoka si profesa wa siasa kwa kuwa alishindwa na mpinzani wake Tunu katika uchaguzi wa jimbo la Sagamoyo.

Tena tunaona kuwa Majoka anamwambia Kenga:

*"Sudi. Sudi hatanikosesha usingizi, laiti angalijua salamu zinazomsubiri hapa! Na hii Runinga ya Mzalendo nayo haina maisha Sagamoyo. Kitabakia kituo kimoja tu!"* (u.k 37)

Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale Majoka anasema ya kwamba Sudi hajui zile salamu zinamngojea. Hapa Majoka anamaanisha kwamba atamwangamiza Sudi na hapa msomsji anaelewa kuwa Majoka hamaanishi kuwa Sudi atasalimiwa bali anamaanisha kuwa Sudi ataangamizwa.

Isioshe tunaona kinaya cha drama wakati tunaona viongozi wakiwaogopa wananchi wanaowatawala. Mfano, wakati Tunu na Sudi wanaenda kwa Majoka kumwelezea malalamishi yao, Majoka anaogopa na kumrai Mwango ambaye alikuwa askari katika makazi yake akae naye kwa kuwa hangependa Tunu na Sudi wamdhuru (u.k 38) Kinaya cha drama kinajitokeza pale msomaji anagundua kuwa Majoka alikuwa anawaoggopa wapinzani wake yaani Tunu na Sudi ndiposa anamwambia Mwango akae naye katika ofisi yake.

Pia tunaona kuwa wakati Tunu na Sudi wanaingia ofisini mwa Majoka, yeye anasema:

*"Karibuni waungwana; viongozi wa usoni wa Sagamoyo…*" (u.k 39)

Kinaya cha drama kinajitokeza pale Majoka anawaita Sudi na Tunu waungwana. Hii ni kwa sababu Majoka alikuwa amepanga njama ya kumwangamiza Tunu na tunaona Tunu akivunjwa mfupa wa muundi naye Sudi mke wake anayeitwa Ashua akafungwa jela ili yeye akubali kumchongea Majoka kinyago.

Tena, Majoka anamwambia Tunu:

*"Mimi na marehemu babako…wajua tulikuwa kama ndugu wa toka nitoke japo hatuna uhusiano wa damu."* (u.k 39)

Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale ambapo msomaji anaelewa ya kwamba baba yake Tunu hakuwa na urafiki na Majoka kwa sababu alikufa katika kampuni ya Majoka kutokana na mazingira duni na anapoaga dunia familia yake haikupewa fidia yoyote na jambo hili likamfanya Tunu kusomea uanasheria ili atetee marehemu baba yake.

Mfano mwingine ni pale tunaona kuwa viongozi huwa wanawaahidi wapinzani wao kuwa watawaoza kwa watoto wao ili waachane na siasa ili hao viongozi waweze kushinda kwa uchaguzi. Katika tamthilia hii ya *Kigogo* tunaona Majoka akimwahidi Tunu ambaye alikuwa mpinzani wake aachane na siasa na anamshawishi kuwa aolewe na mtoto wake anayeitwa Ngao Junior kwamba atapata nafaka akiolewa naye. (u.k 42). Wakati Tunu anakataa kuolewa na Ngao Junior na anaendelea kupigania haki Za Wanasagamoyo, tunaona ya kwamba Tunu anamshinda Majoka kwenye uchaguzi uliofanyika katika jimbo la Sagamoyo. Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale ambapo tunaona kuwa Majoka anamwahidi Tunu aolewe na Ngao Junior ili asipate fanaka ya kuwa kiongozi wa Sagamoyo. Pia Majoka hakuwa anataka Tunu aolewe na Ngao Junior kwa kuwa alikuwa amempangia njama ya kuuawa na vibarakala wake.

Isitoshe tunaona wakati Tunu na Majoka walikuwa wanazungumzia kuhusu kifo cha babake Tunu, Majoka anamuuliza kuwa kama ameenda kumfunza kuhusu sheria. Hiki ni kinaya cha drama kwa kuwa Tunu hakuwa ameenda kumfunza Majoka kuhusu sheria bali alikuwa anamwambia vile baba yake alifilia kwenye Kampuni ya Majoka na akakosa familia yake ikakos kupewa fidia yoyote kutokana na kifo chake. (u.k 44)

Pia tunaona Majoka akisema kuwa hata kama Wanasagamoyo hawataki yeye ajenge hoteli katika soko la Chapakazi atejenga. (u.k 45) Kinaya cha drama kinajitokeza pale ambapo Majoka analifunga soko la Chapakazi na kubomoa vioski vilivyokuwa kwenye soko hili na kusema kuwa atajenga hoteli la kifahari . Alikuwa anafikiria kuwa soko hili litamfaa sana lakini tunaona Wanasagamoyo wakipigania hski zao na kumzuia Majoka kujenga soko hili.

Mfano mwingine ni pale tunampata Sudi alipomtembelea Ashua katika jela, Ashua anamwambia:

" *Nimechoshwa na wewe Sudi. Afadhali hapa pana amani. Nikiwa hapa sikutani nawe na huyo kirukanjia wako. Si umwoe yaishe!*" (u.k 447)

Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale ambapo Ashua anasema heri akiwa katika jelea kuliko kuwa nyumbani na Sudi. Katika jela hii tunaona kuwa Ashua alikuwa anachapwa na polisi vibaya kiasi cha kutoka damu kwa mwili. Hivyo basi hatungetarajia yeye aseme kuwa heri akiwa hapo mahali ambapo alikuwa anadhulumiwa vibaya. Tena anamwambia Sudi kuwa ana uhusiano wa kimapenzi na Tunu jambo ambalo si la ukweli kwa kuwa Sudi na Tunu walikuwa tu wanazipigania haki za Wanasagamoyo na hawakuwa na uhusiano wowote wa kimapenzi.

Tena tunaona ya kwamba Sudi alikuwa amemwahidi Ashua ahadi nyingi ambazo hakuzitimiza. Wakati yeye alimtembelea katika jela Ashua anasema:

(*…Uliniahidi mengi siku hizo, kumbe nilihadaika.”* (u.k 49)

Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale ambapo msomaji anaelewa kuwa Sudi alikuwa amemdanganya Ashua ili akubali kuolewa naye kwa kuwa sasa tunaona kuwa Ashua anakosa hata chakula na watoto wake wanalala njaa. Anapoenda kumwomba Majoka msaada wa chakula yeye anamrai kuwa wajihusishe kimapenzi ili aweze kumsaidia. Wakati Ashua anakataa, Majoka anamfumanisha Ashua na mkewe Husda. Ashua wanapigana na Husda na Majoka anawaitia polisi pale ambapo Ashua anatiwa jela na mkewe Majoka anaachiliwa huru.

Mfano mwingine ni pale viongozi wanawashurutisha wenyeji wa Sagamoyo kuwa wahame Sagamoyo mahali ambapo wameishi kwa miaka mingi. Siti anamwabia mama yake Bi. Hashima kuwa wamepewa vijikaratasi vya kuwaambia wahame Sagamoyo kwa kuwa si kwao. (u.k 52) Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale ambapo Siti na mama yake wameishi huko Sagamoyo kwa miaka mingi na Siti anasema kuwa alizaliwa hapo. Msomaji anaelewa kuwa wakati wanaambiwa kuwa huko si kwao huo ni uongo mtupu.

Tena tunamwona Bi. Hashima akisema kuwa hakunyeshi Sagamoyo kwa kuwa damu nyingi imemwagika Sagamoyo na arddhi kuingia najisi. (u.k 53). Huu si ukweli kwa kuwa msomaji anaelewa fika kuwa mito na maziwa yamekauka kwa kuwa Majoka amefungulia biashara ya ukataji wa miti na kusiponyesha tunaona kuwa maji yanaagizwa kutoka ng’ambo.

Isitoshe tunaona ya kwamba Tunu anaamini kuwa mumewe Sudi na Ashua ndio waliompangia njama ya kuvunjwa mfupa wa muundi. Kinaya cha drama kinajitokeza pale ambapo tunaona kuwa Ngurumo ndiye alimvunja Tunu mfupa wa muundi kama alivyokuwa ameagizwa na Majoka kwa kuwa Tunu ndiye alikuwa anapendekezwa na Wanasagamoyo kuwa kiongozi wao.

Mfano mwingine ni pale tunaona Ngurumo akiwa kwa mamapima akiwaona Tunu na Sudi anawaita wageni mahashumu. Pia anamtafutia Tunu kiti na kuwaambia walevi wale wengine kuwa walisoma na Tunu katika darasa moja. (u.k 57) Kinaya cha drama kinajitokeza pale tunapata kuwa Ngurumo ndiye alikuwa amemvunja Tunu mfupa wa muundi na sasa anaonekana akimkaribisha vizuri jambo ambalo hatungetarajia amfanyie hivyo.

Tena tunaona kuwa Ngurumo anamwambia Mamapima kuwa amemletea wateja wa nguvu yaani Tunu na Sudi. (u.k 57). Kinaya cha drama kinajitokeza pale tunaona kwamba Sudi na Tunu hawakuwa wameenda kwa Mamapima kulewa bali alikuwa ameenda huko kuwakomboa walevi kama vile Ngurumo kutokana na pombe haramu iliyokuwa inauzwa na Mamapima. Hii ni kwa kuwa pombe hii haramu ilikuwa imewafanya vijana wengi kupoteza uhai wao na wengine kuwa vipofu.

Pia, tunamwona Ngurumo akimwambia Mamapima:

*"Ongeza ya tatu Mamapima, sherehe za uhuru zimepamba moto!"* (u.k 58)

Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale tunaona Ngurumo akisema kuwa anasherehekea uhuru ilhali tunaona kuwa katika Sagamoyo hapakuwa na uhuru wowote kwa kuwa watu

waliuawa kiholela na  pia watu wananyimwa haki za kufanya biashara wakati soko lao la Chapakazi lilifungwa na Majoka ili ajijengee hoteli ya kifahari.

Pia tunaona Ngurumo akiwaambia Tunu na Sudi kuwa wasiwaharibie starehe zao kwa hotuba zao za kihistoria na kuwa wakati alikuwa anasoma hakulipenda somo hilo kwa kuwa mwalimu wao wa Historia alikuwa mbaya sana. (u.k 59). Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale tunaona Ngurumo akisema kuwa yeye na walevi wengine walikuwa wanasherehekea starehe zao za kulewa. Ile pombe walikuwa wakibugia ilikuwa haramu kwa kuwa iliwapofusha vijana wengi na wengine wakaaga dunia.

Isitoshe tunaona kwamba Mamapima anawaambia Tunu na Sudi kuwa kwake ni yaha na maraha na kwamba yeye na walevi wengine wanasherehekea uhuru na kwamba kwake watu hupata furaha.(u.k 60). Hiki ni kinaya cha drama kwa kuwa Kwake Mamapima kulisababisha watu wengi kupoteza jamaa zao kwa kuwa alikuwa anauza pombe haramu. Wengine pia walipofuka na kupoteza uwezo wao wa kuona hivyo basi hatungetarajia Mamapima kusema kuwa kwake ni raha na maraha.

Mfano mwingine unajitokeza pale tunaona kwamba Mamapima anasema kuwa amepewa ruhusa ya kuuza pombe haramu kutoka kwa Majoka. (u.k 61) Hiki ni kinaya cha drama kwa kuwa hatungetarajia serikali ya Majoka mbaye alikuwa anawaahidi Wanasagamoyo hali ya usalama kuwa mstari wa kwanza kumpatia Mamapima kibali cha kuuza pombe haramu. Pombe hii haramu imesababisha watu wengi kuaga dunia na wengine kupofuka.

Pia inajitokeza kuwa Mamapima alikuwa amepewa mradi wa kuoka keki kwa Majoka kwa sababu alijihusisha kimapenzi na Ngurumo ambaye alikuwa kibarakala wa Majoka na hivyo basi akazungumza na Majoka ili Mamapima apewe mradi huo. Maneno haya yalisemwa na Boza kwa Ngurumo kama ifuatavyo:

*"Kwamba Asiya aliupata mradi wa keki kwa kukupa uroda*." (u.k 64)

Tena tunaona kwamba Majoka anaanzisha ujenzi wa hoteli ya kifahari katika soko la Chapakazi baada ya kuwazuia wafanya biashara katika soko hilo. Kenga anamwambia Majoka:

*"Taka zote zimeondolewa. Kazi ya kung'oa vibanda nayo ishakamilika. Vifaa vya ujenzi na malighafi yameanza kuwasili kutoka bandarini. Watu wa Tunu walifukuzwa jana asubuhi walipojaribu kukaribia. Ulinzi ni mkali*." (u.k 69)

Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale ambapo tunaona ya kwamba Majoka anawabomolea Wanasagamoyo vibanda vyao pale ambapo walikuwa wanaendeshea biashara zao jambo ambalo hatungetarajia yeye afanye hivyo.

Tena, wakati Majoka anaarifiwa na Chopi kuwa Ngurumo amenyongwa na chatu akitoka mangweni yeye anajibu.

*"Kila mtu Sagamoyo hafanyi kazi yake- hata hao chatu! Kwa hivyo wataka niache raha zangu, nijishike kichwa nilie?"* (u.k 69)

Hapa kinaya kinajitokeza pale ambapo Ngurumo alikuwa kibarakala wa Majoka na tungetarajia kuwa Majoka angehuzunika kusikia kuwa Ngurumo amepoteza maisha yake lakini hata anasema hata azikwe juu ya wengine kwa kuwa maziara yalikuwa yamejaa.

Mfano mwingine ni pale ambapo tunapata kuwa wakati Majoka anakuwa kwa ambulensi, anamwita mkewe Husda nyanya yake na kumwambia kuwa Husda alikuwa anapenda mali yake Majoka bali si mapenzi ya dhati yalifanya yeye amkubali. Kinaya cha drama

kinajitokeza pale ambapo hatungetarajia Majoka kumwita mkewe nyanya yake. (u.k 87)

Isitoshe Majoka anapohudhuria mkutano wa Tunu na Wanasagamoyo anasema:

"*Watu wa Sagamoyo mu wajinga sana*!" (u.k 88)

Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale ambapo Majoka anawatusi Wanasagamoyo kuwa wao ni wajinga. Msomaji anaelewa kuwa Majoka anawatusi Wanasagamoyo wajinga kwa kuwa wanamuunga mkono Tunu na kama wangekuwa wanamuunga Majoka mkono yeye hangewatusi.

Mfano mwingine ni pale tuona kuwa Majoka alikuwa anasema kuwa Tunu hawezi kuzipigania haki za Wanasagamoyo kwa kuwa alikuwa amemlemaza. (u.k 89). Hapa kinaya cha drama kinajitokeza pale ambapo msomaji anatambua kuwa hata baada ya Tunu kulemazwa, bado yeye anaendelea kuzitetea haki za Wanasagmoyo na kuungwa mkono na karibu Wanasagamoyo wengi.

Tena Majoka anaamrisha mkuu wa polisi kwa jina Kingi awapige risasi wafuasi wa Tunu. (u.k 90) Kinaya cha drama kinajitokeza pale Kingi anakiuka amri za Majoka na kukataa kuwapiga risasi wafuasi wa Tunu. Tungetarajia kuwa Kingi afuate amri zake Majoka lakini anakataa

# SURA YA NNE

# KINAYA KATIKA KUBAINISHA MAUDHUI KATIKA RIWAYA YA *CHOZI LA HERI* NA TAMTHILIA YA *KIGOGO*

## 4.0 Utangulizi

Sura hii imeongozwa na mhimili wa nadharia ya kimtindo inayochunguza kinachosemwa ambacho ni maudhui na kinavyosemwa ambacho ni mtindo. Utafiti huu umeangazia vile kinaya kimetumika katika kubainisha maudhui mbalimbali katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo.* maudhui haya ni : Uongozi mbaya, ufisadi, ukatili na unafiki.

## 4.1 KINAYA KUENDELEZA MAUDHUI KATIKA RIWAYA YA *CHOZI LA HERI* NA TAMTHILIA YA *KIGOGO*

### 4.1.1 KINAYA KATIKA UFISADI KATIKA *CHOZI LA HERI*

Ufisadi ni dhana inayojumuisha wizi wa mali ya umma, upokeaji au utoaji wa hongo au matumizi mabaya ya madaraka kwa manufaa binafsi. Katika riwaya ya *Chozi la Heri*, kinaya kimetumika kuendeleza maudhui ya ufisadi kwa kudhihirisha vile wahusika waliendeleza ufisadi kinyume cha matarajio ya jamii kama ifuatavyo:

Mfano ni kwamba, hatungetarajia mabwanyenye kujinyakulia sehemu ambazo zimetengewa barabara na wengine kujijengea majumba yao chini ya vigingi vya nyaya za umeme. Katika mtaa wa Tononokeni,kuna watu waliojenga majumba yao katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya barabara na wengine wakajenga chini ya vigingi vya nyaya za umeme. Baada ya serikali kuwapa ilani ya kuondoa majumba yao, kuna baadhi ya mabwanyenye hawa walioonekana wakitoa milungula hadharani jambo ambalo ni

kinyume cha matarajio ya jamii (uk.13). Hapa hatungetarajia viongozi kuhongwa na hawa mabwanyenye na jambo hili linadhihirisha kinaya cha matarajio yetu kwani hatungetarajia viongozi kupokea hongo.

Hatungetarajia baadhi ya walinda usalama kushirikiana na wahalifu na kugawana mali iliyoibwa, na tena wanapokea hongo kutoka kwenye wananchi wenye magari makuukuu barabarani na kuwaruhusu waendeshe magari hayo. Katika riwaya ya *Chozi la Heri* kupitia hotuba ya Apondi tunaelewa fika kuwa polisi wanashirikiana na wahalifu na kugawana nao mali iliyoibwa na tena ni bayana kuwa walindausalama wanawaruhu wenye magari kuendesha magari makuu barabarani. Apondi anasema:

*"Wapo baadhi yetu ambao wizi unapotokea, inasemekana wanashirikiana na wahalifu wenyewe, na baadaye wanagawanya ngawira nao. Wengine wetu tumeyaacha magari makuukuu barabarani, kisa na maana, wenye magari haya ni miamba isiyogusika*." (uk.114)

Hapa kinaya kinajitokeza pale tunaona walinda usalama wakipokea hongo jambo ambalo ni kinyume na taaluma yao.

Mfano mwingine ni pale tunaona watendaji katika waizara ya ardhi wakiwauzia watu ardhi iliyokwisha uzwa. Katika riwaya hii, kuna ufisadi unaohusu wizara ya ardhi (uk.58). Mwandishi anaonyesha kuwa kuna baadhi ya watendaji katika wizara ambao hushiriki kuwauzia watu ardhi iliyokwisha uzwa na kuwapa hati bandia huku ile halali ikisalia mikononi mwa mnunuzi wa awali. Mwandishi anaendelea kusema kuwa kuna visa pia vya watu kuuziwa hata sehemu zilizokuwa maziara na walioangukia mtego huu, baada ya kuchora ramani zao, walipigwa na butwaa walipowapeleka wahandishi na

mafundi na kupata kuwa makaburi yamejikita kwenye viwanja vyao tena. Kinaya kinajitokeza hapa kwa kuwa hatungetarajia watu kuuziwa sehemu zilizokuwa maziara.

Hatungetarajia matajiri kunyakua mashamba madogo madogo ya wananchi maskini na wanapolalamika wanaambiwa kwamba, tume ya kuchunguza uyakuzi imeundwa lakini huwa hawazioni ripoti zitokanazo na kashfa hiyo. Mfano kutoka riwaya ya *Chozi la Heri* ni kwamba mashamba madogo madogo ya wananchi yaliponyakuliwa na mabwanyenye ambao walikuwa na maelfu na maelfu ya ekari ambapo walijenga viwanda na maduka ya biashara huku wengine wakilima mashamba makubwa makubwa wakidai kuwa ni njia ya kuhakikishia wenyeji wanajitosheleza kwa chakula. Wananchi wanapolalamika kuhusu kashfa hii ya unyakuzi, huambiwa kuwa tume ya kuchunguza unyakuzi imeundwa. Cha kushangaza ni kwamba wananchi hawazioni ripoti zitokanazo na kashfa hizo. Mja aliyevalia shati lililoandikwa Hitman kwa mgongo anasema:

"*Hapa ndipo unashangaa utarudi kwenye shamba lipi na tangu hapo familia yako uliiacha ikiishi kwa msaada wa wale wale waliotoka mbali kule walikotoka, wakapewa maelfu kwa maelfu ya ekari, wakajenga viwanda na maduka ya biashara, wengine wakalima mashamba makubwa makubwa huku wakidai kuwa njia ya kuwahakikishia wenjeji hali ya kujitosheleza kwa chakula. Kumbe wanakuja kutufukarisha zaidi. Tunapolalamikia kashfa za unyakuzi wa hata vikataa vidogo tulivyo navyo tunapozwa roho kwa "Tumeunda tume ya kuchunguza kashfa hii. Waliogawiwa au kununua mali ya umma kwa njia za udanganyifu watakabiliana na mkono thabiti wa sheria."(* Uk.22)

Tunaona kinaya pale tungetarajia wananchi wapewe ripoti za kashfa hiyo lakini hawapewi. Ni wazi kwamba mwananchi wa kawaida hadiriki kuziona ripoti za tume hizi au tuseme ripoti hizi huwa wageni wa rafu za makavazi ya kitaifa.

Isitoshe katika wizara ya elimu, watoto wa matajiri ndio wanapewa mikopo na ruzuku ya kusoma ilhali iliyokuwa imetengewa watoto wa maskini. Ufisadi huu unamwathiri mtoto wa mlalahoi kuliko wa mwenye nacho. Mwandishi anadai kuwa watoto wa matajiri ndio wanaopewa mikopo na ruzuku ya kusoma chuo kikuu ambayo ilikuwa imetengewa watoto maskini. Jambo hili linawalazimu wana wa maskini kufanya vibarua ili wajilipie karo na kugharamia mahitaji mengine. Meko anamwambia Selume:

"… *Nasikia kwamba wanaoishia kupewa mikopo au ruzuku hizi ni watoto kutoka familia zinazojiweza kiuchumi huku wana wa maskini wakilazimika kufanya vibarua wakati wa likizo kujilipia karo na kugharamia mahitaji mengine. Wengine huwa mawindo rahisi ya matajiri wanaotafuta roho za kulangulia na kusafirishia dawa za kulevya ughaibuni* .( u.k.142)

Hiki ni kinaya kwa kuwa tungetarajia mtoto wa maskini ndiye anapewa mikopo na ruzuku ya kusoma katika chuo kikuu lakini tunaona watoto hawa wakiteseka sana katika kusoma kwa.

Hatungetarajia wasimamizi katika hospitali za umma kuanzisha maduka ya kuuza dawa na kwa hayo maduka wanauza dawa zilizokuwa zimetengewa hospitali za umma na serikali. Ufisadi huu unamkera selume ambaye ni muuguzi katika hospitali hiyo kwani wagonjwa wanakosa huduma za msingi kwa sababu shehena za dawa zilizotengewa hospitali ya umma zinaishia kwa maduka ya dawa ya wasimamizi. Selume anasema:

“*Nimechoka kuwatazama wagonjwa wakifa kwa kukosa huduma za kimsingi huku shehena za dawa zilizotengewa hospitali hii zikiishia kwenye maduka ya dawa ya wasimamizi wa hospitali.”* (uk.140)

Hapa kinaya kinajitokeza pale hatungetarajia wasimamizi wawe na ubinafsi kwa kuuza dawa za hospitali kwenye maduka yao.

Mfano mwingie unajitokeza pale maofisa wa forodha wanakubali kupokea hongo kutoka kwa vinara wa biashara za dawa za kulevya. Katika riwaya ya *Chozi la Heri*, kuna wauzaji wa dawa za kulevya ambao wamekuwa wakitoa rushwa kulainisha maofisa wa forodha ili wawapitishe vijana wanaotumwa kusafirisha dawa hizo. Wauzaji hawa wanaendelea kuuza dawa hizi za kulevya kwa vijana ambao baadhi yao wanaaga dunia na wengine kuwa vipofu kutokana na kuathiriwa na dawa hizi za kulevya. Dick anawazia maneno haya:

“*…Je, isingekuwa mwajiri wako kuvilainisha viganja vya maofisa wa forodha, wewe na wenzako msingekuwa mmeozea kwenye magereza ya kitaifa na kimataifa kama wengine wengiwanavyofanya*.” (u.k 123)

Hiki ni kinaya kwa kuwa hatungetarajia wauzaji wa dawa za kulevya kuruhusiwa kuuza dawa hizo na maofisa wa forodha.

Tena tunawaona waajiri wakiwashurutisha wafanyakazi wao kujihusisha nao kimapenzi na wanapokataa wanasingiziwa maovu na mwishowe kufutwa kazi. Kwa mfano, tunapata Naomi ambaye alikuwa ameajiriwa na mwanamume kwa jina Kimbaumbau. Alipokataa kujihusisha naye kimapenzi, anasingiziwa kuwa yeye ni mwizi na pia wakati mwingine

kuchapwa. Baadaye anafutwa kazi baada ya kukataa kujihusisha naye kimapenzi. Mwandishi anasema:

"*Haukupita muda kabli ya kukumbana na bwana Kimbaumbau, shaibu mmoja tajiri ambaye alimwajiri Naomi kumwendeshea biashara yake ya nguo kuukuu. Hata hivyo, ilimbainikia Naomi kuwa Kimbaumbau alikuwa na nia nyingine tofauti. Naomi alipigana kwa jino na ukucha kuutetea utu wake… Hata Kimbaumbau alipoona kwamba Naomi kakataa katakata kuingia mtegoni, alimpiga kalamu*" (u.k 191)

Hapa tunaona kinaya kwa kuwa hatungetarajia Kimbaumbau kuwa mzinzi kwa waajiri wake.

Hatungetarajia mfanyakazi kufutwa kazi kwa kuwatetea wananchi dhidi ya kuuziwa mahindi ya njano ambayo yalikuwa hatari hata kwa usalama wa panya. Katika riwaya ya *Chozi la Heri*, tunapata kinaya kinachojitokeza pale Lunga Kiriri kangata anafutwa kazi baada ya kupinga kitendo cha wakuu wake kuwapa raia mahindi ya njano ambayo yalikuwa hatari hata kwa usalama wa panya. Mkurugenzi mkuu katika shirika la kuuza mahindi bwana Kalima katika barua yake kwa Lunga anasema:

"*Shirika hili linasikitika kukuarifu kuwa wewe ni mmoja wa walioathirika, na kwamba umeachishwa kazi kuanzia tarehe 31 Julai mwaka huu."* (u.k 62)

Mfano mwingine unajitokeza pale matajiri wananyakua ardhi ya maskini kama vile bwana Mabavu kutumia hati bandia kunyakua ardhi ya baba Shamsi na raia wengine. Akina Shamsi wanabaki wakiteseka mpaka baba yake anashindwa kumwelimisha baadaye baba yake Shamsi anaaga dunia aliposhindwa kugharamia matibabu yake katika

hospitali. Pia baada ya msitu wa Mamba kufungwa, kuna watu fisadi waliondelea kukata miti, kuchoma makaa na kuharibu mazingira Shamsi anasema:

*"Alipokuja Bwana Mabavu,*

*Shamba la asili akatwaa*

*Ati ni yake milki*

*Alonunua,*

*...Alipotuonyesha hatimiliki bandia*" (u.k131)

Hatungetarajia ajira za wale waliofuzu chuo kikuu kutolewa kwa upendeleo na ufisadi. Katika riwaya ya *Chozi la Heri* tunaona Shamsi akikosa kazi kwa sababu ya ubaguzi pale tunagundua kuwa wale wanapata ajira hawajahitimu kama bwana Shamsi (u.k 133). Hapa kinaya kinajitokeza pale ambapo tunaona kuwa katika nchi ya Wahafidhina, maskini kama Shamsi ambao wameenda hata vyuo vikuu wananyimwa nafasi za kazi na nafasi hizo zinapatiwa watu ambao hawajahitimu. Shamsi anaishia kutamauka na kuwa mlevi kupindukia na kupoteza matumaini katika maisha yake.

### 4.1.2 KINAYA KATIKA UFISADI KWA KIGOGO

Hatungetarajia viongozi kutumia vitisho kuwanyang'a wafanyabiashara mali zao. Katika tamthilia ya *Kigogo* wafanya biashara wananyang'anywa soko lao pale wanauzia bidhaa zao. Soko hili linanyakuliwa na Majoka na anajenga hoteli lake la kifahari na kusababisha maskini kama vile Ashua na Sudi kushindwa kugharamia mahitaji yao ya

kimsingi kama vile kuwalisha watoto wao. Sudi anasema:

"*Si haki kuchukua kilicho chetu na kututisha*" (U.k3)

Hapa kinaya kinajitokeza pale tunaona kwamba matajiri kama vile Majoka kunyang'anya watu mali yake.

Hatungetarajia waandamanaji kuuawa wanapotetea haki zao kwa kuwa tungetarajia viongozi kusikiliza vilio vyao na kuwahimiza hali njema ya maisha. Katika tamthilia ya *Kigogo*, tunapata vijana watano waliokuwa wakifanya maandamano ili kupinga kupanda kwa bei ya chakula katika kampuni ya Majoka wanauawa. Kinaya kinajitokeza pale ambapo Majoka ambaye ni kiongozi wa Sagamoyo anawaagiza polisi kuwaua vijana hawa jambo ambalo ni kinyume cha matarajio yetu. Siti anawaambia Sudi na Tunu:

"*Vijana watano wachuuzi sokoni waliokuwa wakiandamana pia wameumia"*(u.k 16)

Hapa kinaya kinajitokeza pale hatungetarajia wauawe kwa kuwa tungetarajia serikali ya Majoka isikilize malalamishi yao.

Tena, tunawaona wapinzani wanaopinga utawala wa serikali baadhi yao kuuawa na wengine kulemazwa. Katika tamthilia ya *Kigogo* viongozi wa upinzani wanaopinga utawala wa kiimla wa Majoka wanalemazwa kisiasa na hata kuuawa.Viongozi wanatumia mbinu za kisiri kuwaua washindani ili kuficha ukatili wao. Kwa mfano, Jabali, kiongozi wa upinzani ambaye alikuwa na chama chake cha Mwenge kuuawa na Majoka na chama chake kusambaratishwa na Majoka. Naye Tunu mpinzani mkuu wa Majoka analemazwa kwa kuvunjwa mfupa wa muundi. Majoka anamwambia Kenga:

"*Wewe Kenga ni hatari.Hata hicho chama chake cha Mwenge kilimfuata huko akhera*". (u.k 35) Mfano mwingine ni pale tunagundua watu wakivamiwa mara kwa mara na kuishi kwa hofu. Katika tamthilia ya *Kigogo* watu wanaishi kwa hofu kutokana na uvamizi wa mara kwa mara. Kwa mfano, Hashima na Siti hawana utulivu kwa sababu ya hali mbaya ya usalama jimboni. Pia watu wanyonge ambao hawana hatia, kupigwa na kutiwa mbaroni hasa wanawake ambao wanakataa kujihusisha kimwili na viongozi. Kwa mfano Ashua, licha ya kwamba ananyonyesha na wanawe kulala njaa, anatiwa mbaroni na kupigwa bila kosa. Pia ni kinaya Tunu kuvamiwa na wahuni wanaomjeruhi muundi wa mguu. Nia ya wavamizi ilikuwa kumuua kwa vile Kenga anamwambia Majoka:

"*Tunu bado yuko. Hawakumvunja mguuwakitamathali"* (u.k 68)

Ni kinaya kwa kuwa Maelezo haya yanaonyesha ukatili wa viongozi kwa sababu wahuni waliomvamia walitumwa na viongozi wenyewe.

### 4.1.3 KINAYA KATIKA UONGOZI MBAYA

Uongozi mbaya ni maudhui yanayodhihirisha vile viongozi wanakosa uwajibikaji katika nyadhifa zao. Kinaya kinajitokeza uongozi mbaya pale ambapo viongozi wanakosa kuwajibikia raia wao waliowachagua kwa kukosa kutimiza ahadi walizowaahidia wakati wa kampeni kinyume na matarajio yao kama ifuatavyo:

### 4.1.4 KINAYA KATIKA UONGOZI MBAYA KWA CHOZI LA HERI

Hatungetarajia kiongozi kutumia wafuasi wake kuwavamia watu na kuwatendea uhalifu. Katika riwaya ya *Chozi la Heri* kiongozi mwanamume kwa jina Mwanzi anayewania kiti cha uongozi na kushindana na mwanamke Mwekevu, kutumia nafasi yake vibaya. Kupitia kwa wafuasi wake, watu wanachomewa nyumba na magari. Wengine wanahama

na kuwa wakimbizi katika msituwa Mamba. Pia wasichana wa Kaizari ambao ni Lime na Mwanaheri wanabakwa na vijana mabarobaro watano kutokana na ghasia za baada ya uchaguzi. (u.k28).

Pia watoto wa maskini wananyimwa mikopo ya kuwasaidia kusoma wakiwa chuo kikuu. Katika riwaya ya *Chozi la Heri* halmashauri ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wa chuo kikuu, hutumia mamlaka yake kuwabagua wanafunzi wa maskini na kutoa mikopo kwa wanafunzi wa walio na mali. Hiki ni kinaya kwa kuwa tungetarajia viongozi kuwasaidia watoto kutoka familia za maskini. Meko anamwambia Selume:

*"Nasikia wanalewa kujipurukusha nahali duni ya maisha vyuoni. Wanasema kuwa gharama ya masomo imekuwa ghali, nayo halmashauri ya elimu inayotoa mikopo ya masomo haimudu kutosheleza mahitaji ya idadi kubwa ya wanafunzi wanaohitaji mikopo na ruzuku. Isitoshe, nasikia kwamba wanaoishia kupewa mikopo au ruzuku ni watoto kutoka familia zinazojiweza kiuchumi huku wana wa maskini wakilazimika kufanya vibarua wakati wa likizo kujilipia karo na kugharamia mahitaji mengine. Wengine huwa mawindo rahisi ya matajiri wanaotafuta roho za kulangulia na kusafirishia dawa za kulevya ughaibuni*." (u.k142)

Pia hatungtarajia mfanyikazi mwaminifu kufutwa kazi bila makosa yoyote. Mfano katika riwaya ya *Chozi la Heri* afisa mtendaji katika shirika la maghala ya Fanaka anatumia mamlaka yake vibaya kwa kumfuta kazi Lunga Kiriri kwa kupinga uuzaji wa mahindi ya sumu yaliyokuwa yametoka ughaibuni. Lunga alikuwa anapinga kuwa wananchi wasiuziwe mahindi ambayo yanaweza kuathiri afya zao na akafutwa kazi na bwana Kalima jambo ambalo ni kinyume cha matarajio yetu. Katika barua ambayo alimwandikia Lunga, Afisa mkuu mtendaji anamwambia:

*"Shirika hili linasikitika kukuarifu kuwa wewe ni mmoja wa walioathirika na kwamba umeachishwa kazi kuanzia tarehe 31 Julai mwaka huu"* (u.k 72)

Mfano mwingine ni pale serikali inaharibu misitu baada ya kuwakataza wananchi na kuwafukuza kutoka msitu wa Mamba. Mfano ni pale serikali inatumia mamlaka yake vibaya kwa kuwatoa wakimbizi wa baada ya vita vya uchaguzi katika msitu wa Mamba na baadaye, matrekta yanasikika yakibeba mahindi yaliyoachwa na wakimbizi na yanabeba mbao. Hiki ni kinaya kwa kuwa hatungetarajia serikali a miti na kuvuna mahindi yaliyoachwa na wakimbizi badala ya kuwasaidia wakimbizi.

Isitoshe wasimamizi wa hospitali za umma wanaiba dawa kutoka hospitali na kuziuza katika maduka yao. Katika riwaya ya *Chozi la Heri*, wasimamizi wa kituo cha afya cha serikali Selume anakofanyia kazi wanachukua dawa zilizotengewa kituo hiki na kuzipeleka katika maduka yao. Tendo hili linawafanya wengi kuangamia na kupoteza maisha yao katika mchakato wa kutibiwa. Hiki ni kinaya kwa kuwa (u.k 77)

Mfano mwingine ni pale tunaona kuwa walinda usalama wanakubalia wauzaji wa dawa za kulevya kuendelea na biashara hiyo haramu. Kwa mfano ni kinaya kwa polisi katika uwanja wa ndege kuruhusu dawa za kulevya kuingia na kutoka ili wakubali dawa hizo zipite baada ya kukaguliwa. Hiki ni kinaya kwa kuwa tungetarajia walinda usalama wapinge biashara hii haramu ya uuzaji wa dawa za kulevya lakini wanaikubalisha.

Tena nchi haijaendelea kutokana na uongozi mbaya na inaendelea kutegemea nchi zingine. Mfano katika riwaya ya *Chozi la Heri* ni pale tunaona kuwa baada ya miaka hamsini ya maendeleo, nchi bado haikuwa inajitegemea. Jambo hili linajitokeza pale ambapo pana mazungumzo kati ya Tila na babake pale Tila anasema:

"*…Wageni ndio wanaamua wakuze nini katika ardhi yetu. Tunabaki kuwategemea, si kwa lishe tu, bali pia kwa ajira."* (u.k 5)

Hapa kinaya kinajitokeza pale tungetarajia nchi ambayo ilipata uhuru miaka hamsini iliyopita bado ikitegemea nchi zingine kwa maendeleo yake. Pia tunaona viongozi wanaendeleza ukiukaji wa haki za kibinadamu. Kwa mfano, tunapata waandamanaji waliofunga barabara na kukataa kubanduka wakipigwa risasi na kuuawa. Hapa kinaya kinajitokeza pale ambapo hatungetarajia polisi kuwaua waandamanaji (u.k 14).

Pia, hatungetarajia wanasiasa kutumia vijana katika kuwahadaa wapiga kura wakongwe wakati wa uchaguzi. Kwa mfano viongozi wanaendeleza ufisadi na udanganyifu katika vituo vya kupigia kura. Wanatumia vijana kudanganya wakongwe na kuwawekeza alama potofu ambavyo hawakupenda. Hitman anasema:

"*…Mama unataka KIBOKO au PAPA?". "Mimi simtaki huyo Kiboko nataka Papa."Kiboko hata chumvi hatoi. Afadhali Papa, amepita hapa mara tatu akatugawia kila mtu shilngi mia mia na vibaba viwili viwili vya unga. Mama anajibu. "Basi tia alama X kwenye picha ya Kiboko kuonyesha humtaki kabisa". Anaambiwa kisha kusaidiwa kutia alama hiyo bila kujua kuwa kumchagua huyo huyo Kiboko." Sasa miaka kumi hii, tungali tunabisha hodi kwenye afisi za mabwana wakubwa si ndugu sasa"* (u.k 122)

Pia viongozi wanawapatia vijana ahadi hewa ili wawachague wakati wa uchaguzi na hatimaye hawa viongozi wakichaguliwa wanakosa kutimiza ahadi hizo.Katika tamthilia ya *Kigogo* tunawaonaVijana wakighadhibishwa na viongozi wa aina hiyo. Hitman anasema:

*“Wengine tulikuwa tumeahidiwa makubwa wakati wa vuguvugu la kuwania nafasi za uongozi. Haya yote husahaulika mara tu baada baada ya uchaguzi na kuvyazwa kwa serikali mpya. Tunaambiwanchi haina uwezo wa kuzalisha mali.”* (u.k 23)

Hiki ni kinaya kwa kuwa tungetarajia viongozi wakiahidi vijana ahadi chungu nzima wakose kuzitimiza.

Tungetarajia ugawaji wa hazina ya vijana ufanywe kwa njia halali. Katika tamthilia ya *Kigogo* ni kinaya kuwa, ugawaji wa hazina ya vijana ulifanywa kwa njia isiyo halali. Kuna kupendelea kutegemea nasaba ya mhusika au hata kabila lake. Suala hili linajitokeza kwenye wimbo wa Shamsi kama ifuatavyo:

*“Kwani hawakunikabidhi kazi*

*walizoahidi kwenye mabuku?*

*Kwani hawakunipa nyenzo*

*zakujiendeshea maisha?*

*Kwani walitupuuzilia mbali*

*tulipolilia kuhiniwa?*

*Nafasi za kazi*

*zilipotwaliwa*

*na ndugu zao*

*huku tukiambiwa kindanindani,*

*Viganja huoshana,*

*aso mwana aeleke jiwe*" (u.k 133)

Hatungetarajia kuwa hakuna usawa katka umiliki wa ardhi. Kwa mfano katika riwaya ya *Chozi la Heri* tunaona kwamba hakuna usawa katika kumiliki ardhi kwa nchi ya uhafidhina. Waheshimiwa ndio waliomiliki mashamba huko vijijini na jambo hili linadhihirisha uongozi mbaya. Hiki ni kinaya kwa kuwa tungetarajia pawe na usawa katika umiliki wa ardhi na jambo hili ni kinyume cha matarajio yetu.

Pia tume za kuchunguza kashfa za ufisadi zinatoa ripoti za uchunguzi wa kashfa hizo. Katika tamthilia ya *Kigogo*, viongozi hawatilii maanani mahitaji ya raia wake. Jambo hili linadhihirika kwa kuwepo kwa tume za uchunguzi wa kashfa mbalimbali kama za unyakuzi wa ardhi bila kutoa ripoti ya tume hizi. Hitman anasema:

*"Tunapolalamikia kashfa za unyakuzi wa hata vikataa vidogo tulivyo navyo, tunapozwa roho kwa kuambiwa", "Tumeunda tume ya kuchunguza kashfa hii kwa njia za udanganyifu watakabiliana na mkono thabiti wa sheri*a*"*(u.k 22)

Hapa ni kinaya kwamba mwananchi wa kawaida hadiriki kuziona ripoti za tume hizi kuhusu kashfa za ufisadi na hivyo kwamba wanakosa kupata haki za mali yao ambayo imeibiwa na matajiri.

### 4.1.5 KINAYA KATIKA UONGOZI MBAYA KWA *KIGOGO*

Hatungetarajia viongozi kuambia watu wasimamishe kazi zao kwa mwaka mmoja. Majoka anaagiza kuwa soko lifungwe kwa muda wa mwezi mmoja ili wanaSagamoyo kusherehekea miaka sitini ya uhuru iliyoshabihiana na siku ya kuzaliwa kwa Majoka (u.k

4). Hiki ni kinaya kwa kuwa Majoka kama kiongozi hafai kuwaambia watu ambao ni maskini wakose kufanya kazi zao.

Hatungetarajia viongozi wakose kusafisha mazingira pale wananchi wanafanyia kazi zao. Kwa mfano Wachonga vinyago kama vile Sudi katika soko la Chapakazi wanatujuvya kuwa uvundo unaokirihi katika soko hili unatokana na taka na kemiali kutupwa katika eneo hili (u.k 2). Hiki ni kinaya kwa uongozi wa Majoka kwa kuchangia pakubwa katika kuliharibu soko la Chapa kazi badala ya kulilinda.

Pia, vibarakala wa Majoka wanapanga njama ya kuwaangamiza wapinzani wake. Mfano ni pale bwana Kenga anapanga njama na wahuni chini ya mbuyu ili kuhakikisha kwamba wamewaangamiza wapinzani wa Majoka. Tunu anasema:

"*Mzee Kenga anapanga njama fulani. Anahutubia wahuni chini ya mbuyu* (u.k15)

Baada ya kupanga hayo, wahuni wake wanamuumiza Tunu ambaye ni mtetezi wa haki za wananchi wa Sagamoyo. Uongozi huu umekuwa ukiwaangamiza wanamapinduzi kama Jabali ambaye alipangiwa ajali na Kenga ambaye ni mshauri wa Majoka. Hiki ni kinaya kwa kuwa hatungetarajia serikali kuangamiza wapinzani wake.

Tena hatungetarajia viongozi wanyakue mali ya wanasagamoyo. Kulingana na maelezo ya Tunu, mipango ya Majoka kulifunga soko la Chapakazi na uuanzishaji wa mradi wa kujenga hoteli la kifahari ni kuwahini wanaSagamoyo kilicho chao. Tunu anamwambia Majoka:,

*"Usinifanyie masihara. Ninakukumbusha kuwa Wanasagamoyo wana haki ya kuishi, na ugatuzi sio unyakuzi. Nasikia mmebomoa vioski vilivyoko kwenye soko la Chapakazi*" (u.k 43)

Hapa kinaya kinaitokeza pale tunaona kuwa Majoka ananyakua mali ya Wanasagamoyo jambo ambalo ni kinyume cha matarajio ya Wanasagamoyo.

Pia ni kinaya kwa wananchi kutozwa kodi Zaidi na serikali ya Majoka. Kodi hii haitumiwi vyema kukidhia mahitaji muhimu kama vile kuwalipa waalimu na madaktari mishahara ifaayo. Ashua anamwambia Majoka:

"*Hakuna mchuuzi asiyelipa kodi.*" (u.k 25)

Kuna migomo ya madaktari wanaotaka nyongeza ya mishaharana jambo hili linadhihirisha kwamba kodi wanayolipa Wanasagamoyo haitumiwi vyema na uongozi wa Majoka.

Hatungetarajia kiongozi kuingilia biashara ya ukataji miti kwa kuwa miti huboresha mazingira na hata kuvutia mvua. Kwa mfano Majoka ambaye ni kigogo wa Sagamoyo anaendeleza biashara ya ukataji miti. Jambo hili limesababisha mvua kukataa kunyesha na wanaSagamoyo wanahofia kuwa isiponyesha hata maji ya kunywa yatatoka ng'ambo. Jambo la kushangaza ni kuwa kundi tawala limejichimbia visima vya maji na kuwasahau wananchi. Hashima anamwambia Siti:

"… *Hasara ni kwetu kina yakhe sasa, isiponyesha hata maji ya kunywa yatatoka ng'ambo*" (u.k 53)

Hapa kinaya kinajitokeza hapa kwa sababu hatungetarajia viongozi wa Sagamoyo wakate miti ili watu wakose maji na wao wajichimbie visima ili wasikose maji.

Mfano mwingine ni kwamba viongozi wanajitokeza wakiwa fisadi. Mfano tunapata serikali ya Majoka ikishiriki katika ufisadi. Ngurumo anasema:

*"... Tangu kufungwa kwa soko mauzo yetu ni maradufu. Mara kwa mara watu wa Kigogo wetu wakipitia hapa hawakosi kututupia mkono. Hapa kila mtu hupewa kwa raha zake*" (u.k60)

Hapa kinaya kinajitokeza pale tunaona kwamba viongozi wanaendelea kuwadhulumu maskini wa Sagamoyo Pia Kenga anatengewa kipande cha ardhi katika soko la Chapa kazi. Majoka anamwambia Kenga:

*"...Si unajua kipande chako sokoni tayari kimetengwa?. Pia sokoni wanyonge wanahangaishwa na wenye nguvu. Ashua anamwambia Kombe*: " *hakukaliki huko. Uvundo na kuhangaishwa na wenye nguvu ndiyo hewa tunayopumua huko. Kwetu wanadai kitu kikubwa au kitu chote.*" (U.k 5)

Tena hatungetarajia kiongozi kutoa ahadi kwa wananchi ambazo hatimizi na watu wanajuttia kwa kumteua kama kiongozi wao. Hiki ni kinaya kinachojitokeza pale tunamwona Majoka akitoa ahadi chungu nzima Majoka wakati wa sherehe za uhuru ambazo hazitimizwi. Husda anatueleza kuwa ni maneno ya kumtoa nyegere shimoni siku ya sherehe ya uhuru (U.k70).

Mfano mwingine kuwa hatungetarajia kiongozi kuipiga marufuku runinga yoyote kwa madai kwamba haimuungi mkono. Hali hii inajitokeza pale tunamwona Majoka akipanga njama ya kuikosesha runinga ya mzalendo nafasi hapo Sagamoyo. Hii ni baada ya runinga hii kutangaza habari za wanaharakati wa ukombozi na kutoa maoni kwamba Tunu ambaye alikuwa mpinzani wa Majoka alikuwa amemshinda Majoka kulingana na maoni yao baada ya kuwahoji wananchi wa Sagamoyo. Majoka anamwambia Kenga:

*" Sudi hatanikosesha usingizi, laiti angalijua salamu zinasomsubiri hapa na hii runinga ya Mzalendo nayo haina maisha Sagamoyo. Kitabakia kituo kimoja tu"* (u.k 37)

Hiki ni kinaya kwa kuwa hatungetarajia kiongozi kufunga runinga yoyote kwa kuwa zina uhuru wa kujieleza.

Pia serikali haiwachukulii wauzaji wa pombe haramu hatua. Ni kinaya kuona kuwa kuna wauzaji wa pombe haramu katika jimbo la Sagamoyo kama vile Asiya  Serikali inafaa uwachukulia hatua kali wanabiashara kama hao kwa kuwa pombe haramu huwadhuru watumizi wake kama vile kuna wale wanakufa na wengine kuwa vipofu. Kinaya ni kwamba Ngurumo anawaeleza kina Tunu kuwa ni serikali ya Majoka itowayo vibali vya kuuza pombe haramu na katiba haifuatwi. (u.k 61)

Tena kiongozi ambaye ameoa anakili kwamba hataacha kuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanawake wengine licha ya kuwa ameoa. Kwa mfano tunamwona Majoka akimwomba Ashua amkubali kuwa mpenzi wake hata kama ameoa . Pia tunamwona Majoka akisema:

"*Sitaacha kula mkate kwa kuchelea kiungulia*". (u.k 23)

Hapa Majoka anamaanisha kuwa hataacha kuwa na uhusiano na wanawake hata kama ameoa. Hiki ni kinaya kwani kiongozi anafaa kuwa kielelezo bora kwa umma anaouongoza.

Pia hatungetarajia kiongozi aongezee wafanyakazi mishahara kisha kupandisha kodi. Kinaya kinajitokeza pale serikali ya Majoka inatarajia kuwalipa wauguzi na walimu mishahara duni kisha kuwaongezea kodi. Kinaya kinajitokeza pale tunawaona walimu na wauguzi wakisitisha mgomo wao kwa kuwa wameongezewa mishahara yao na baadaye wanakuja kugundua kwamba hawajaongezewa kwa kuwa wameongezewa kodi kubwa.

Pia Majoka anapanga njama ya kumtambulisha Ngao Junior kama mrithi wake rasmi kwenye siasa.

Pia kiongozi anawanyima watu uhuru wa kuteua kiongozi wanaopendelea. Hapa kinaya kunajitokeza pale tunamwona Majoka akiwa dikteta kwa kusema kwamba mtoto wake Ngao Junior ndiye atamrithi kuwa kiongozi wa Sagamoyo (u.k 76).

### 4.1.6 KINAYA KATIKA UKATILI KWA *CHOZI LA HERI*

Ukatili ni kuwatendea watu matendo ya kinyama kwa kukosa huruma. Ukatili hutokea pale ambapo mtu au kundi la watu linawanyanyasa, kuwapiga na kuwaua wengine kwa sababu zao za kibinafsi jambo ambalo ni kinyume cha matarajio ya watu kama ifuatavyo:

Mfano mwingine ni pale tunampata mja ambaye amewasaidia majirani zake wao wamlipe kwa maovu. Jambo hili linajitokeza pale tunaona kwamba daktari Ridhaa ingawaje yeye ndiye aliyebadilisha Ughaishu kutoka jangwa na kuwa msitu uliokoleza rangi ya Chanikiwiti, majirani walimchomea jumba lake na familia yake mpaka akapata mfadhaiko wa akili na ikabidi baadaye afanyiwe ushauri nasaha (u.k 3). Hiki ni kinaya kwa kuwa tungetarajia hao majirani wailinde familia yake kwa kuwa amewasaidia sana lakini unaona wakiangamiza familia yake kwa kuwateketeza mke, watoto wake na mjukuu wake.

Tena, hatungetarajia mtu ambaye anawasikitikia watu wale wengine wanaoteswa na wahalifu naye kuvamiwa na kutendewa uovu uo huo. Tukio hili linajitokeza pale tunamwona kaizari akivamiwa na mabarobaro watano wakati wakitazama runinga akisikitika yale mauaji ya vijana waliokuwa wanaandamana na kuuawa na walinda

usalama. Subira mkewe alizabwa kofi na kukatwakatwa kwa sime akazimia nao Mabinti zake Lime na MwanaHeri wakabakwa mbele ya baba yao (u.k25). Hiki ni kinaya kwa kuwa hatungetarajia Kaizari ambaye anatazama kwa runinga uovu wanagamoyo wanatendewa naye familia yake inatendewa uovu huo.

Mfano mwingine ni pale hatungetarajia mzazi yeyote kufanya uzinzi mbele ya watoto wake. Tunamwona watoto wa Kimai mke wa bwana Tenge kutendwa na baba yao ukatili. Aliwaleta wanawake katika chumba chao kimoja walimoishi wakati mkewe amesafiri. Chandachema anaambia wenzake,

"*Usiniulize niliyaona na kuyasikia mangapi katika chumba hiki ambacho kiligeuka danguro wakati Bi. Kimai alipokuwa ameenda mashambani. Wakati huu Bwana Tenge angeamua kumleta mwanamke mmoja baada ya mwingine, hapo hapo, mbele ya macho ya wanawe, hadi usiku wa kuamkia siku ya kurudi kwa Bi. Kima*i (u.k 106)

Hiki ni kinaya kwa kuwa bwana Tenge anawadhulumu watopto wake kisaikolojia kwa kufanya uzinzi na wanawake wengine mbele ya watoto wake. Pia kinaya kingine ni pale anafanya uzinzi na kumwendea mkewe mwaminifu kinyume cha matarajio yake.

Pia hatungetarajia mfadhili wa makiwa kuanza kulalamika kuwa huyo yatima anatumia vitu vya nyumbani vibaya. Tunamwona Satua ambaye ni jirani wa chandachema na ambaye aliahidi kukaa naye wakati wazazi wake walipofariki kumtendea Chandachema ukatili kwa kumsimanga wakati alipoenda kuishi nao. Chanda chema anasema,

*"Satua alianza kulalamikia hili na lile. Alilalamikia kuisha haraka kwa sukari, alilalamikia matumizi ya kiholela ya sabuni ya kuogea, alinung'unika kuhusu kubanana kwa jeshi la watoto kwenye chumba cha malazi …zadi kila kitu kilikuwa na doa machoni mwa Satua*" (u.k103)

Hapa kinaya kinajitokeza pale tungetarajia Satua kuishi na Chandachema kama mtoto wake bila kulalamikia vile anatumia vitu vya nyumbani lakini tunaona analalamika.

Isitoshe tungetarajia mzazi ampatie mtoto wake malezi mema. Mfano tunamwona mwalimu Fumba akimtendea Chandachema ukatili kwa kumtelekeza kwa nyanya yake bila msaada wowote wa malezi yake na kisha kuhamia ughaibuni pamoja na familia yake. Chanda chema anasema:

"*Nasikia baba yangu Fumba alikuwa kahamia Uingereza na familia yake, anafundisha katika chuo kikuu*" (u.k 102)

Hiki ni kinaya kwa kuwa tungetarajia mwalimu Fumba kumlea mtoto wake aliyetokana na uzinzi wake na mwanafunzi wake wa kidato cha pili.

Pia tunamwona mwalimu kufanya uzinzi na mwanafunzi wake. Rehema anringwa na mwalimu wake Fumba aliyepaswa kuwa mshauri wake. Katini alimwambia Chandachema, "*Mama yako ni mzaliwa wa pwani. Huko ndiko babayako Fumba alikokuwa akifundisha alipokutana naye. Fumba alisuhubiana na Rehema akiwa kidato cha tatu. Wewe ni zao la uhusiano huo.* (u.k 103)

Tena hatungetarajia mzazi kuwatelekeza watoto wao na kuwafanya waibiwe na wafanyakazi wa nyumbani. Mfano tunamwona Naomi akiwaacha watoto wake (Umu,

Dick na Mwaliko) wakiwa wadogo. Naomi alimwandikia Lunga barua ya kumwambia ametoka kwake kama ifuatavyo.:

*"Nimeondoka. Acha nitambe na ulimwengu, huenda nikaambulia cha kukusaidia kuikimu familia. Nasikitika kwa uchungu nitakaokusababishia wewe na wanao. Kwaheri"* (u.k 81)

Hiki ni kinaya kwa kuwa Naomi hakuwajali watoto wake na mwishowe wanakuja kuibiwa na kijakazi wao Sauna.

Tena hatungetarajia mama mkwe kusingizia wake ambao wameolewa kwake kwamba ni wao chanzo cha masaibu ya familia yake. MwanaHeri anaelezea kuhusu mama yake subira kama ifuatavyo:

"*Daima mama alichukuliwa kama mgeni, si katika boma letu tu, bali pia katika kijiji kizima…uhasama ulizidi baada ya vurugu za miaka mitano iliyopita. Nyanya alimwona mama kuwa chanzo cha kuharibiwa kwa mali yetu, kwamba ndiye aliyewafanya majirani zetu kutuchomea boma ili watuondolee gugu ambalo liliutia najisi utambulisho wetu*" (u.k 95)

Isitoshe baadhi ya wakimbizi wanajigawia chakula maradufu kuliko wale wengine. Kinaya kinajitokeza pale bwana Kuti ambaye alikuwa diwani hapo awali yeye na familia yake kwa kujigawa mara tatu na kuwatendea wakimbizi wale wengine ukatili kwa kuwa yeye na familia yake walichukua chakula mara tatu zaidi ya wakimbizi wale wengine (u.k 33).

Hatungetarajia mwanamke ambaye ameolewa kumwacha mumewe peke yake na kwenda kuishi ng'ambo. Ukatili unajitokeza pale tunampata Kiriri akiachwa na mkewe Annette alipokimbia na kwenda ng'ambo na akamwachia upweke hata baada ya rai za mumewe kwamba asimuache peke yake alikataa (u.k 65). Hapa kinaya kinajitokeza pale tunaona baada ya Kiriri kumrai mkewe tungetarajia mkewe kubadili nia yake lakini tunaona kwamba alikataa.

Tena, hatungetarajia polisi kuzima zogo baada ya uchaguzi kwa kuwapiga watu risasi. Hapa kinaya kinajitokeza pale wanawapiga watu risasi na kwa kutumia risasi wakati wa baada ya uchaguzi(u.k 24). Tungetarajia polisi wawatulize waandamanaji hawa kwa amani lakini tuinapata kuwa vijana wengi wanapoteza roho zao.

Tena ni kinaya kwa  waajiri kuwashurutisha wafanyakazi wao kufanya na wao mapenzi ili waendelee kuwadumisha katika kazi zao. Kinaya kinajitokeza pale tunaona ya kwamba katika riwaya ya *Chozi la Heri,* Naomi anafutwa kazi na bwana Kimbaumbau kwa kukataa kujihusisha naye katika ngono. Ni kinaya kwa Naomi kuajiriwa kazi na Kimbaumbau ambaye alikuwa na nia ya kumhujumu na kumtendea unyama kwa kumnajisi. Anaposhindwa kutekeleza haya, anamfuta kazi (u.k 121).

### 4.1.7 UKATILI KATIKA TAMTHILIA YA *KIGOGO*

Hatungetarajia viongozi  kutumia vitisho na kuwanyang'anya wafanyabiashara mali zao. Katika Sagamoyo ni kinaya kwamba viongozi wanatumia vitisho na kuwanyang'anya wafanyabiashara soko lao pale walikuwa wanauzia bidhaa zao. Haya yanadhihirika katika kauli ya Sudi anaposema:

"*Si haki kuchukua kilicho chetu na kututisha*" (u.k 3)

Tena, hatungetarajia watu wanaoandamana kwa amani kuuawa. Katika Sagamoyo kinaya kinajitokeza pale watu wanaoandamana Vijana watano waliokuwa wakifanya maandamano ili kupinga kupanda kwa bei ya chakula katika kampuni ya Majoka wanauawa nao wachuuzi sokoni wanaumizwa na walinda usalama. Siti anasema:

*"Vijana watano. Wachuuzi sokoni waliokuwa wakiandamana pia wameumia*"(u.k 16)

Hatungetarajia Viongozi wa upinzani wanaopinga utawala wa kiimla wa Majoka wanalemazwa kisiasa na hata kuuawa. Viongozi wanatumia mbinu za kisiri kuwaua washindani ili kuficha ukatili wao. Kwa mfano, Jabali, kiongozi wa upinzani ambaye alikuwa na chama chake cha Mwenge, aliuliwa katika ajali ya barabarani na chama chake cha Mwenge kusambaratishwa (u.k 36)

Tena hatungetarajia wpinzani wa viongozi katika Sagamoyo kujeruhiwa. Katika tamthilia ya *Kigogo*,mpinzani wa Majoka anayeitwa Tunu anavamiwa na wahuni wanaomjeruhi kwa kumvunja mfupa wa muundi. Tunaona Kenga akimwambia Majoka:

"*Hawakumvunja mguu wa kitamathali. Tunu bado yuko" (u.k* 68)

Hiki ni kinaya kwa kuwa uvamizi huu unaonyesha udhalimu wa viongozi kwa sababu wahuni waliomvamia walitumwa na viongozi wenyewe ambao hawawezi kudhaniwa na wanaachi wa Sagamoyo.

Hatungetarajia wananchi wa Sagamoyo ambao wako katika nchi huru kuishi kwa hofu. Katika nchi ya Sagamoyo tunapata kuwa ni kinaya watu kuishi kwa hofu kutokana na uvamizi wa mara kwa mara. Kwa mfano, Hashima na Siti hawana utulivu kwa sababu ya hali mbaya ya usalama jimboni. Hashima anasema:

*“Nusura roho inianguke mwanangu, wametutia woga mwingi sana. Twaishi kwa hofu. Kila siku tuamkapo, mimi na Tunu wangu, twapiga alhamdulilahi”* (u.k 5)

Jambo hililinadhihirisha kinaya kwa kuwa hatungetarajia wanaSagamoyo kuishi kwa hofu ya kuvamiwa na wenzao ambao wanatarajiwa kuishi kwa amani.

Tena, hatungetarajia watu kutiwa mbaroni bila hatia yoyote. Kinaya kinajitokeza pale tunapata kuwa wanawake ambao wanakataa kujihusisha kimwili na viongozi kwa mfano, Ashua, licha ya kwamba ananyonyesha na wanawe kulala njaa, anatiwa mbaroni na kupigwa bila kosa (u.k31).

### 4.1.8 UNAFIKI KATIKA KINAYA KWA *CHOZI LA HERI*

Unafiki ni hali ya mtu kujifanyanya mwema kwa lengo la kuyaficha maovu. Ni kinaya kwa wahusika kutumia unafiki kuyaficha maovu yao. Mambo wanayoyatenda ni kinyume na wanayoyasema kama ifuatavyo:

Mfano wa unafiki ni pale tunapata watu wakifanyia majirani yao maovu ilhali hapo mbeleni walikuwa marafiki. Mfano ni pale Mzee Kedi aliteketeza familia na mali yote ya Ridhaa hata kama alikuwa jirani yake na kumfanya augulike moyoni alipokumbuka mkewe Terry, watoto wake wawili, mkazamwana Lily na mjukuu Becky. Hapa kinaya kinajitokeza pale tunaona kwamba hapo mbeleni alikuwa akijifanya mwema kwa Ridhaa. Lakini mwishowe anamtendea maovu.ni unafiki kwa kuwa Ridhaa alikuwa amempatia mtoto wake mhandisi Kombo kazi ya kusimamia ujenzi wa nyumba yake. Pia mkewe mzee Kedi na mkewe Ridhaa walikuwa marafiki (u.k 3).

Hatungetarajia mwalimu kumringa mwanafunzi wake kwa kuwa jambo hilo ni kinyume na taalima yake. Katika riwaya ya *Chozi la Heri* Mwalimu Fumba anamringa mwanafunzi wake Rehema akiwa kidato cha tatu. Mwalimu Fumba alikuwa mnafiki kwa kuwa alikuwa anajifanya kwamba ana maadili mema lakini tunaona akijihusisha na mwanafunzi wake kimapenzi na kumfanya awe mjamzito (u.k 103).

Tena ni kinaya kumwona mzazi akimringa mtoto wake kwa kuwa anafaa kuwa mlezi wake. Mfano ni kwamba bwana Maya anamdhulumu binti yake wa Kambo Sauna, hata akapata mimba. Huu ni unafiki kwa kuwa alikuwa anajifanya mlezi mwema kwa Sauna na mwishowe kumfanyia unyama (u.k 152). Hiki ni kinaya kwa kuwa hatungetarajia bwana Maya kumringa bintiye.

Tena tunamwona mama mkwe akimsingizia mkaza mwanawe kuwa ndiye anasababisha familia yake kushambuliwa. Mfano unajitokeza pale Subira anasingiziwa na mama mkwe kuwa ndiye alisababisha kushambuliwa Ni kinaya kwa mkwe wake Subira kumsingizia kuwa yeye ndiye aliyesababisha familia yake kushambuliwa. Kwa mfano binti zake wawili yani Lime na MwanaHeri walibakwa na mabarobaro watano na mali yake na mumewe Kaizari kuteketezwa. Huu ni unafiki wa mama mkwe wake kwa kuwa alimchukia kwa kuwa alikuwa wa kabila tofauti na mumewe (u.k154).

Isitoshe tunawaona wanandoa wanapokosa watoto wakikashifiwa na majirani. Kinaya kinajitokeza pale Mwangemi na Neema walikuwa hawana mtoto. Kitoto kimoja walichopata kilifariki kutokana na ugonjwa wa Selimundu. Ni unafiki kwa majirani kumchekelea na kumkashifu Neema kwa kukosa mtoto. Ilimbidi yeye kutafuta usalama kwa kutafuta mwana wa kupanga (Mwaliko) (u.k 154) Kinaya kinajitokeza pale ambapo

tungetarajia majirani walioishi nao kwa uhusiano mwema kwa miaka mingi wamhurumie alipokosa mtoto lakini tunaona kwamba walikuwa mstari wa mbele kumkashifu.

Tena, wagonjwa wa Ukimwi na Saratani wanateseka wakati serikali ilikuwa inazitoa bure ili wapewe katika hospitali bila malipo. Ni kinaya kwa wagonjwa katika hospitali za umma kuteseka kutokana na maradhi ya ukimwi na saratani huku dawa zao kunyakuliwa na viongozi waliozipeleka kwenye maduka yao ya dawa. Huu ni unafiki wa hawa viongozi waliokuwa wamewaahidi matibabu na dawa za bure wakati wa kampeni. Jambo hili lilisababisha Selume afikirie kustaafu mapema. Selume anasema:

"*Tazama pia dawa za kukabiliana na makali ya ukimwi na saratani. Wanaoweza kuimudu gharama yazo ndio hao hao wanaozinyakua dawa zilizotengewa raia wasiojiweza*" (u.k 140-141)

Hapa kinaya kinajitokeza pale tunawaona wagonjwa wa ukimwi na saratani kupiga dunia teke ilhali wale viongozi wanaowaambia kuwa wanawashughulikia wananufaika na dawa zao.

Mfano mwingine ni pale wasimamizi wa ardhi ambao wameaminiwa sana na watu wanatumia ulaghai kuwatapeli. Ni kinaya pale ambapo wasimamizi wa ardhi wana unafiki kwa kuwa matapeli kwa kuuza ardhi kwa njia ya udanganyifu. Kwa mfano ardhi ambayo ina wamiliki tayari, huuzwa tena. Aidha wanunuzi hupata hasara kubwa (u.k 6). Hiki ni kinaya kwa kuwa hatungetarajia hawa wasimamizi wawatapeli watu wanaowaamini sana.

Tena viongozi wanawaahidia vijana ahadi nyingi ambazo hawatimizi. kinaya katika riwaya ya *Chozi la Heri* kinajitokeza pale wanasiasa wanajifanya wazuri sana kwa vijana

kwa kuwaahidia ahadi nyingi ili wawateue katika uongozi. Baada ya kuchaguliwa, hawa wanasiasa wanawasahau kabisa. Wanawafanya vijana hawa kuwa na msongo wa mawazo na wengi wao wanaandamana kwa hasira na kuharibu mali kama vile Hitman anayeteketeza gari la usafiri bila kujali abiria waliokuwa ndani (u.k 123).

Pia akinamama wanajifungua watoto na kisha kuwatupa katika jalala. Katika nchi hizwahafidhinaNi kinaya kwa wamama kuwa wanafiki kwa kujifungua watoto na kisha kuwatupa kwa jalala kwa mfano Neema anaokota kimoja na kukipeleka kwa makao ya Benefactor kikapewa jina la Riziki Immaculata. Neema anasema,

"*Hata hivyo, nguvu imara za kimaumbile zilinisukuma, nikainama kwenye mchafukoge huo wa taka. Nilitwaa ile karatasi ya sandarusi, nikaifunua na kupata kilaika cha kike*" (u.k 161)

Pia, hatungetarajia mwanamume ambaye ameoa kuwa mzinzi. Kinaya kinajitokeza kwa bwana Tenge aliyekuwa na unafiki. Alikuwa anajifanya kuwa mwaminifu kwa Bi. Kimai wakati alikuwa nyumbani. Wakati Bi. Kimai alisafiri mbali kufanya kazi, bwana Tenge alikuwa analeta wanawake wengine chumbani mwao na kufanya uzinzi nao mbele ya watoto wao. Jambo hili lilisababisha athari za kisaikolojia kwa watoto wao. Hapa kinaya kinajitokeza pale tunaona kwamba mkewe Kimai alikwa anamwamini sana lakini kumbe alikuwa mnafiki.

Tena vijakazi wanaoaminiwa sana na waajiri wao, wanawatorosha watoto wao. Ni kinaya Kijakazi Sauna kujifanya mwema kwa watoto wa Lunga aliokuwa akiwalea. Kinaya ni kwamba baada ya Lunga kufariki, Sauna aliwaiba watoto wawili yani Mwaliko na Dick na kwenda kuwauza (u.k 81).

Isitoshe, hatungetarajia tajiri kumnyang'anya maskini shamba lake kwa kuwa anaelewa hali yake. Kwa mfano ni kinaya kwa bwana Mabavu ambaye ni tajiri kujifanya mwema kwa baba yake Shamsi lakini mwishowe anamnyang'a ardhi yake kwa njia ya utapeli (u.k 131). Hiki ni kinaya kwa kuwa tungetarajia bwana Mabavu ambaye ni tajiri amsaidie baba Shamsi ambaye ni maskini kwa kuwa anashindwa hata kumwelimisha Shamsi.

Tena tungetarajia viongozi wahahakishe kuwa kuna dawa hospitalini za kuwatibu wagonjwa ili wasife kutokana na ugonjwa. Ni kinaya kwa baba yake Shamsi kufariki kutokana na kula mizizi yenye vijisumu alipokuwa anajikinga kwa makali ya njaa. Hakuweza kupata matibabu kwa sababu hapakuwa na dawa kutokana na ufisadi wa wakubwa hospitalini. Huu ni unafiki wa wakubwa kwa kuwa walifaa kupatia wagonjwa dawa lakini waliziiba na kuuza kwa maduka yao (uk 134-135).)

Tena, wasimamizi wa vyuo wanatoa fedha kwa upendeleo na kukosa kuwasaidia wanafunzi kutoka familia maskini. Tunapata tukio la vijana wa chuo kikuu kuwa na msongo wa mawazo kutokana na ukosefu wa fedha za mikopo na ruzuku za kulipia chuo kikuu. Jambo hili linatokana na unafiki wa wasimamizi wa vyuo hivyo kutoa fedha kwa upendeleo (u.k 142). Kinaya kinajitokeza pale wasimamizi katika vyuo hivi wanatoa fedha za mikopo na ruzuku kwa wanafunzi kutoka familia za matajiri kinyume cha matarajio yetu pale ambapo tungetarajia wawapatie wanafunzi kutoka familia maskini.

Hatungetarajia mwanamke kumwacha mumewe kwa sababu mumewe amefutwa kazi. Mfano tunampata Naomi katika riwaya ya *Chozi la Heri* akimtoroka Lunga wakati alipokuwa anamhitaji Zaidi alipofutwa kazi. Huu ni unafiki kwa kuwa wakati Lunga alikuwa na kazi Naomi alikuwa anampenda sana lakini akamwacha wakati alifutwa kazi (u.k 82). Hiki ni kinaya kwa sababu tungetarajia Naomi kuendelea kuishi na Lunga na kumtia moyo wakati alifutwa kazi.

### 4.1.9 KINAYA KATIKA UNAFIKI KWA *KIGOGO*

Hatungetarajia viongozi kutoa hotuba kwamba watu wasiwaruhusu wale wanadhulumu maskini waendelee katika maeneo yake na yeye ndiye anayewadhulumu hao maskini. Mfano tunapata Majoka akisema kuwa kuwa wanasagamoyo wasiruhusu watu wachache waliojazwa kasumba za kikoloni kuwarejesha katika utumwa. Pia, anadai kuwa hawawezi kukubali kutawaliwa kidhalimu tena ilhali yeye anayatenda mambo yayo hayo anayokashifu. Huu ni unafiki vile anawadhulumu wapinzani wake kama vile Tunu na Jabali. Kwa mfano alikuwa amepanga kuuawa kwa wapinzani hawa wawili na tunaona Jabali aliuawa kwa madai kuwa alikufa kutokana na ajali ya barabara. Naye tunu wale walipewa kazi ya kumuua walishindwa kutekeleza njama hiyo lakini wakamvunja mfupa wa muundi. Pia, tunamwona Majoka akitegemea pesa za wafadhili kutoka mashariki na magharibi katika kujitajirisha badala ya kuwasaidia maskini wa Sagamoyo. (u.k 10). Hiki ni kinaya kwa kuwa yeye Majoka ndiye anayewadhulumu WanaSagamoyo.

Tena, wimbo wa uhuru unawasifu viongozi wanaowanyanyasa wananchi badala ya kuwakashifu. Mfano wimbo wa uhuru unatumiwa kumsifu Majoka. Unammiminia sifa kiongozi ambaye anawakandamiza wananchi. Kupitia kwa wimbo huo, Majoka na familia yake inajitia sifa bandia ili wazidi kupendwa nao umaarufu wao uenee zaidi na huu ni unafiki (u.k3). Hiki ni kinaya kwa kuwa hatungetarajia Wanasagamoyo kumsifu Majoka ambaye amesababisha vifo vya watu wengi katika jimbo lake. Kwa mfano Majoka alitoa amri kwa polisi kuwaua vijana watano waliokuwa wakiandamana na kulalamikia bei ya juu ya chakula katika kampuni iliyomilikiwa na Majoka na hao vijana wakauawa kiholela.

Mfano mwingine, ni pale viongozi wanaamrisha soko lifungwe ili wajijengee hoteli la kifahari ilhali tunapata kuwa wachuuzi wengi walilolitegemea soko hili wanaishia kuteseka pamoja na familia zao. Mfano tunapata kuwa soko linafungwa ili kina Sudi wakose riziki kisha walazimishwe kuyatimiza matakwa ya viongozi. Majoka anamwambia Ashua:

"*Ha-ha-ha-ha… Soko halifunguliwi ng'o. Limefungwa milele"* (u.k 25)

Hiki ni kinaya kwa kuwa hatungetarajia kiongozi Majoka kuwafungia maskini soko lao pale wanafanyia biashara zao ili waweze kujikimu na kukimu familia zao.

Hatungetarajia viongozi kuwafumanisha wake zao na wanawake wengine katika ofisi zao ili kusababisha vita baina yao na kusababisha hao wanawake wengine wafungwe jela kwa kuwa wamekataa kuwa na uhusiano wa kimapenzi nao. Kwa mfano, njaa inamsukuma Ashua kwa Majoka akienda kutafuta msaada wa chakula. Anapokataa kufanya mapenzi na Majoka, yeye Majoka anamwita mkewe ofisini ili itokee rabsha. Mkewe anapompata Ashua ofisini ya mumewe anamtusi hawara na wanaanza kupigana. Baadaye, Ashua anatiwa ndani ili kumlazimisha Sudi mumewe kumchongea Majoka kinyago ili Ashua mkewe aachiliwe huru na huu ni unafiki wa viongozi. Ashua anamwambia Majoka,

"*Wanangu wamelala njaa…hawajala"* (u.k 22)

Hapa kinaya kwa kuwa tungetarajia Majoka kama kiongozi wa Sagamoyo amsaidie Ashua kwa chakula ili alishe watoto wake lakini anamwamuru kwamba lazima kwanza afanye mapenzi naye ili amsaidie. Kama kiongozi, hatungetarajia Majoka kuwa na hulka ya uzinzi.

Mfano mwingine ni kwamba hatungetarajia viongozi kuwaongezea wananchi mishahara kisha waongeze kodi ili hawa wananchi wasinufaike. Mfano ni pale tunapata viongozi wanapanga kuongeza mishahara ya walimu na wauguzi kisha wapandishe kodi ndipo pesa ziwarejee walimu na madaktari wasinufaike na nyongeza ya mshahara. Kenga anasema:

*"Ni mbinu ya kutia kwa kushoto na kutoa kwa kulia*."(u.k 36). Huu ni unafiki kwa kuwa watawala hawa wanahakikisha kuwa wanapata sifa nzuri kwa kuongeza mshahara na wakati uo huo wanatoza watumishi hawa kodi kubwa.

Hatungetarajia viongozi kupanga wapinzani wao wanawake waolewe na watoto wao ili kudhoofisha upinzani. Mfano tunampata Majoka akipendekeza Tunu aolewe na Ngao Junior. Tunu anapokataa, anamshauri aachane na Sudi kwa sababu wana ajenda mbili tofauti. Anamwambia amtafute mume amwoe. Mbinu hiyo inapokosa kufaulu, anatuma wahuni kumuua Tunu lakini haewatekelezi uhalifu huo wa mauaji na badala yake wananmvunja mfupa wa muundi. Wahuni hao wanaeneza propaganda kwa kusema kuwa Sudi na Ashua ndio wanaowinda roho ya Tunu ili Tunu atengane na Sudi. (U.k 54). Hapa kinaya kinajitokeza pale hatungetarajia Majoka kama kiongozi wa Sagamoyo kumshawisha Tunu kuolewa na mtoto wake Ngao Junior ili kuzima upinzani.

Hatungetarajia kiongozi kusema wafu wazikwe kwenye makaburi yaliyojaa na wazikwe juu ya wengine na anaendelea kusema kwamba kibarakala wake mmoja auawe na watu waanze maandamano kutokana na kifo chake ili watu wasielekeze macho yao kwa wale wanazikwa kwa maziara yaliyojaa bali waelekeze macho yao kwa waandamanaji. Kwa mfano, tunaona kwamba baada ya kifo cha Ngurumo, Majoka anapendekeza kuuliwa kwa chatu Moja kama njia ya kuwafanya watu wasitilie maanani kifo cha Ngurumo,

badala yake wafanye maandamano wakilalamikia kuuliwa kwa chatu. Kwa njia hiyo, kamera zote zitaelekezwa kwa waandamanaji ili watu wasione namna makaburi yalivyojaa (u.k 72). Hiki ni kinaya kwa kutuonyesha sifa hasi ya Majoka ya kuwa muuaji kwa sababu Chatu alikuwa kikaragosi wake na anapendekeza auawe.

Viongozi wanawafukuza wafadhili wa wapinzani wao wanaotetea haki za watu katika Sagamoyo na kuwaunga mkono wapinzani wanaowaunga mkono. Kwa mfano, Viongozi wanakopa pesa kutoka kwa wafadhili ambao wanaunga serikali mkono. Hata hivyo, wanapanga njama ya kuwafukuza wafadhili ambao wanapinga utawala wa kiimla kwa kuwafadhili wapinzani wanaozipigania haki za wengi. Wanadai kuwa wanajiweza wenyewe kwa wenyewe huko Sagamoyo (u.k 33).  Kinaya cha unafiki wao ni kuwa nia yao ni kuzisambaratisha shughuli za wapinzani.

Hatungetarajia serikali vyombo vya dola kueneza propaganda. Mfano katika tamthilia ya *Kigogo* viongozi wanatumia vyombo vya dola kama vile televisheni na askari kueneza propaganda. Unafiki ni kuwa kwa sababu wameshindwa kutekeleza majukumu yao, inawabidi kutumia mbinu za udanganyifu ili kuonekana wema mbele ya umma na kuficha maovu yao (u.k 37)

Isitoshe viongozi wanakodisha mabasi ili wawasafirishe wafuasi wao kwa mikutano yao. Kwa mfano, viongozi wa Sagamoyo Wana mazoea ya kuwasafirisha wafuasi kwa mabasi kuhudhuria mikutano yao.  Kenga anajuta kuwa iwapo wangejua kwamba watu hawatahudhuria mkutano wao, Wangekodisha mabasi ya kuwasafirisha vijana na kina mama kuja kuuhudhuria. Hiki ni kinaya kwa sababu wanatumia mbinu ya kuwapumbaza wananchi kwamba viongozi wao bado wana umaarufu wakati ambapo ni dhahiri kwamba watu hawawapendi tena (u.k 87).

# SURA YA TANO

# KINAYA KUSAWIRI SIFA ZA WAHUSIKA KATIKA RIWAYA YA *CHOZI LA HERI* NA TAMTHILIA YA *KIGOGO*

## UTANGULIZI

Sura hii imeongozwa na mhimili wa nadharia ya kimtindo unaodokeza kuwa kila kazi ya fasihi ina ubunifu fulani ambao unapochanganuliwa kwa undani husaidia uelewekaji wa undani wa matini za fasihi kulingana na madai ya Simpson (2004). Utafiti huu unaelezea vile Matei katika riwaya ya *Chozi la Heri* na Kea katika tamthilia ya *Kigogo* walivyodhihirisha sifa za wahusika bila ya kutumia njia ya moja kwa moja bali kwa kutumia kinaya kama ifuatavyo:

## 5.1 WAHUSIKA KUBAINISHA KINAYA KWA *CHOZI LA HERI*

Utafiti huu umedhihirisha wahusika ambao wanatenda mambo kinyume na matarajio ya watu au wasomaji wake. Wahusika hawa ni : Zohali, Sauna, Pete na bwana Maya na Mwimo msubili.

### 5.1.1 SIFA ZA ZOHARI KUBAINISHA KINAYA KATIKA *CHOZI LA HERI*

Zohali ni binti mwenye wazazi ambao wana maisha mazuri. Mama yake ni mwalimu mkuu. Ni kijana aliyekumbwa na changamoto za ujana kwa kushindwa kudhibiti matamanio ya mwili na kujikuta anapata ujauzito akiwa angali mdogo. Alikosa upendo wa wazazi baada ya kupata ujauzito na kuachishwa masomo akiwa bado kidato cha pili. Utafiti huu umedhihirisha sifa hasi za zohali ambazo ni kinaya cha matarajio ya watu au wasomaji wa riwaya hii ya C*hozi La Heri* kama zifuatazo:

Yeye anajitokeza kama mzinzi pale tunaona kwamba alishindwa kudhibiti hisia za ujana akajikuta amepata ujauzito akiwa bado katika umri mdogo na akiwa kidato cha pili (u.k 98). Hiki ni kinaya kwa kuwa hatungetarajia mwanafunzi kama vile Zohali akijihusisha na mapenzi yanayosababisha uja uzito wake akiwa kidato cha pili.

Pia anajitokeza kama mwongo kwa kuwa anmdanganya mtawa Pacha kuwa wazazi wake walifariki na wajomba wake wenye tama wakampora urithi (u.k 100). Hiki ni kinaya kwamba hatungetarajia Zohali amdanganye mtawa pacha kuwa wazazi wake walifariki na walikuwa hai.

Zohali anajitokeza kama mwenye kinyongo kwa kuwa anashindwa kuwasamehe wazazi wake na badala yake ameamua hata kutowapelekea mtoto wamuone wakati aliambulia ujauzito. Hiki ni kinaya kwa kuwa tungetarajia wazazi wa Zohali wamuone mjukuu wao lakini Zohari akawanyima nafasi hiyo (u.k 103).

Pia ni mwenye kutamauka kwa sababu alishindwa kuvumilia kazi alizopewa na wazazi wake baada ya  kupata ujauzito (u.k 103). Ni kinaya kwa Zohali kushindwa na kazi za nyumbani alizopewa na wazazi wake baada ya kuambulia uja uzito na akatoroka kwao. Tungetarajia Zohali afanye kazi hizo ili wazazi wake wamtunze hadi paleatakapojifungua na wamsaidie kulea mjukuu wao.

### 5.1.2 SIFA ZA SAUNA KUBAINISHA MAUDHUI KATIKA CHOZI LA HERI

Alikuwa mfanyakazi aliyekuwa anaajiriwa kufanya kazi za nyumbani. Katika riwaya hii anadhihirisha sifa ambazo ni kinyume cha matarajio ya watu kama vile:

Yeye anajitokeza kama mhusika mwovu kwa kuwa alifanya uovu wa kuwatorosha Dick na Mwaliko kuwapeleka kwa watu kama vile Bi. Kangara na mzee Buda wanaolangua

binadamu (u.k 156). Hiki ni kinaya kwa kuwa tunaona kwamba Sauna alikuwa ameaminiwa na waajiri wake na hatungetarajia kwamba anaweza kuwatorosha watoto wao kama vile alivyofanya.

Pia yeye ni mnafiki kwa kuwa alionyesha tabasamu la kinafiki kwa polisi huku akijua kuwa siku yake ya arobaini imetimia (u.k 158). Hapa hatungetarajia atabasamu wakati alishikwa na polisi kwa kuwa alikuwa achukuliwe hatua kali kwa sababu ya kufanya biashara ya kuwalangua watoto.

Tena anajitokeza kama mhusika mwongo pale alimdanganya Dickson kuwa akienda kwa Buda atasomeshwa (u.k 154). Hapa kinaya kinajitokeza pale hatungetarajia Sauna kumdanganya Dick kuwa anapelekwa kwa Buda ili aendelee na masomo yake ilhali alikuwa anampeleka huko ili awe analangua dawa za kulevya.

Yeye anajitokeza kama mvunja ahadi kwa kuwa aliwaahidi Umuikheri, Dick na Mwaliko kuwa angewatunza baada ya kifo cha Lunga lakini hakutimiza ahadi hiyo. Kinyume chake aliendа kuwauza Dick na Mwaliko (u.k 140).

### 5.1.3 SIFA ZA PETE KUBAINISHA KINAYA KATIKA RIWAYA YA CHOZI LA HERI

Huyu ni miongoni mwa wagonjwa waliolazwa katika kituo cha afya cha Mwanzo Mpya. Ni maskini anayeishi kwa dhiki kwenye mitaa ya mabanda. Ingawa ana umri mdogo, tayari ana watoto watatu. Wazazi wake hawakuwajibika katika kumlea na badala yake alilelewa na nyanya yake. Aliozwa kwa bwana Fungo mara tu alipopashwa tohara kutokana na mila zao. Baadaye, aliondoka kwa mumewe baada tu ya kujifungua kwa sababu ya kuchoshwa na masimango. Baadaye, aliishi na Nyangumi ambaye alimwacha

baada ya kupata mtoto mwingine. Alitenda matendo ambayo ni kinyume cha matarajio yetu kama vile:

Ni mwepesi wa kushawishika kwa kuwa alimwamini Nyangumi kwa haraka na kuishi naye lakini baadaye Nyangumi anamsaliti, akamwacha na kurudi kwa mkewe (u.k 151). Hiki ni kinaya kwa kuwa hatungetarajia Pete kushawishika kwa haraka na Nyangumi bila kuchunguza kama alikuwa na mke.

Pia anajitokeza kama mlevi wakati akifanya kazi ya kuuza pombe alilewa na kujikuta amejihusisha kimapenzi ovyo akapata mimba ya mtoto wa tatu (u.k 152). Hapa ni kinaya kwa kuwa hatungetarajia Pete kulewa chakari na kujihusisha na mapenzi kwa wanaume ovyo ovyo na kujipata akiwa mjamzito.

Pia ni mtamaushi kwa kuwa baada ya kupata watoto watatu kwa wanaume mbalimbali anakata tamaa na kutaka kijiua ili afe pamoja na mtoto. Anasema:

"…hii ya kuulia panya haitashindwa kunifisha mimi pamoja na kilichomo tumboni" (u.k 152). Hapa ni kinaya kwa kuwa hatungetarajia Pete kunywa sumu ajiangamize pamoja na kile kijusi kilikuwa kwa tumbo lake.

Pia yeye ni mpyoro kwa kuwa anatumia lugha mbaya katika kuwataja watoto wake. Anasema: "*Na usidhani hata kitoto hiki cha pili sikujaribu kukiangamiza… Nilikuwa nimejaribu mara nne kukiavya kwa vidonge, kisikubali"* (u.k 151)

Hiki ni kinaya kwa kuwa hatungetarajia Pete kutumia lugha ya ukali na matusi kuwarejelea watoto wake.

## 5.2 SIFA ZA WAHUSIKA KUBAINISHA KINAYA KWA KIGOGO

Utafiti huu umeshughulikia wahusika ambao wanatenda kiyume na matarajio ya watu au wasomaji. Wahusika hawa ni: Majoka, Kenga, Husda na Mamapima

### 5.2.1 SIFA ZA MAJOKA KUDHIHIRISHA KINAYA

Majoka ni kiongozi tajiri wa jimbo la Sagamoyo. Ni mwanawe marehemu Marara bin Ngao na mjukuu wa marehemu Mzee Ngao. Utafiti huu umeangazia vile Majoka ana sifa hasi ambazo ni kinyume cha matarajio ya wananchi wa Sagamoyo ambao walimteua kama kiongozi wao na pia kwa wasomaji kama zifuatazo:

Katika tamthilia ya *Kigogo* ni bayana kuwa Majoka ni katili kwa kuwa hawahurumii watawaliwa. Anawakandamiza wafanyakazi kwa kuwapandishia bei za vyakula katika kampuni yake. Pili anawaamuru polisi kutumia nguvu kuwatawanya waandamanaji. Isitohe, hababaishwi na kifo cha Ngurumo. Anapoambiwa kuwa hapana nafasi kaburini, anasema kuwa kinba ni kimba tu, azikwe juu ya wenzake (u.k 69). Tatu, anawaagiza askari wamzulie na kumpiga Ashua anapokataa kuwa mpenzi wake licha ya Ashua kujitetea kwamba yeye ni mke wa Sudi. Isitoshe, Ashua ana mtoto mdogo ambaye hata alilala njaa. Matukio haya yanamdhihirisha kama kiongozi katili.

Tena Majoka ni mwenye dharau na matusi kwa kuwa anamdharau Sudi kwa kutamka kauli nyingi za kumdunisha Sudi anapojaribu kushawishi Ashua amkubali. Pia, anawaita watoto wa Sudi vichekechea. Ashua anapomuuliza Majoka kwa nini soko lilifungwailhali wafanyabiashara hulipa kodi, Majoka anasema:

*"Kuna miradi ya hadhi ya kushughulikiwa kuliko hivyo visoko vya kichochole"* (u.k 24)

Anapoambiwa kuwa Sudi na Tunu wanataka kumwona, anamwambia askari, Mwango, kukaa naye ili makunguru wasimdhuru. Anawarejelea Tunu na Sudi kama makunguru

(u.k 38). Tena anawarejelea wapinzani wake Tunu na Sudi kama watoto anapowaita mbu anaposema hawatatumia bomu kuulia mbu. Anamwambia Kenga kina Tunu ni watu wadogo kwa hivyo asichoshe akili bure (u.k 35). Mwishowe, anawatusi Wanasagamoyo Wajinga (u.k 88). Hiki ni kinaya kwa kuwa hatungemtarajia Majoka kuwa na dharau na matusi kwa Wanasagamoyo.

Majoka anajitokeza kuwa ni mwenye taasubi ya kiume kwa kuwa anawaambia Ashua na Husda kuwa hana *time* ya wanawake (u.k 125). Ana mtazamo hasi kwamba wanawake ni watu duni ambao hata hafai kupoteza wakati wake akiwapatanisha; Wanafaa kujipatanisha wenyewe huku wakiteseka kwenye seli.

Husda anapojaribu kujitetea wakati wa mzozo kati yake na Ashua, Majoka anamwambia: "*Shut up woman"* (u.k 27)

Anazungumza na mkewe kwa hasira akimwita *woman* kama aiyejua jina lake.

Tunu anapowahutubia watu, Majoka anakasirika na kumwambia mkuu wa polisi, Kingi, kwamba hataki kuaibishwa na mwanamke. Eti hawezi kumsikiliza mwanamke kama Tunu (u.k 90). Pia anaamini kuwa wanawake wote ni sawa kwa kusema wanaake ni wanawake tu (u.k 27). Hiki ni kinaya kwa kuwa hatungetarajia kiongozi anayewabagua wanawake kwa misingi ya kijinsia.

Katika tamthilia hii ya *Kigogo* Majoka anajitokeza kuwa mjinga kwa sababu anaongoza Sagamoyo kwa kuzingatia ushauri a mzee Kenga bila kutambua kuwa anapotoshwa. Amekuwa kama zuzu asiyepima mashauri ili kuchuja yafaayo. Kwa mfano, Kenga anamshauri amfunge Ashua ili aweze kumshurutisha Sudi kumchongea kinyago naye

anafanya vivyo hivybila kuuliza busara au madhara yanayofungamana na ushauri huo. Kenga anamshauri Majoka:

*"Kubali pendekezo letu la kufungwa kwa soko…huoni kuwa hii ni fursa nzuri ya kulipizia kisasi kwa huyo Sudi na kumnasa Ashua? Najua umekuwa ukimmezea mate…akija ofisini …bila shaka, kutatokea patashika na papo hapo, amuru askari wamtie Ashua nguvuni kwa madai ya kuzua vurugu katika ofisi ya serikali"* (u.k 29)

Hiki ni kinaya kwa kuwa hatungetarajia Majoka kufuata ushauri potovu kutoka kwa washauri wake kwa sababu hatimaye tunawapata Wanasagamoyo wakimtoa uongozini kwa sababu alifeli katika uongozi wake kwa sababu ya kufuata ushauri hasi kutoka kwa Kenga.

Tena tunamwona Majoka akiwa mzinifu kwa sababu ana mke lakini bado anamtongoza Ashua (u.k 29). Mkewe anakiri kwamba haonekani kwake akidhani anashinda na kukesha pamoja na Ashua (u.k 26). Ingawa Ashua hampendi Majoka, kauli za Husda zinaonyesha kuwa anajua Majoka haji nyumbani kwa sababu ya uzinifu; labda anazini na wengine. Hiki ni kinaya kwa kuwa tungetarajia Majoka awe mwaminifu kwa kuwa yeye ni kiongozi ambaye ameheshimiwa na jamii yake na pia ameoa mke anayeitwa Husda na pia ana mtoto kwa jina Ngao Junior.

Mfano mwingine ni kwamba Majoka anajitokeza akiwa muuaji kwa kuwa anawaua watu ovyoovyo, kinyume na sheria kama ifuatavyo:

Anapanga njama ya Jabali kuuawa kutokana na ajali mbaya barabarani. Pia katika maungamo yake akipelekwa hospitalini, nafsi yake inamsuta kutokana na mauaji

aliyotenda; Anasema kwamba damu inamlilia jambo linalomaanisha ameshiriki katika mauaji ya watu wengine bali na Jabali (u.k 73).

Isitoshe, Majoka na Kenga wanapanga kumuua Chopi kwa kuwa aliteleza katika majukumu yake, anafahamu njama zao na wanahofia huenda akazifichua. Tena anamtisha mkuu wa polisi kuwa atauliwa na chatu kwa sababu ya kutomtii kwa kuzingatia anavyomtisha Kingi, huenda yeye '*aliyemtuma*' chatu kumuua Ngurumo kwa sababu Ngurumo aliifahamu mienendo yake katili (u.k 68). Hiki ni kinaya kwa kuwa tungetarajia Majoka kama kiongozi ahakikishe kwamba wananchi wanapata usalama badala ya kutekeleza mauaji ovyo ovyo.

Sifa nyingine ya Majoka ni kwamba yeye ni mnafiki kwa sababu zifuatazo:

Yeye anasema mambo yaliyo kinyume na matendo yake. Anajifanya kuwa na huruma huku akishirikiana na Kenga kuwadhulumu wananchi. Kwa mfano, wamemuua Jabali. Amewaruhusu polisi kuwapiga waandamanaji. Pia, anawaagiza Chopi na Ngurumo kumpiga Tunu hadi wamvunje mguu wa kitamathali yaani wamwangamize (u.k68).

Unafiki wake pia unaonekana anapojidai alimsomesha Tunu kwa insafu ilhali alilazimishwa, kisheria, kufanya hivyo kwa sababu ajali ya Jabali (babaye Tunu) ilitokea akiwa kazini katika kampuni yake. Pia anadai kuwa atatoa chakula cha msaada kwa watu wasiojiweza lakini anakataa kumpa Ashua msaada wa chakula kwa wanawe. Hata keki ya uhuru anatoa tu makombo (u.k 13).

Tena, anapanga kuongeza mishahara ya walimu na madaktari wakati huo huo akiongeza kodi ili pesa hizo zirejee mfukoni mwa serikali; anaingiza kwa kushoto na kutoa kwa kulia (u.k36).Tena namwambia Ashua :

*“Siwezi kukudhuru; kitu aali na cha tunu kama wewe”* (u.k 20)

Baadaye anamwita anamwita mkewe Husda) ili aje apigane na Ashua mwenye udhaifu wa mwili kutokana na njaa. Mwishowe anawaruhusu askari kumpiga Ashua hadi kumjeruhi.

Anamwambia Ashua:

“*Haja zako ni haja zangu, shida zako ni shida zangu na kiu yangu ni kiu yako*” (u.k 23) lakini hamsaidii bali anataka Ashua ajihusishe naye kimapenzi ili akubali kumsaidia. Kupitia matukio haya, inajitokeza kwamba Majoka alikuwa anajifanya mzuri sana kwa Ashua lakini kumbe alikuwa chui ambaye amevalia ngozi ya chui lakini hataki kudhihirisha unafiki wake hadharani.

Tena, tunamwona Majoka akiwa mbinafsi kwa kuwa anapanga kufunga runinga ya Mzalendoile lilikuwa inamsifu Tunu ambaye alikuwa mpinzani wake ili yake ibaki pekee (Sauti ya Mashujaa) ili iwe inamsifu kuwa yeye pekee ndiye mwajibikaji hapo Sagamoyo. Jambo hili linajitokeza kwa sababu mbali na kuogopa ushindani na maovu yake kufichuliwa, amejazwa na wivu kwa Tunu kwa kuwa mpinzani wake (u.k 17).

Pia yeye ni mchonganishi kwa kuwa anasababisha ugomvi kati ya mkewe na Ashua kwa makusudi kwa sababu Ashua alikataa kutimiza matakwa yake kwa mfano, kufanya naye mapenzi, kuajiriwa katika shule yake, na kwa kushinikiza Sudi amchongee kinyago (u.k 28).

Yeye ni msaliti kwa sababu zifuatazo:

Alimsaliti babaye Tunu kwa kuwa alifia katika kampuni yake kwa njia tatanishi na Majoka akakataa kumpatia fidia ingawa awali,walikuwa marafki wa karibu; walikuwa kama ndugu wa toka nitoke (u.k39).

Tena anawasaliti wanaSagamoyo kwa kuwakandamiza na kuyatelekeza majukumu ya kuhakikisha kuwa soko lao ni safi na wanalindwa ipasavyo. Pia anamsaliti Ashua anayedai kumpenda kwa kumtia kizuizini badala ya kumpa msaada aliokuja kuomba.

Isitoshe,anamsaliti Ngurumo kwa kutomzika kiheshima na kumwomboleza kwa heshima anaponyongwa na chatu ilhali alikuwa mfuasi wake mkuu na hata alimsaidia kuwaangamiza wapinzani wake hapo awali. Tena ana nia ya kumsaliti Chopi kwa kumuua kwa madai kwamba yeye anatelekeza majukumu yake kama vile hakumuua Tunu kama ilivyopangwa ilhali Chopi amemhudumia kwa uaminifu katika uongozi wake (u.k70). Hapa kinaya kinajitokeza pale hatungetarajia Majoka kuwasaliti Wanasagamoyo kwa kuwatendea maovu na alikuwa amewaahidi ahadi nyingi ambazo hakuzitimiza.

Tena Majoka anajitokeza kama mhusika mwoga kwa kuwa anapoambiwa na Chopi kuwa Sudi na Tunu wanataka kumwona, anamwambia askari, Mwango, akaye naye mle ofisini ili kina Tunu wasimdhuru ilhali ana bastola (u.k38). Hapa ni kinaya kwa kuwa hatungetarajia kiongozi Majoka awaogope akina Sudi na alikuwa anawatusi kunguru.

Majoka pia ni mwenye hila kwa kuwa tunamwona akiwadanganya Wanasagamoyo kwamba wamelifunga soko la Chapakazi ili walisafishe kwa kuwa ni chafu sana. Hapa ni kinaya kwa kuwa analinyakua soko hilo na kujenga hoteli la kifahari huku akiwaacha wachuuzi kuteseka.

Majoka ni mwenye tamaa kwa sababu ya matendo yake yafuatayo:

Ana tamaa ya kimapenzi. Licha ya kuwa amemwoa Husda, angali anataka kushiriki mapenzi na wake wa wengine. Ashua anaposema kuwa yeye ni mke wa mtu, Majoka anamwambia kuwa hataacha kula mkate kwa kuchelea kiungulia (u.k 23). Anaonyesha kuwa hajali ikiwa Ashua ana mume au la; anachotaka ni uroda. Pia, Kenga anamwambia Majoka:

*"Najua umekuwa ukimmezea mate.*"(u.k29)

Tena anataka kumrithi Hashima, mamaye Tunu, Jabali alipoaga dunia lakini Bi. Hashima akakataa. Hii ni tama ya mapenzi kwani Majoka ana mke wake aitwaye Husda na mtoto wake Ngao Junior. Pia ana tamaa ya kujilimbikizia mali bila kujali maslahi ya watawaliwa. Kwa mfano analifunga soko la Chapa kazi kwa madai kwamba anataka kulisafisha ilhali alikuwa na tamaa ya kulinyakua na kujijengea hoteri yake ya kifahari

Pia Majoka ni mbadhirifu kwa sababu zifuatazo:

Anaharibu mali za umma. Anafuja pesa za umma zilizotengewa usafishaji wa soko la Chapakazi kupitia kwa madai ya Tunu kupitia kwa kauli ya Kenga yanathibitisha haya. Tunamwona pia akitumia pesa nyingi kuandaa sherehe ya uhuru badala ya kuzitumia kuwafaa wananchi (u.k 4).

Tena Majoka ni mshirikina kwa sababu zifuatazo:

Amefuga swila ambaye humpeleka hata ofisini na anatumia chatu kuwadhuru watu. Katika utamaduni wa Kiafrika, mfugaji nyoka huaminika kuwa mshirikina, ndio maana ana uwezo wa kuwafanya nyoka hao wamtii na kuwaua watu.

Tena, anaamini kwamba ndoa ya Sudi imejengeka kwa msingi wa ushirikina. Anasema kwamba mwanamke mrembo kama Ashua hawezi kuolewa na maskini Sudi ila kwa kuzungushiwa Ndonga (u.k 24).

Majoka ni mtelekezi wa majukumu kama ifuatavyo:

Hajali maslahi ya watawaliwa. Anafuja pesa za kusafisha soko la umma na kujijengea hoteli ya kifahari huku akihatarisha maisha ya wachuuzi waliokuwa wanalitegemea soko hili kwa sababu ya mtaji wao, Anapuuza majukumu yake ya ndoa kwa kutoonekana nyumbani kwa muda mrefu na ameruhusu uvunjaji wa sheria kwa kumpa Mamapima kibali cha kuuza pombe haramu inayowapofusha na kusababisha wengine kupoteza maisha yao.

### 5.2.2 SIFA ZA KENGA KUDHIHIRISHA KINAYA

Kenga ni binamuye Majoka. Yeye ni mzee mshauri wa Majoka. Ndiye mratibu na mtekelezaji wa miradi mbalimbali ya kiongozi wa Majoka. Anahusika katika upangaji na uandalizi wa shughuli za siku ya sherehe za kuadhimisha miaka sitini ya uhuru wa Sagamoyo. Utafiti huu umedhihirisha sifa hasi za Kenga ambazo ni kinyume cha matarajio ya wanaSagamoyo na pia wasomaji wa tamthilia ya Kigogo kama zifuatazo:

Yeye ni katili kwa kuwa anatenda matendo yafuatayo:

Anapanga kuwaangamiza wapinzani wa Majoka. Anashirikiana na Majoka kumuua mpinzani wao, Jabali pia yeye na Majoka wanapanga kuwawekea kina Tunu (watu wanaopinga uongozi mbaya) vidhibiti mwendo na hata kuwaangamiza kabisa kama njia ya kuwanyamazisha ili kuendeleza utawala mbaya.

Majoka anamwambia Kenga kuwa yeye ni hatari (u.k 35). Tena anajitokeza akimtisha Sudi kwa kumwambia achunge ulimi usije ukamtoma katika bahari mchafukoge. Yeye na majoka wanapanga kumuua Chopi kwa kuwa aliteleza katika njama ya kumwangamiza Tunu nb ssa kuwa anafahamu njama zao kwa hivyo huenda akatoboa siri zao. Hiki ni kinaya kwa kuwa hatungetatajia Majoka kuwa katili kwa kuwa kama kiongozi anafaa kulinda usalama wa wananchi lakini si kuwaangamiza.

Tena Majoka ni mwenye mapuuza kwa kuwa anapuuza umaarufu wa kina Tunu akidai gazeti lililochapisha habari hizo linawapendelea. Hata hivyo, umaarufu wa wanaharakati hao unadhihirika baadaye kwa kuwa Tunu alimshinda Majoka kwenye uchaguzi (u.k38). Kenga pia ni mtelekezi wa majukumu kwa sababu zifuatazo:

Majoka anapomuuliza Kenga kuhusu wafadili wa gazeti lililoandika kuwa asilimia zaidi ya sitini ya watu inamuunga mkono Tunu, Kenga anamuuliza majoka:

*"…Na mwamba ngoma huvutia wapi*?" (u.k33).

Anatumia methali hii kuonyesha maoni hayo yanaegemea upande mmoja. Ni mbinu yake kumliwaza na kumfumba macho Majoka ili kumhakikishia angali maarufu. Mambo yanamwendea kombo watu wanapohudhuria mkutano wa hadhara ulioitishwa na Tunu.

Anamwambia Majoka kuwa dalili ya mvua ni mawinguu.k34. Hapa ni pale anahisi kuwa Tunu anazidi kupata umaarufu na huenda akamng'oa Majoka mamlakani wasipochukua hatua. Tena, anamshauri Majoka kuwaalika Ashua na Husda ofisini mwake ili itokee rabsha kasha amtie Ashua mbaroni kwa kupata fursa ya kumshurutisha Sudi achonge kinyago kama sharti la kuachhiliwa huru kwa mkewe. Huu si ushauri bora unaoweza kutolewa na kiongozi wa umma anayewajibika kazini.

Maandamano yanayoongozwa na kina Tunu yanapopeperushwa moja kwa moja katika runinga na mitandao ya kijamii, Kenga anamwambia Majoka:

“*Udongo tungeuwahi uli mbichi. Limekuwa donda dugu sasa*”(u.k35)

Anamtanabahisha Majoka kuwa umaarufu wa Tunu umekwisha kukita mizizi na huenda hawatafaulu kumkomesha. Matamshi yake yanakinzana kwani awali alipuuza taarifa kuwa asilimia zaidi ya sitini inamuunga mkono Tunu. Hali hii inadhihirisha utepetevu kazini; hatoi mashauri ya hakika, yanayumbayumba. Hiki ni kinaya kwa sababu tunapata kwamba hakuwa anafanya uchunguzi kuhusu umaarafu wa Tuni kisiasa na mwishowe Tunu anamshinda Majoka kwenye uchaguzi.

Kenga ni mnafiki kwa sababu zifuatazo:

Anamwita Majoka shujaa ilhali Majoka hana sifa zozote za ushujaa. Anawaita kina Sudi waungwana ilhali wanawapa makombo ya keki na hata kupanga njama ya kuwaangamiza. Pia anaposoma taarifa kuhusu kuongezeka kwa umaarufu wa Tunu kuwa zaidi ya asilimia sitini ya watu iko tayari kumpigia kura, anazipuuza taarifa hizo akidai gazeti hilo limefadhiliwa na wafadhili wanaounga mkono upinzani, badala ya kufanya uchunguzi na kubuni mikakati kabambe ya kuwawezesha kuepuka kupoteza umaarufu. Umaarufu wa Tunu unaongezeka mpaka siku ya kusherehekea uhuru, watu wanadinda kuhudhuria maadhimisho na badala yake wanahudhuria mkutano wa hadhara unaoandaliwa na Tunu (u.k 28). Hiki ni kinaya pale ambapo tunamwona Kenga akimhadaa Majoka kwamba ana umaarufu Sagamoyo na anaendelea kugawiwa mali ya umma na mwishowe Majoka anashindwa na Tunu.

Kenga ni mwenye dharau kwa kuwa anamdharau Sudi anposema.

*"Huo ujasiri wenu wa peni tisa". Pia anawapa kina Boza makombo ya keki. Anaidharau elimu ya Tunu ambayo haijamwezesha kupata ajira*" (u.k13)

Hiki ni kinaya kwa kuwa Kenga alikuwa anamrai Sudi kumchongea kinyago kwa sababu ya uchongaji wake wenye umaarufu kuliko wachongaji hao wngine.

Kenga pia ni mjinga kwa kuwa hatambui maana fiche ya urembo wa nafsi. Anasema kuwa urembo ni wa nje pekee. Hamtambui shujaa ambaye Sudi anamchonga, ilhali ni mtu anayemjua Tunu (u.k 10). Hiki ni kinaya kwa kuwa anasema hajui Tunu msichana ambaye alikuwa maarufu sana kisiasa ukimlinganisha na Majoka.

Kenga ni mwenye matusi pale anamwita Tunu hawara wa Sudi. Kenga anamwambia Sudi, "*Umelishwa kiapo na huyo hawara wako, sio*?" (u.k12)

Hapa ni kinaya kwa kuwa Tunu hakuwa na uhusiano wowote wa kimapenzi na Sudi kwa kuwa Sudi alikuwa na mkewe Ashua na watoto wawili na tena hakuwa mzinifu.

### 5.2.3 SIFA ZA HUSDA KUDHIHIRISHA KINAYA

Ni mkewe Majoka. Ana mwana mmoja; Ngao Junior. Aliozwa kwa Majoka licha ya Majoka kutompenda kwa kuwa Majoka alitaka kuchaguliwa kama kiongozi wa jamii ya Sagamoyo. Utafiti huu umedhihirisha sifa hasi za Husda ambazo ni kinyume cha matarajio ya wanasagamoyo na wasomaji wa tamthilia ya Kigogo kama zifuatazo:

Ni mwenye dharau kwa kuwa anamdunisha Ashua kwa kusema: "*Umeshindwa kufuga kuku, kanga wafikiri utamweza*"(U.K28)

Kinaya kinajitokeza pale tunaona kwamba anamsingizia Ashua kuwa ana uhusiano wa kimapenzi ilhali Ashua alikuwa mwaminifu na alikuwa ameiheshimu ndoa yake kati yake na Sudi.

Yeye ni mnafiki kwa kuwa Majoka anadokeza kuwa yeye ni mnafiki kwa kumwita "*Chui anayeishi ndani ya ngozi ya kondoo"* (u.k75)

Hiki ni kinaya kwa kuwa Husda hakuolewa kwa Majoka kwa sababu ya mapenzi bali alitamani mali yake.

Yeye ni mdaku kwa kuwa Ashua anasema:

"*Ya wenziwe hadharani, yake faraghani. Nani asiyemjua mkeo mdaku, msambaji wa kanda za umbeya kwenye vikao vya masengenyo*" (u.k28)

Jambo hili ni kinaya pale hatungetarajia mke wa kiongozi kumsimanga Ashua kwamba anajihusisha kimapenzi na mumewe Majoka jambo ambalo si ukweli kwa kuwa Ashua hakuwa na uhusiano wa kimapenzi na Majoka.

Husda ni mgomvi kwa kuwa anazua fujo anapomfumania Ashua katika ofisi ya Majoka, hata baada ya Ashua kumweleza hana uhusiano wowote wa kimapenzi na mume. Anasema:

"*Leo nitaua mtu mie*" (u.k 26)

Hiki ni kinaya kwa sababu hatungetarajia Husda kumtusi Ashua hawara na kumsingizia kwamba ana uhusiano wa kimapenzi na mumewe jambo ambalo si la ukweli. Tena Husda ni mwenye tama ya mali. Majoka anasema kuwa hampendi kwa dhati bali anazipenda tu mali zake.

Majoka anasema: "*Nyanya tafadhali. Husda hanipendi. Anazipenda mali zangu. Hayo siyo mapendo ya dhati"* (u.k 75)

Pia Husda ni mwenye husuda kwa kuwa mumewe Majoka anasema kwamba jina lake Husda, linaiakisi tabia yake ya kupenda mali na kutoyafurahia mafanikio ya wengine (u.k 75). Hapa kinaya kinajitokeza pale tunampata Husda hapendi mafanikio ya watu wengine jambo ambalo ni kinyume cha matarajio yetu kwa kuwa tungetarajia akifurahia ufanisi wa watu wengine kama alivyokuwa mke wa kiongozi.

Pia tunagundua ya kwamba Husda ni mzinzi. Katika tamthilia hii ya *Kigogo*, tumeelezwa na mwandishi kwamba Husda anamtazama Chopi kwa macho ya uchu (u.k 70). Hiki ni kinaya kwa sababu hatungetarajia yeye awe na tamaa ya wanaume wengine na ameolewa na Majoka.

Isitoshe, Ashua anajitokeza kama mwenye hasira pale ambapo tunaona ya kwamba akipandwa na hasira na kumgombeshana kumpiga Ashua anapompata katika ofisi ya Majoka. Anaendelea kumwambia ya kwamba anaweza kumuua Ashua na kumtusi pwagu (u.k 27).

### 5.2.4 SIFA ZA MAMAPIMA KUDHIHIRISHA KINAYA

Jina lake halisi ni Asiya. Ni mkewe Boza japo anashiriki mapenzi na Ngurumo, mmoja wa wateja wake. Ana kibali cha kutengeneza na kuuza pombe haramu.Yeye ndiye anayepata kandarasi ya kuoka keki za sherehe. Utafiti huu utadhihirisha sifa hasi za Mamapima ambazo ni kinyume cha matarajio yetu kama zifuatazo:

Mamapima ni mzinifu kwa kuwa anajihusisha kimapenzi na Ngurumo. Anatekeleza uhawara huo ili apendekezwe na Ngurumo kwa Majoka kiongozi wa Sagamoyo ili apewe kandarasi ya serikali ya kuoka keki (u.k 64)

Hiki ni kinaya kwa kuwa hatungetarajia mamapima kujihusisha kimapenzi na wanaume wengine na yeye ameolewa na ana bwana.

Mamapima anajitokeza kuwa mhalifu kwa kuwa amepata kibali cha kuuza pombe haramu ambayo imefanya wengi wapofuke na wengine kuaga dunia (u.k 62). Hatungetarajia yeye kuuza pombe haramu lakini anafanya biashara hii ili ajitajirishe na wanunuzi wage dunia.

Pia anajitokeza kama mwenye matusi kwa kuwa katika wimbo wake wa uchokozi, anamtukana Sudi kuwa ana mdomo uliojitokeza mbele kama wa mbweha, yaani Sudi ana maneno mengi yasiyofaa (u.k61). Hiki ni kinaya kwa kuwa hatungetarajia Mamapima kumtusi Sudi kuwa ana mdomo kama wa mbweha.

Tunamwona Mamapima akiwa mchokozi pale anaongoza na kuchochea walevi kuwaimbia Tunu na Sudi wimbo wa kinaya (u.k 60). Hapa ni kunaya kwa kuwa hatungetarajia yeye awachokoze akina Tunu na hawakua wamemfanyia vibaya.

Tena, hatungetarajia Mamapima kuwa mvunjasheria. Kwa mfano anavunja sheria kwa kuuza pombe haramu japo anafahamu madhara ya pombe hizo (u.k 61).

Kwa upande mwingine anajitokeza akiwa mwenye hasira pale tunaona ya kwamba

wateja wake wawili walipoondoka baada ya Tunu na Sudi kuwashawishi kuwa walikuwa wanakunywa pombe haramu, anawaonya kina Tunu kuondoka maskani yake au wajue kwa nini anaitwa Mamapima (u.k62).

Hiki ni kinaya kwa kuwa hatungetarajia Mamapima kuwafukuza kina Tunu kwa sababu walikuwa wanaelezea walevi ukweli kuhusu ukali ya kunywa pombe haramu.

# SURA YA SITA

# HITIMISHO

## 6.0 MUHTASARI NA MATOKEO YA UTAFITI

### 6.1 UTANGULIZI

Sura hii imeshughulikia muhtasari wa utafiti mzima kuanzia sura ya kwanza hadi ya mwisho. Aidha, sura hii imetoa matokeo ya utafiti kupitia ugunduzi mbalimbali ambao umetokana na uchunguzi kuhusu kila lengo la utafiti kwa kuzingatia misingi ya nadharia za utafiti. Vile vile, sura hii imetoa changamoto katika utafiti huu na mapendekezo ya masuala muhimu ambayo yanaweza kuwa kichocheo cha uchunguzi mwingine zaidi kuhusu fasihi ya Kiswahili kwa ujumla. Kutokana na uchanganuzi wa data iliyotokana na riwaya na tamthilia teule ambazo ni *Chozi la Heri* na *Kigogo,* imebainika kwamba mbinu ya kinaya imetumika kuendeleza maudhui katika katika kazi hizi teule za kifasihi.

### 6.1 MUHTASARI WA TASNIFU

Utafiti huu ulidhamiria kuchunguza kinaya vile kimetumika kubainisha maudhui katika riwaya ya Matei (2015) na tamthilia ya Kigogo (2017). Ari ya kufanya utafiti huu ilitokana na sababu ya waandishi wa riwaya na tamthilia teule kuangazia mbinu ya kinaya kwa kina ingawa vitabu hivi viliandikwa nyakati tofauti. Isitoshe mbinu ya kinaya ni muhimu sana ambayo hutumiwa na waandishi wengi kuelezea mambo ambayo ni kinyume cha matarajio ya watu ingawa si kwa njia ya moja kwa moja. Mbali na hayo, riwaya na tamthilia hii ni kati ya zile zimewahi kuteuliwa ili zihakikiwe na kutahiniwa katika shule za upili nchini Kenya na kwa hivyo hadhira yake ni kubwa.

Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni ya uhakiki wa kimtindo. Nadharia hii, ilisaidia sana kuchunguza mbinu ya kinaya katika riwaya na tamthilia husika. Mbinu zilizotumika kuafikia malengo ya utafiti ni kusoma riwaya na tamthilia teule kwa kina na kuchanganua mbinu ya kinaya na ikabainika kuwa maudhui na sifa za wahusika hujengwa na mbinu hii.

**6.2 MATOKEO YA UTAFITI**

Utafiti huu ulibaini kwamba kuna aina mbalimbali za kinaya katika fasihi ya Kiswahili kama vile: Mazungumzo, drama, hali, kisokratia na kilimwengu. Katika utafiti huu, vinaya cha drama, mazungumzo na hali ndivyo vimeangaziwa katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo* kwa kuwa kazi hizi mbili zina utajiri wa mbinu hii. Mfano wa kinaya cha hali ni pale tunampata kijakazi Sauna ambaye alikuwa akijifanya mwaminifu kwa waajiri wake na baadaye anawatorosha watoto wao. Wakati Naomi alitoroka nyumbani mwake na kumwacha Sauna kuwalea watoto wake ambao ni Dick,Umu na Mwaliko, anajiaminisha kwao na kisha kuwateka nyara Dick na Mwaliko. (u.k 98)

Utafiti huu kisha umeangazia vile kinaya kinatumika kuendeleza maudhui mbalimbali katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo.* Maudhui ambayo yanashughulikiwa katika kazi hizi teule ni:Uongozi mbaya, ufisadi, ukatili na unafiki. Kwa mfano katika tamthilia ya *Kigogo*, kuna ufisadi pale ambapo tunawaona viongozi wakitumia vitisho kuwanyang'anya wafanyabiashara mali zao. Mfano unajitokeza pale ambapo tunamwona Majoka akifunga soko la Chapakazi ili ajenge hoteli ya kifahari na akawafurusha wafanyabiashara kama vile Ashua na Sudi. (u.k 3)

Utafiti huu pia umebainisha vile kinaya kimetumika katika kujenga sifa za wahusika katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo.* Mfano, Majoka ambaye ni

kiongozi wa Sagamoyo, anajisifu kwamba yeye ni mwenye utu lakini kupitia kwa kinaya anajitokeza akiwa katili kwa sababu anamwangamiza Jabali ambaye alikuwa mpinzani wake kupitia ajali mbaya barabarani. (u.k 26)

## 6.3 MCHANGO WA UTAFITI

Kutokana na kazi hii, tumebaini kwamba katika uandishi wa kazi za kifasihi, lugha ni nyenzo kuu na muhimu katika kuwasiliosha ujumbe wa mtunzi. Tumegundua kwamba, dhamira na maudhui ya mtunzi haziwezi kuwasilishwa vizuri bila ubunifu wa hali ya juu wa matumizi ya lugha. Aidha, utafiti huu umedhihirisha uhusiano uliopo kati ya ujumbe wa mwandishi na lugha ya kinaya, hivyo, lugha ya kinaya ikitumiwa vizuri hufanikisha kazi za mtunzi.

Hali kadhalika kutokana na utafiti wa riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo*, tumeweza kushadidia msingi uliowekwa na watafiti wengine walioshughulikia riwaya na tamthilia hizo. Kazi hii hasa , imeweza kudhibitisha kuwa Matei na Kea wana upekee na ubunifu wa hali ya juu katika matumizi ya mbinu ya kinaya.

## 6.4 CHANGAMOTO

Kutokana na kazi hii tulikabiliana na tatizo la ukanganyifu wa mbinu ya kinaya. Katika utafiti huu tuligundua kuwa dhana ya kinaya inakanganya kwa jinsi wataalamu mbalimbali wanafafanua mbinu hii. Baadhi ya wataalamu wengine wanafafanua kinaya kama mbinu moja finyu ya kuwasilisha ujumbe kwa kutumia kinyume cha matarajio. Utafiti huu ulishughulikia mbinu ya kinaya vile kimetumika katika kubainisha maudhui mbalimbali katika riwaya ya *Chozi la heri* na tamthilia ya *Kigogo.*

Aidha tulikumbana na tatizo la tafsiri. Tatizo hili lilijitokeza sana hasa katika kushughulikia nadharia. Machapisho katika lugha ya Kiswahili yanayozungumzia nadharia ya kimafumbo ya kisasa hayapo. Ililazimu kutegemea machapisho na vitabu vya kiingereza kupata data toshelevu. Aidha, haikuwa rahisi kupata baadhi ya visawe ili kupata maana kamili kwa sababu baadhi ya visawe vilipoteza maana wakati wa kutafsiri. Hata hivyo, mtafiti alitumia kamusi mbalimbali pamoja na kutafuta usaidizi kutoka kwa watwalamu wa lugha, ili kusuluhisha tatizo hili.

## 6.5 MAPENDEKEZO

Utafiti huu umelenga kuchunguza matumizi ya mbinu ya kinaya kubainishia maudhui katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo.* Hata hivyo kuna mambo mengine ambayo utafiti haujashughulikia na yanaweza kushughulikiwa na watafiti wengine.

Mtafiti mwingine anaweza kufanya kufanya utafiti kuhusu mbinu zisizo za kinaya katika riwaya ya *Chozi la Heri* ya na tamthilia ya *Kigogo* kwa kutumia nadharia ya kimtindo, sehemu hii haijafanyiwa utafiti wa kina na itakuwa na manufaa kwa wasomi wa lugha ya Kiswahili.

Vilevile, mtafiti anaweza kulinganisha na kulinganua wahusika katika riwayaya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo*, kwani zilitungwa katika nyakati tofauti . Mtafiti anaweza kutumia nadharia ya uhakiki wa kimtindo au nyingine yoyote inayohusu mbinu za lugha.

## 6.6 HITIMISHO

Utafiti huu uliongozwa na maswali matatu. Kwanza: Je, aina zipi za kinaya zimejitokeza katika riwaya na tamthilia teule? Utafiti huu umebaini kuwa mwandishi amefaulu kusawiri aina tano za kinaya katika kazi ya fasihi. Aina hizi ni kinaya cha: Drama, hali

maigizo, kisokrasia na kilimwengu. Utafiti huu ulichunguza kinaya cha drama, hali na cha mazungumzo katika riwaya ya *Chozi la Heri* na tamthilia ya *Kigogo*. Mfano wa kinaya cha mazungumzo unajitokeza pale Majoka anaonekana akizungumza mambo ambayo ni kinyume na matendo yake aliyokuwa akifanya. Mfano anamwita Tunu kigogo mtarajiwa lakini tunaona kwamba hakuwa anapenda Tunu awe kiongozi kupitia njama yake ya kuuawa kwa Tunu. Pia kinaya cha mazungumzo kinajitokeza pale tunamwona Majoka akimwambia Ashua anampenda lakini alisema hivyo kwa kuwa alitaka kufanya naye mapenzi na wakati Tunu anakataa kufanya naye mapenzi anamfunga jela bila makosa yoyote. Pia katika riwaya ya *Chozi la Heri*, kinaya cha hali kinajitokeza pale ambapo watu wanapitia hali mbaya za maisha kama vile umaskini, njaa, ukosefu wa makao, utengano kwa wanandoa na mauaji ya kiholela. Hali hizi mbaya zimesababishwa na viongozi waliowachagua na pia marafiki zao jambo ambalo ni kinyume cha matarajio yao.

Lengo la pili lilikuwa kutathmini vile kinaya kimetumika katika kuendeleza maudhui mbalimbali.Utafiti huu umeonyesha kwamba, kinaya kimetumika kubainisha maudhui mbalimbali katika riwaya na tamthilia teule. Hili linajitokeza pale ambapo tunaona viongozi na baadhi ya wahusika wengine, wakiendeleza maudhui hasi mbalimbali jambo ambalo ni kinyume cha matarajio ya watu. Maudhui haya hayajaelezwa moja kwa moja bali ni kwa kinaya na inambidi msomaji kuwa makini ili kuelewa vile maudhui haya yanavyoendelezwa na mbinu ya kinaya. Utafiti huu umeangazia maudhui kama vile: Uongozi mbaya, ufisadi, ukatili na unafiki. Kwa mfano Majoka anaendeleza maudhui ya ukatili anapowaagiza walinda usalama kuwaua watu ovyo ovyo. Kwa mfano waandamanaji watano wanauawa kiholela na askari kupitia maagizo ya Majoka.

Tatu: Kutathmini vile kinaya kimejitokeza kutathmini sifa za wahusika katika Riwaya ya *Chozi la Heri* na Tamthilia ya *Kigogo.* Utafiti huu umebaini kuwa waandishi wa Riwaya na Tamthilia teule wameelezea sifa za wahusika kama hasi lakini si kwa njia ya moja kwa moja bali kwa kutumia mbinu ya kinaya. Wahusika wanaonekana wakitenda maovu jambo ambalo ni kinyume cha matarajio ya wasomaji. Baadhi ya wahusika ni viongozi ambao wanatenda maovu kama vile; Mauaji ya watu kiholela, unyang'anyaji wa mali ya umma, udanganyifu na uzinzi. Mfano unajitokeza pale ambapo Majoka anasema hadharani kwa Ashua kuwa hatakosa kuwa mzinzi hata kama ameoa.

# MAREJELEO


Ali, J.N. (2015). *Matumizi ya kinaya katika ushairi wa Kithaka wa Mberia.* Tasnifu ya uzamili chuo kikuu cha Kenyatta.

Chimerah, R. (2014). *Ufundishaji wa fasihi: Nadharia na mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Coombes, G. (1953). *The penguin dictionary of literary terms and literary theory*. Heinemann Kenya.

Chapman, N. (2012). *The language of English literature*. London: Edward Arnold.

Haji, M. (2022). Kuchunguza Matumizi ya Semi zilizoandikwa katika Kuta za Nyumba za Vijiji: Mfano Kutoka Pemba (Doctoral dissertation, The Open University of Tanzania).

Hussein, E. (1971). *Ufundi wa Abdulla katika uchambuzi wa maandishi ya Kiswahili*. Nairobi: OUP.

Kamachu, J. (2015). *Matumizi ya mafumbo katika riwaya za Mafuta na Walenisi*. Nairobi Focus Publishers.

Kamau, M. (1992). *"Ufundi katika riwaya za Mohammed Said Abdalla"*. Tasnifu ya M. A. Chuo kikuu cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa).

Publishers Ltd.

Kamunde, M. (1983). Vitendawili: *Fani ya fasihi simulizi.* Mulika, nambari 13, u.k 21-28.

Katola, E. (2006). *Udhalimu dhidi ya wahusika wa kike katika tamthilia za Kiswahili*. Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kairu, S. (2007). *Taswira ya mwanamke katika tamthilia za Kikenya*. Makala ya Baragumu. Jarida la chuo kikuu cha Maseno.

Kea, P. (2016). Kigogo. Nairobi: Story Moja Publishers.

Kibutu, S.W. (2013). *Vitendawili*. Nairobi: Oxford University Press.

Kilonzo, P. na Masaku, G. (2017). Mwongozo wa tamthilia ya Kigogo. Nairobi. Globalink

Kisiroche, R. (2008). *Uchambuzi wa fasihi.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Leech, G. H. na Short, M. H. (2007). *Style in Fiction*. *A linguistic English fiction prose.* England: Longman group limited.

________ (1969). *A linguistic guide to English poetry*. London: Longman.

Materu, M. I . (1987). *Tanzu na fani za fasihi simulizi*. Mulika u.k. 19. TUKI. Dar es Salaam.

Matei, K. A. (2017). Chozi La Heri. Nairobi.Publishing and Media Services.

Masinde, E. (2007). *Ufundishaji wa ushairi katika shule za upili na vyuo*. Nairobi. Taaluma Publishers.

Musembi, N. (2008). *Matumizi ya taswira na ukinzano kama kichocheo cha zinduko katika riwaya za G. K. Mkangi Mafuta (1984) na Walenisi* (1995).Tasnifu ya M.A. chuo kikuu cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa).

Mbatiah, M. (2000). *Kamusi ya fasihi.* Nairobi: Standard textbooks graphics and publishing limited.

Miriji, T. (2005). *Mtindo katika pungwa ni hatua katika kuwasilisha ujumbe.* Tasnifu ya uzamili, chuo kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

M'Ngaruthi, T. K. (2008). *Fasihi simulizi na utamaduni.* Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Msokile, M. (2013). *Stylistic criticism and the African novel*. London: Heinmann.

Mutiso, K. (2005). *The nature of forbidden language*; A paper presented at the symposium organized by university of Nairobi.

Ndumbu, M. J. (2012). Matumizi ya takriri na sitiari katika utenzi wa Rasi'Ighuli. Tasnifu ya uzamili, chuo kikuu cha Nairobi.

Njogu, K. (2008). *Uhakiki wa riwaya za visiwani Zanzibar*. Nairobi: Nairobi University Press.

Ngara, E. (2011) . Stylistic criticism and the African novel. London: Heinmann.

Njogu, K. na Chimera, R. (2014). *Ufundishaji wa fasihi, nadharia na mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ngure, A. (2007). *Fasihi simulizi kwa shule za sekondari*. Nairobi. Phoenix Publishers Ltd.

Nyanchama, M. (2004). *Matumizi ya taswira na ishara katika Sauti ya Dhiki.* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa).

Oiko, F. G. (2017). Uhakiki Wa Mtindo Katika Tamthilia Za Arege (Doctoral dissertation).

Okwena, S. (2013). *Matumizi ya jazanda katika tamthilia za Arege*. Tasnifu ya uzamili, chuo kikuu cha Kenyatta. Uhakiki wa tamthilia, historia na maendeleo yake. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Oyoyo, J.O. (2013). *Uhakiki wa fani katika ngano tano za Kiswahili.* Tasnifu ya uzamili, chuo kikuu cha Nairobi.

Osore, F. (1994). *Tamrini za fasihi simulizi*. Dar es Salaam: Business Printers Ltd.

Senkoro, F. E. M. K. (1982). Fasihi. Dar - es - salaam: Press and Publicity Center.

Simpson, P. (2004). *Stylistics: A resource book for students.* London: Routledge.

TUKI. (2006). *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za uhakiki wa fasihi*. Nairobi: JKF.

Wanyama, A. (2007). *Maudhui na mtindo katika utendi wa Khuswala Kumuse.* Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. Nairobi. (Haijachapishwa).

Weche, M. O. (2000). *Children`s literature as an image force.* A case study of Ezekiel Alembis books, M.A. Thesis Kenyatta University.


Wamitila, K.W. (2000). *Uhakiki wa fasihi*, *Misingi na vipengele vyake*. Nairobi; Phoenix publications Limited.

Wamitila K.W, (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istiari na nadharia*. Nairobi; Focus Publishers.

Wamitila K.W, (2004). *Kichocheo cha fasihi simulizi na andishi*. Nairobi; Focus Publishers.


Wamitila K.W, (2008). *Kazi ya fasihi: Misingi ya uchanganuzi wa fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.

**KIAMBATISHO 1**
**JALADA LA RIWAYA YA CHOZI LA HERI**



**KIAMBATISHO2**

**JALADA LA TAMTHILIA YA *KIGOGO***



# KIAMBATISHO III LESENI YA UTAFITI

REPUBLIC OF KENYA

NACOSTI

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: **138063**

Date of Issue: **30/June/2023**

## RESEARCH LICENSE



**This is to Certify that Ms.. MILKA mwaniki wanjugu of Karatina University, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Nyeri on the topic: MATUMIZI YA KINAYA KUBAINISHIA MAUDHUI KATIKA FASIHI YA KISWAHILI:MIFANO KUTOKA CHOZI LA HERI NA KIGOGO for the period ending : 30/June/2024.**

License No: **NACOSTI/P/23/27041**

**138063**

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR
SCIENCE,TECHNOLOGY &
INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

**See overleaf for conditions**

National Commision for Science, Technology and Innovation -